

**MCHANGO WA MASHAIRI YA BI MADINA ALI EL-BUHRIY KATIKA
ARUDHI YA KISWAHILI**

JOYCE KAGUO

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA, IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA
KUPATIYA SHAHADA YA UZAMILI (KISWAHILI FASIHI) YA CHUO
KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2015

UTHIBITISHI WA MSIMAMIZI

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma Tasinifu hii iitwayo “*Mchango wa Mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy Katika Arudhi ya Kiswahili Tanga*” na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....

Prof. Dkt. Sheikh, T.S.Y.M Sengo

(Msimamizi)

.....

Tarehe

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama yote au sehemu ya Tasinifu hii, isipokuwa shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma kwa idhini ya Joyce Yonah Fundi Kaguo au kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

IKIRARI

Mimi Joyce Kaguo, nathibitisha kuwa, Tasinifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya Digrii yoyote.

.....
Saini

.....
Tarehe

TABARUKU

Natabaruku kazi hii kwa Mama yangu Mzazi Adelhelma Lucas Samdendemi, Baba yangu mzazi Marehemu Yonah Richard Fundi Kaguo, mume wangu Jacob Mgogo pamoja na watoto wangu Luhozyo Jacob na Twilumba Jacob. Naitabaruku pia kazi hii kwa Watanzania wote.

SHUKURANI

Leo ninayo furaha kubwa moyoni mwangu kwa kufikia hatua hii katika uandishi wa tasinifu hii, ya masomo yangu ya Uzamili. Shukurani za pekee zimwendee Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai, nguvu na afya njema hatimaye kuweza kukamilisha kazi hii. Kama ilivyo ada, kazi nyingi za kitaaluma huhitaji msaada, ushauri usimamizi na mapendekezo kutoka kwa watu mbalimbali. Kwa mwenye busara yeyote afanikishapo jambo lake haachi kutoa shukurani kwa aliyemfanikishia. Nina orodha ya watu walioniwezesha kukamilisha kazi hii, sina budi japo kuwataja wachache wafuatao:

Shukurani za pekee zimwendee mwalimu na msimamizi wangu Prof. Dkt. Sheikh, T.S.Y.M. Sengo, kwa kunitia moyo, na kuniongoza kuanzia mwanzo wa wazo hadi mwisho bila kukata tamaa. Mwenyezi Mungu tu ndiye awezaye kumlipa kwa elimu kubwa niliyoipata kupitia kwake.

Nawashukuru wazazi wangu Yonah Richard Fundi Kagu (Mwenyezi Mungu Amrehemu) na mama yangu Adelhelma Lucas Samdendemi ambao ndio walinileta hapa duniani, kwa moyo wao wa dhati, wa kunifunza, kunitia moyo na kuwajibika kwangu kama wazazi wangu nami kama mtoto. Naishukuru familia yangu, mume wangu Jacob Patrick Mgogo, wanangu Luhozyo Jacob na Twilumba Jacob, ambao walinitia moyo sana na kunivumilia nikiwa katika harakati za kufanya kazi hii.

Shukurani nyingi ziwaendee baba, Mwalimu, Sheikh Ali Hemed Ali na mama Mwanaiki Hamdun kwa moyo wao wa upendo wa kunipokea kwa dhati na kuwa

wenyeji wangu pale nilipohitaji kuonana na mtafitiwa, tangu mwanzo kabisa wakati wa kukusanya data za awali mpaka nafanikisha kazi hii, na kuwa walimu wangu kwa kunifunza utamaduni wa watu wa Tanga. Walikuwa msaada mkubwa sana kwangu. Bila kumsahau Bi Madina Ali El-Buhriy, namshukuru sana kwa upendo na moyo wa kunisikiliza kila nilipohitaji kuwa naye, iwe ana kwa ana au kwa simu hata alipokuwa na shughuli zingine. Nasema, asante sana.

Kadhalika natoa shukurani zangu za dhati kwa walimu wangu wa Kiswahili walionilea na kunikuza tangu ngazi ya Shule ya Msingi mpaka hivi leo. Vilevile natoa shukurani zangu kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kwa kunipa ruhusa na muda wa kusoma Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, vinginevyo nisingefanikiwa kufika hapa nilipo.

IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchunguza dhamira zinazojitokeza katika mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy na namna tamathali za usemi zinavyosaidia kujenga dhamira hizo. Tumefikia malengo kwa kuibua dhamira kumi na mbili na kuchambua tamathali za usemi nane. Tasinifu hii ina sura kuu sita. Katika Sura ya Kwanza kuna utangulizi wa jumla, historia fupi ya Bi Madina Ali El-Buhriy, Usuli wa mada ya utafiti, Usuli wa tatizo la utafiti, Tatizo la utafiti, Nia kuu ya utafiti, Malengo maalumu ya utafiti, Maswali ya utafiti, Umuhimu wa utafiti, Eneo la utafiti. Sura ya Pili, kuna Uhakiki wa kazi za mashairi, Utafiti uliofanyika katika ushairi na hitimishi. Kuna mikabala ya kinadharia, Maana ya Nadharia, Ufafanuzi wa Nadharia. Sura ya Tatu, kuna maelezo juu ya mbinu na njia zilizotumiwa na mtafiti katika ukusanyaji wa data na zana za utafiti, Ratiba ya mtafiti, bajeti. Katika Sura ya Nne, kuna uwasilishaji wa matokeo ya utafiti, dhamira kumi na mbili zimejadiliwa; Dhamira ya kutenda na kutendewa mema, Dhamira ya utunzaji wa Mazingira, Dhamira ya Kuhamasisha wanawake katika utunzi wa mashairi, Dhamira ya umalaya katika jamii, Dhamira ya umuhimu wa Wazazi, Dhamira ya hulka za binadamu, Dhamira ya kumbukizi, Dhamira ya matatizo ya maji katika Jiji la Dar Es Salaam, Dhamira ya Rushwa, Dhamira ya mabomu ya Mbagala, Dhamira ya ugomvi/mafarakano. Katika Sura ya Tano, kuna matumizi ya fani, kipengele kilichopewa uzito ni; lugha, tamathali za usemi zimechambuliwa kulingana na muktadha wa utunzi wa mashairi, tashibiha, taswira, stiari, nidaa, takriri, tashihisi, ritifaa, kejeli. Sura ya sita kuna maoni na mapendekezo kwa ajili ya jamii na tafiti zijazo.

YALIYOMO

UTHIBITISHI WA MSIMAMIZI.....	ii
HAKIMILIKI	iii
IKIRARI	iv
TABARUKU	v
SHUKURANI	vi
IKISIRI	viii
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xiv
ORODHA YA VIELEZEO	xv
ORODHA YA VIAMBATISHI	xvi
VIFUPISHI	xvii
SURA YA KWANZA.....	1
1.0 UTANGULIZI WA JUMLA	1
1.1 Utangulizi	1
1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti	5
1.4.1 Tamko la Tatizo la Utafiti	6
1.3.2 Tatizo la Utafiti	8
1.4 Lengo Kuu	8
1.5 Malengo Maalumu ya Utafiti	8
1.6 Maswali ya Utafiti	9
1.7 Umuhimu wa Utafiti.....	9
1.8 Eneo la Utafiti	9
1.8.1 Eneo la Kijiografia	10

1.8.2	Eneo la Kitaaluma	10
SURA YA PILI.....		11
2.0 UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA		11
2.1	Utalii wa Kazi Tangulizi	11
2.1.1	Utangulizi.....	11
2.1.2	Dhanna ya Ushairi	11
2.1.3	Asili ya Ushairi wa Kiswahili.....	13
2.1.4	Uhakiki wa Kazi za Ushairi wa Kiswahili.....	14
2.1.5	Utafiti Uliofanyika Katika Mada za Ushairi.....	21
2.1.6	Umuhimu wa Mashairi	22
2.1.7	Hitimishi	23
2.2	Mkabala wa Kinadharia.....	23
2.2.1	Ufafanuzi wa Nadharia	24
2.2.2	Nadharia ya Kijamii.....	24
2.2.4	Nadharia ya Uhalisia	27
SURA YA TATU.....		31
3.0 MBINU ZA UTAFITI.....		31
3.1	Utangulizi	31
3.2	Mbinu za Kukusanyia Data	31
3.2.1	Usaili	31
3.2.2	Upitiaji wa Nyaraka.....	31
3.2.3	Wasaidizi Katika Kukusanya wa Data	32
3.3	Ukusanyaji wa Data.....	32
3.3.1	Vyanzo vya Data.....	32

3.3.2	Data za Msingi.....	33
3.3.3	Data za Upili.....	33
3.4	Uteuzi wa Walengwa.....	33
3.5	Zana za Utafiti	34
3.5.1	Kalamu na Karatasi	34
3.5.2	Ngamizi	34
3.5.3	Simu ya Mkononi (Rukono).....	34
	SURA YA NNE.....	36
4.0	UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA.....	36
4.1	Utangulizi	36
4.2	Uchambuzi wa Data	36
4.3	Dhamira katika mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy.....	37
4.3.1	Dhamira ya Utunzaji wa Mazingira	37
4.3.2	Dhamira ya Umalaya Katika jamii.....	41
4.3.3	Dhamira ya Kuhamasisha Wanawake Katika Utunzi wa Mashairi	46
4.3.4	Dhamira ya Umuhimu wa Wazazi	49
4.3.5	Dhamira ya Kutenda na Kutendewa Mema	52
4.3.6	Dhamira ya Athari za Hulka za Binadamu.....	55
4.3.7	Dhamira ya Utengano wa Wanandugu.....	56
4.3.8	Dhamira ya Kumbukizi	60
4.3.9	Dhamira ya Matatizo ya Maji Katika Jiji la Dar es Salaam	64
4.3.10	Dhamira ya Rushwa	67
4.3.11	Dhamira ya Athari za Mabomu ya Mbagala	72
4.3.12	Dhamira ya Ugomvi/Mafarakano.....	78

4.4	Hitimishi	83
SURA YA TANO.....		85
5.0	MATUMIZI YA FANI KATIKA USHAIRI WA BI MADINA ALI EL- BUHRIY	85
5.1	Utangulizi	85
5.2	Matumizi ya Lugha	85
5.3	Matumizi Ya Tamathali za Usemi Katika Mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy	86
5.3.1	Lugha ya Tashibiha	87
5.3.2	Lugha ya Sitiari	88
5.3.3	Lugha ya Tashihisi	90
5.3.4	Lugha ya Kejeli	91
5.3.5	Lugha ya Ritifaa	92
5.3.6	Nidaa	93
5.3.7	Lugha ya Takriri	94
5.3.8	Tabaini	96
5.2.9	Lugha ya Taswira	96
5.3.8.1	Taswira Zinazoonekana	96
5.3.8.2	Taswira za Mawazoni/Kufikirika.....	97
5.3.8.3	Taswira za Hisiya.....	98
5.4	Hitimishi	98
SURA YA SITA.....		100
6.0	MUHTASARI NA MAPENDEKEZO	100
6.1	Utangulizi	100

6.2	Muhtasari wa Utafiti.....	100
6.2.2	Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti	101
6.3	Mapendekezo.....	102
6.3.1	Mapendekezo Katika Utafiti Ujao.....	102
6.3.2	Mapendekezo kwa Wasanii wa Mashairi.....	102
6.3.3	Mapendekezo kwa Jamii	103
	MAREJELEO	104
	VIAMBATISHI.....	112

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 3.1: Ratiba ya Mtahiniwa.....	110
Jedwali 3.2: Bajeti ya Mtahiniwa.....	111

ORODHA YA VIELEZEO

Kielelezo 4.1: Rais Kikwete na Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Emmanuel Nchimbi, wakiangali baadhi ya vipande na mabaki ya mabomu, vilivyookotwa katika eneo la Mbagala.....	75
Kielelezo 4.2: Sehemu ya Mabaki ya Nyumba, Baada ya Kulipuliwa na Mabomu, Eneo la Mbagala	76
Kielelezo 4.3: Hii ndiyo Mbagala Iliyolipuliwa	78

ORODHA YA VIAMBATISHI

Kiambatanishi 1: Maswali ya Utafiti kwa Ajili ya Ndugu Zake Bibi Madina

Ali El- Buhriy 112

Kiambatanishi 2: Maswali kwa Ajili ya Bi Madina El- Buhriy..... 113

Kiambatanishi 3: Historia ya Bi Madina Ali El- Buhriy..... 114

Kiambatanishi 4: Baadhi ya Mashairi ya Bi Madina Ali El- Buhriy 121

VIFUPISHI

DAWASA	Dar Es Salaam Water Supply and Sewage Authority
DAWASCO	Dar Es Salaam Water Supply and Sewage Company
Dkt	Daktari
JWTZ	Jeshi la Wananchi wa Tanzania
K. v	kama vile
KKKT	Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania
M.A	Masters of Arts
N. k	Nakadharika
Prof	Profesa
TAG	Tanzania Assemblies of God
TAKUKURU	Taasis ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
Uk	Ukurasa
UKIMWI	Upungufu wa KInga Mwilini

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI WA JUMLA

1.1 Utangulizi

Fasihi na historia ya maisha ya mwanadamu haviwezi kutenganishwa kamwe, kipindi ambacho binadamu alianza kutumia lugha kama nyenzo ya mawasiliano pia aligundua sanaa ya lugha, na utanzu wa ushairi ukiwa miongoni mwa sanaa hizo. Mayoka (1993) anashadidiya kwamba ushairi umetokana na jamii ya wanadamu wenyewe na umesheheneza mafundisho mengi ambayo yamekuwa yakitumika katika hatua zote za maisha ya mwanadamu, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Hatua hizo zimeanza kupitiwa na mwanadamu tangu enzi za kale za kuishi mapangoni, enzi za uwindaji, ujima, utumwa, vita vya makabila, uvamizi wa wageni, ukoloni na harakati za kupambana na ukoloni hadi kufikia utumwa wa akili na utandawazi. Kwa mtazamo huu imekuwa ni vigumu, hata kubainisha, ni tarehe ipi na mwaka gani, utanzu wa ushairi ulianza kutumika katika jamii za wanadamu.

Abedi (1973) na Chiraghdin (1977) wanasema, kwa asili ushairi andishi, chimbuko lake ni ushairi simulizi, ambao ulitungwa kwa madhumuni ya kughaniwa kwa ghibu kwenye matukio ya kijamii kama sherehe za jando na unyago, kubembelezea watoto, kuliwaza watu misibani. Hayo ni matukio ya kawaida, ambayo yapo tangu azali. Hivyo, ni dhahiri kwamba, kila jamii ilikuwa na sanaa yake ya ushairi. Katika historia ya ushairi wa Kiswahili, Mulokozi (1996) anasema kwamba, majilio ya wageni walowezi wa Kiarabu, hasa kuanzia mwaka 1000 BK, yalileta athari kubwa tena ya kudumu, katika maendeleo ya ushairi wa Kiswahili. Mambo hayo ni kuingia

kwa Dini ya Kiislamu na taaluma ya uandishi katika hati ya Kiarabu. Maisha ya Waswahili yalianza kufungamanishwa na utamaduni wa Kiislamu, kwa kukubali kukamilisha Uwisilamu wao na kujifunza taaluma za kusoma na kuandika Quraani katika madrasa za Dini ili waweze kujisomea wenyewe Msahafu wa Dini yao. Kwa njia hiyo, ujuzi na tabia ya kuandika na kusoma ilianza kuenea miongoni mwa Waswahili Waisilamu.

Mulokozi (1996) anaendelea kusema, Kati ya miaka ya 1000 hadi 1500 BK miji ya Waswahili iliendelea kupanuka katika eneo zima la Pwani kuanzia Kisimayuu hadi Sofala. Kwa upande wa pili, fasihi nayo iliendelea kukua na kupanuka. Kwa hiyo, kuenea kwa utamaduni wa maandishi kuliendeleza kushika kasi kwa ushairi andishi ambao ulifikia kuwa ni sehemu ya utamaduni wa Waswahili. Tungependa kuweka wazi kwamba Waarabu walipofika katika jamii ya Waswahili, waliikuta jamii hiyo na sanaa yake ya utunzi wa ushairi. Mchango wa Waisilamu wageni katika kukuza ushairi wa Waswahili, ni kufundishana nao njia mpya ya kuhifadhi tungo, kwa njia ya maandishi.

Miongoni mwa tungo za awali kabisa za Arudhi ya Kiswahili zinazotajwa na wanazuoni, Kimani (1983) ni Utenzi wa Tumbuka ambao pia hujulikana, kwa jina la, Chuo cha Herekali, ni maarufu sana katika historia ya Ushairi wa Kiswahili. Utenzi huu ni wa kwanza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Utenzi huu unasimulia habari za Fumo Laiti, Nabahani ambaye alikuwa ni Sultani wa eneo la Pate kwa wakati huo. Utenzi huu pia unasimulia vita vya miezi nane iliyotokea Syria kati ya Waarabu na wenyeji wa Byzantine kwa ajili ya Dini ya Kiislamu. Inasemekana kwamba kabla utenzi huu haujaandikwa na Mwego bin Athuman mwaka 1728 kulikuwa na

mashairi mengine yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili, ambayo hatuna nakala zake kutokana na uhalibifu wa uchomaji moto wa miji ya pwani uliofanywa na Wareno.

Jamii za Waswahili ziliendelea kutongoa tungo ili kusawiri matukio ndani ya vipindi tafautitafauti vya maisha yao Mulokozi (1982), Ushairi wa Kiswahili ulitumika kama silaha muhimu ya kupinga utawala wa kikoloni kwa kuelezea madhila yanayofanywa na wakoloni hao dhidi ya wananchi. Dhima kuu katika mashairi ya kipindi hicho ni kuwataka wakoloni waondoke nchini na kuwaachia wananchi nchi yao huru ili wajitawale wenyewe.

Mapambano ya aina hii yalianza tangu kipindi cha utawala wa Wareno ambapo watawala hao walipewa onyo kali na washairi na kutakiwa kuondoka hapa nchini. Baadhi ya mashairi ya kipindi hicho ni, Utendi wa Hamziyya (Sayyid 1652), Siri li Asirari (binti Lemba 1663), Utendi wa tambuka (Mwego 1728) Tendi za kipindi hicho zilikuwa ni istiaara juu ya migogoro ya kisiasa iliyowakabili Waswahili.

Katika kipindi cha mwaka 1750-1900 ni kipindi chenye historia nyingine juu ya tungo za ushairi wa Kiswahili, mashairi mengi yalikuwa ni mashambulizi ya Waswahili juu ya utawala wa Waarabu, baadhi ya washairi maarufu katika kipindi hicho ni pamoja na Muyaka bin Haji wa Mombasa (1776-1840), Suud bin Said (1810-1876). Wote hao walitunga mashairi yaliyohusu harakati za kisiasa na za kijamii, za wakati wao na baadhi yao waliuawa au kufungwa gereza kwa sababu ya kupinga kutawaliwa. Tungo za kiutamaduni, mawaidha na tumbuizo zilianza kuenea zaidi. Miongoni mwa tungo hizo, ni pamoja na Utendi wa Mwanakupona (1858).

Katika kipindi cha karne ya ishirini, maendeleo ya Arudhi ya Kiswahili yaliathiriwa na kuja kwa wageni wa kimagharibi. Walianzisha shule, maandishi ya kirumi, itikadi na elimu ya kimagharibi walieneza biashara zao kwa lugha ya Kiswahili kutoka pwani kuelekea bara. Kwa kisomo cha shule mafunzo ya Ukiristo, hati ya Kirumi ilianza kutumika zaidi badala ya hati ya Kiarabu, Ushairi ulianza kutungwa na kusomwa na watu wengi, hata wale ambao hawakujua kuzisoma hati za Kiarabu. Kuanzishwa kwa gazeti la Mamboleo, lililokuwa na ukurasa kwa ajili ya mashairi, mwaka 1923, lilitoa nafasi ya kuwakutanisha na kuwashajiisha watunzi wa mashairi wa maeneo mengi ya Afrika Mashariki. Miongoni mwao ni Shaaban Robert (1909-1962), Mdanzi Hanassa (1880-1952), Salehe Kibwana (1887-1996), Mwalimu Kihere (1903-1974). Kuanzia mwaka 1948 Mnyampala, Akilimali Snow-White, Amri Abeid walianza kuchapisha diwani zao katika shirika la uchapishaji vitabu la Afrika Mashariki (EALB).

Ushairi wa Kiswahili, ambao, kwanza ulistawi kwenye upwa wa Kenya na Tanganyika, hasa katika karne ya 10-15, leo hii, umekuwa ni sanaa ya Afrika mashariki nzima hadi Burundi, Uganda, Rwanda na Demokrasia ya watu wa Kongo. Ni fani ambayo inazidi kukua, kupanuka na kuchanua, ni utanzu ambao umeitumikia jamii zaidi kuliko tanzu nyingine za fasihi. Maisha ya mwanadamu ni safari ndefu isiyokuwa na mwisho, pia kazi za fasihi zimo safarini, hazijafika mwisho wake. Kila siku dunia ina matukio na mambo mapya, ni wajibu wa wasanii kuyabeba mambo hayo na kuwajulisha walimwengu. Bi Madina Ali El-Buhriy mzawa wa jamii ya Waswahili, ambako ndiko liliko chimbuko la Ushairi wa Kiswahili amebeba wajibu huo katika utanzu wa Ushairi.

1.2 Usuli wa Mada ya Utafiti

Duniani kote, yupo mtu mmoja tu, (Sengo, 1985) Mtu huyo ni mwanamume na mwanamke kwa pamoja. Watu hao ni wawili kwa macho na akili za kutegemeana. Katika jamii nyingi za Kiafrika pamoja na jamii hiyo inayofanyiwa utafiti, mwanamke hupewa nafasi ya vyeo tisa katika familia yake:

1. Anaitwa mama na watoto aliowazaa.
2. Anaitwa dada na ndugu aliozaliwa nao.
3. Anaitwa nyanya na wajukuu wa kizazi chake.
4. Anaitwa mke na mume aliyemuoa.
5. Anaitwa mkwe. Mke wa mjomba kwa watoto wa wifizi wake
6. Anaitwa mama mkwe na;
 - (i) Waume wa mabinti wake
 - (ii) Wake wa vijana wake
 - (iii) Wazazi wa Mume wake
7. Anaitwa shangazi na watoto wa kaka wake.
8. Anaitwa shemeji na wakubwa au ndugu wa mumewe.
9. Anaitwa binti kwa baba wake.

Sengo (2014 darasani) Katika hali ya harakati za kupigania haki za kina mama, jamii za kimagharibi na za kiafrika zina tafauti kubwa. Katika jamii za kimagharibi, mtoto ana uhuru wa kuasiana na wazazi wake anapofika umri wa miaka 18. Katika jamii za kiafrika, mtoto hata anapokuwa na umri wa miaka 100, bado ni mtoto kwa wazazi wake. Hata wazazi wakifa, bado mtoto atawajibika kwa wazazi wafu kwa jina la mizimu na kwa wazazi walezi warithi.

Wanafasihi wa kiafrika wanalipa uzito jambo hilo na kulichambua kulingana na mazingira. Wanawapa thamani kubwa akina mama. Waswahili wana maneno yao yanayoonesha umuhimu wa mama katika jamii. Wanafasihi wanabeba wajibu wao wa kuelezea hali hiyo kwa njia ya kisanii, wao hutumia maneno machache k.v, “Nani kama mama!” Hakuna mzazi na mlezi amshindaye mama. Mama kwa mwanawe. Pia kuna vitendawili kama; Mama hachoki kunibeba (kitanda). Mama hatui mzigo wake (konokono). Mzigo mzito unapomshinda kuubeba kichwani (kama baba au jamii) huangukia fuzini. Mama hubeba mzigo wote juu ya mtoto. Hupata taabu za kujifunga, kujifungua na kulea. Uchungu hasa wa uzazi aujua mama, baba ni mhudumu tu.

Utafiti mwingi uliotangulia na kushughulikia kipengele cha dhamira zinazojitokeza katika mashairi, ulihusu mashairi yaliyotungwa na kuandikwa na wasanii wanaume. Baadhi ya kazi hizo ni k.v, Kitogo (2002) *The poets contribution to political development: A case of Saadan Abdul Kandoro, M.A thesis*. Pengo kubwa lilikuwa linamsubiri mtafiti, kwa bahati, ni mwanamke kuteua mada ya jinsi Bi Madina Ali anavyoweza kutumia sanaa ya ushairi wa kwao, kuzungumzia mambo ya kijamii k.v Siasa, uchumi na utamaduni, na kuonesha kama kuna tafauti zozote za kidhamira zinazotungwa na washairi wanaume. Sababu ya pili ni kuonesha ushahidi kuwa, mwanamke, naye anaweza kutunga, kueleza na kuihakiki jamii, bila ya kusema “akiwezesha ataweza”.

1.4.1 Tamko la Tatizo la Utafiti

Wataalamu wengi wanakubaliana kuwa asili ya Ushairi wa Kiswahili ni tungo simulizi, hasa nyimbo Chiraghdin (1971), Chiraghdin na wenzake (1975), Shariff

(1988), Nassir (1977), Sengo (2009) wanaunga mkono hoja ya kuwa, Ushairi ni utanzu mkongwe na kwa asili yake ni mwanadamu na hisia zote zilizohusu matukio ya maisha yake. Mazingira na vituko vya maisha, vilisaidia kutongoa tungo za kishairi, zikatungika kulingana na utashi wa pahala, hali na wakati. Utendi wa Mwanakupona ni kati ya tenzi chache zilizotungwa na mwanamke ambaye alikuwa anatoa wasia kwa binti yake na mabinti wa mfano wake, namna ya kukabiliana na maisha ya ndoa. Katika baadhi ya beti, binti anaelezwa;

Binti mchanga kamawe
 Mchachefu wa sanatiwe
 Tulizana uwambiwe
 Kwanda, kamata Dini
 Pili, kuwa na adabu
 Tatu, uwe sadiqi

Kutokana na kazi ya Mwanakupona hapo juu, tunajifunza kwamba tangu kale mwanamke alitumia sanaa ya Ushairi kama njia muhimu ya kutolea hisia zake juu ya mambo ya kijamii. Jitihada za wanawake kujiingiza katika mashairi hazikuishia kwa Mwanakupona peke yake. Kazi yake inatumika kama kokwa iliyopandwa kwenye rutuba na maji, sasa tunaona namna inavyostawi na kutuletea matunda bora. Wanawake wa sasa wanaojitokeza katika utunzi wa mashairi, ujasiri wao unatokana na watangulizi wa fani hii, kinachowatafautisha ni kwamba kila mmoja anatongoa tungo kulingana na kipindi cha wakati wake. Utamaduni wa urithi wa Dini ya Kiislamu ulioshamiri katika kipindi cha uhai wa Mwanakupona umeathiri ujumbe wa mashairi yake. Kwa waisilamu, Dini yao ndiyo msingi mama unaorejelewa na kusimamiwa kwa yote mengine yanayotokea duniani. Bi Madina Ali El-Buhriy aliyetunga mashairi yake katika kipindi cha taifa huru la Tanzania, amepata

mawanda mapana ya tajiriba ya maisha aliyoyazungumzia kwenye dhamira za mashairi yake.

1.3.2 Tatizo la Utafiti

Ushairi wa jamii yeyote, umeficha siri nyingi. Watunzi wengi wa mashairi na tenzi katika Arudhi ya Kiswahili ni wanaume. Akina mama Uswahilini, wamejihifadhi na kuhifadhika katika majumba yao, kwa sababu za kiushunuzi na kiutamaduni. Wanawake Uswahilini wamefananishwa na kitambala cheupe kisicho doa. Kwa thamani hiyo, mambo yao mengi pamoja na mawazo yao hufikishwa nje na akina baba. Ni utaratibu uliokubalika. “La konokono na kobe, halifahamiki kwa kipanga na mwewe”.

Bi Madina Ali El-Buhriy, ni mtoto wa kike aliyerukhusika kutoa fikra na mawazo yake yeye mwenyewe kwa njia ya Ushairi kama ilivyokuwa kwa Siti bint Saad. Mawazo, fikra, hekima, utashi, na weledi wa Bi Madina Ali El-Buhriy, ambaye ni mzawa katika familia ya usanii na taaluma ya utunzi. Bi Madina Ali El- Buhriy, kazi zake hazijaingizwa sana katika maandishi na kuwekwa wazi kwa wanajamii wengi. Kufanywa kwa utafiti huu kwa kiwango cha Uzamili, kunalenga kufichua tatizo la uwezo wa mwanamke wa kutunga na kutungua mambo katika Arudhi ya Kiswahili.

1.4 Lengo Kuu

Ni kukusanya, kutathimini, kubainisha na kuchambua maudhui ya tungo za kutosha zilizotungwa kwa mtindo wa Arudhi ya Kiswahili na Bi Madina Ali El- Buhriy.

1.5 Malengo Maalumu ya Utafiti

1.5.1 Kuanisha tungo za Ushairi wa Bi Madina Ali El-Buhriy.

1.5.2 Kuchambua dhamira katika Mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy.

1.5.3 Kutathimini kipengele cha fani katika mashairi teule ya Bi Madina Ali El-Buhriy

1.6 Maswali ya Utafiti

1.6.1 Jee, tunawezaje kupata mashairi yaliyotungwa na Bi Madina Ali El-Buhriy?

1.6.2 Jee, kuna dhamira zipi zilizojitokeza katika mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy?

1.6.3 Jee, Bi Madina Ali El-Buhriy amezingatia vipi kipengele cha fani katika mashairi yake?

1.7 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utasaidia kuhifadhi Ushairi wa Bi Madina Ali El-Buhriy kwa njia ya maandishi, tasnifu, vitabu na mitandao. Utatoa hima kwa wapenzi wa kazi za Ushairi watafiti watahimizika kuendelea kufanya utafiti juu ya watunzi wengine ili kuhifadhi kazi zao zilizo muhimu kwa jamii ndogondogo na kubwa. Utafiti huu utawakumbusha wanajamii juu ya umuhimu wa kutunza amali za jamii kuzirithisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine ili kuilelea jadi ambayo haitakiwi kufuwawa. Utafiti huu utatoa mchango mkubwa wa fikra na mipango ya kujenga upya taswira ya mwanamke katika jamii. Utafiti huu utaibua mijadala ambayo itatoa fursa kwa watafiti wengine kufanya utafiti na kuchunguza kwa kina ushairi wa mwanamke.

1.8 Eneo la Utafiti

Eneo la kijiografia na kitaaluma yamebainishwa ili kuweka uwazi juu ya maeneo lengwa kwenye kazi hii.

1.8.1 Eneo la Kijiografia

Eneo la kijiografia la utafiti huu ni jiji la Tanga, ambako ndiko yaliko makaazi ya Bi Madina Ali El-Buhriy, tulikofika na kufanikiwa kuonana naye kwa ajili ya kutupatia nakala za mashairi ambayo aliyatunga. Pia, alitusaidia kujibu baadhi ya maswali na kufanya majadiliano katika baadhi ya vipengele vya tasnifu hii.

1.8.2 Eneo la Kitaaluma

Eneo la kitaaluma ni tungo zake zote zilizopatikana tangu alipoanza kutunga mwaka 1967 akiwa na umri wa miaka 15, akiwa mwanafunzi wa darasa la sita, hadi sasa. Utafiti huu ulishughulikia kipengele cha dhamira, matumizi ya lugha, kipengele cha tamathali za usemi na jinsi vilivyosaidia kupatikana kwa dhamira kutokana na mashairi ya Bi Madina Ali EL- Buhriy.

1.9 Hitimishi

Sura hii ya kwanza, imejadili masuala ya awali kuhusu tatizo la utafiti lililoshughulikiwa katika tasnifu hii. Masuala hayo ni pamoja na; Utangulizi wa jumla, tamko la tatizo la utafiti, Tatizo la utafiti, Malengo na maswali ya utafiti, eneo la utafiti. Aidha umuhimu wa utafiti na kufafanuliwa pia. lengo la kuya jadili hayo ni kuweka misingi, kuhusu haja na ulazima wa kufanyika kwa utafiti huu.

SURA YA PILI

2.0 UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utalii wa Kazi Tangulizi

2.1.1 Utangulizi

Utalii, hapa una maana ya usomaji wa mzamo, wa kuibua mapya yaliyojificha, aghalabu vitabuni. Katika sura hii, mtafiti alisoma kazi za wanazuoni waliomtangulia na kuyatumia maarifa, aliyoyapata kwenye uandishi wa taarifa za utafiti wake. Nafasi ya kazi tangulizi katika uandishi wa tasnifu ni kipengele kinachosisitizwa sana kwani ni sehemu muhimu mno ya kufanikisha kazi ya utafiti.

Omari (2011) anasema kuwa, kazi tangulizi, hutoa ujuzi na maarifa ya wanazuoni waliowahi kufanya kazi yenye mwelekeo na lengo la mtafiti. Hatua hii, humsaidia mtafiti kutambua mambo yapi yamefanyiwa utafiti na yapi bado hayajafanyiwa utafiti, Kombo na Tromp (2006) wanashadidiya kuwa, kazi tangulizi ina umuhimu mkubwa katika utafiti, humsaidia mtafiti kupata pengo la utafiti, kuepuka kufanya kazi ambayo ilikwishafanywa, kutambua nadharia zilizotumika katika kupata majibu ya kazi za utafiti. Kwa kuzingatia msisitizo uliyotolewa na wanazuoni hao hapo juu, mtafiti alipata nafasi ya kutalii kazi zilizopatikana katika maktaba za Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam na Maktaba binafsi ya Prof Tigiti Sengo ingawa bado anajenga.

2.1.2 Dhanna ya Ushairi

Katika kipindi cha miaka ya 1970 kuliibuka mgogoro wa ushairi, wanamapokeo wanawashutumu wanausasa kuwa, wanania ya kuua ushairi wa Kiswahili, kutokana

na kukwepa kanuni za utunzi wa ushairi. Wanausasa kwa upande wao wanawashutumu wana mapokeo kukataa kupokea mabidiliko katika ushairi. Jambo hili limekuwa chanzo kikubwa cha mkanganyiko kwa mwanafunzi mwenye nia ya kutaka kujifunza fasili ya neno ushairi.

Mnyampala (1965) anasema ushairi ni msingi wa maneno ya hekima tangu kale. Ndicho kitu kilicho bora sana katika maongezi ya dunia kwa kutumia maneno ya mkato na lugha nzito yenye kunata inayopangwa kwa urari wa mizani na vina maalumu. Yeye kausemea Ushairi wa Kiswahili. Mawazo hayo yameungwa mkono na Shaaban (1958), Abedi (1965), Abdilatif (1973), Chraghdin (1977), Kandoro (1978), Sengo (1983), Mayoka (1986), Kwao hao, matumizi ya sheria za vina, urari na mizani ndiyo uti wa mgongo wa Arudhi ya Kiswahili. Senkoro (1987) anasisitiza kuwa, wasioweza kuzitimiza sheria hizo kali basi wasijiite kuwa ni washairi wa mashairi ya Kiswahili.

Mtazamo huu unatafautiana na kundi jingine ambalo linatoa maelezo tafauti juu ya dhanna ya ushairi. Kezilahabi (1976) Ushairi ni tukio au wazo ambalo limeoneshwa kwetu kutokana na upangaji mzuri wa maneno fasaha yenye mizani kwa kifupi ili kuonesha ukweli fulani wa maisha. Maelezo haya yanaungwa mkono na Topan (1974), Mulokozi na Kahigi (1982), Henry Muhanika na Theobald Mvungi (1982). Kwao wao, sheria ya vina, na urari wa mizani kuitwa uti wa mshairi wanakataa. Wanasisitiza kuwa siyo lazima shairi la Kiswahili kubanwa na sheria za wanamapokeo. Jee maelezo haya, yanalenga ushairi upi? Wa Kiswahili? Au wa jamii nyingine za kigeni? Mtafiti anaona kuwa, usomi una asili. Asozawa na tumbiri, si rahisi kumthamini tumbiri wala nduguze.

2.1.3 Asili ya Ushairi wa Kiswahili

Dhanna ya chimbuko inafasiliwa na TUKI (2004) kuwa ni mwazo au asili ya kitu. Baadhi ya wataalamu wameweza kuelezea chimbuko la Ushairi wa Kiswahili kwa kutumia mitazamo au nadharia mbili; Nadharia ya kwanza inadai kuwa; Chimbuko la ushairi wa Kiswahili ulitokana na ujio wa Waarabu. Harries (1962) na Knappert (1979) wanasema kuwa, ushairi wa Kiswahili umetokana na Uislamu, ulianza kwenye upwa wa kaskazini mwa Kenya hususani Lamu. Na maudhui ya ushairi wa Kiswahili yalitokana na ushairi wa Kiarabu. Ushairi wa Waswahili ulianza katika karne ya 17 na pia ni ushairi wa Kiislamu huchanganya sifa za tungo za kiafrika na za kiajemi.

Hoja hizo hazina ushawishi wa kutosheleza kutufikisha katika hatua ya kuzikubali na kuziamini. Hoja ya kuwa Ushairi ulianza pwani ya kaskazini ya Kenya si kweli kwa sababu Waswahili walikuwepo hata sehemu nyingine kama vile Kilwa na Bagamoyo hadi Sofala ambapo ushairi ulitumika katika shughuli zao k.v matambiko, misiba, jando na unyago, kilimo na uvuvi. Hoja ya kusema ushairi wa Kiswahili ulitokana na Kiarabu haina mashiko, Waswahili walikuwepo hata kabla ya Waarabu na walikuwa na tungo zao za kishairi. Dai la kwamba, Waswahili walianza kutunga ushairi katika karne ya 17 siyo sahihi. Hoja zao zimechanganya dhanna ya asili na chimbuko la ushairi wa Kiswahili, ingefaa zitenganishwe. Suala la kujua lini na wapi ushairi wa kwanza, ulianza kutungwa na kutumika, bado ni mjadala unaoendele katika safari ya wanazuoni. Hata hivyo hatuwezi kupuuza moja kwa moja hoja za Knappert (1979) na Harries (1962) Hoja zao ni mwanzo mzuri wa kuendeleza utafiti juu ya asili ya ushairi wa Kiswahili.

Nadharia ya pili inasema kuwa ushairi ni zao la Waswahili wenyewe. Nadharia hii imejadiliwa na kuungwa mkono na wataalamu wakiwemo Shaban (1967), Mayoka (1993), Senkoro (1987), Mulokozi (1996) na Sengo (1985). Wanakubaliana kwamba ushairi umetokana na jamii ya wanadamu wazawa waishio pwani ya Afrika Mashariki, walipoanza kutumia lugha kama chombo cha mawasiliano na msingi wa kujiletea maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii ambayo huambatana na ukuaji wa sanaa, ikiwemo ushairi uliotumika katika harakati za maisha ya mwanadamu.

Kwa muktadha wa kazi hii, tunakubaliana na nadharia inayosema kuwa, chimbuko la ushairi wa Kiswahili ni zao la Waswahili wenyewe, kwa sababu Waswahili wana makazi zao asilia, ambayo yapo katika mwambao wa Bahari ya Hindi na visiwa vyake, wana utamaduni wao ambao ulikuwepo hata kabla ya ujio wa wageni wa Kiarabu. Mwanzoni Waswahili waliutumia ushairi wa kughani kama nyimbo, ujio wa Waarabu uliwasaidia kupata hati ya maandishi, ndipo wakaanza kutunza tungo zao kwa kuziandika kwa kutumia hati ya Kiarabu.

2.1.4 Uhakiki wa Kazi za Ushairi wa Kiswahili

Mulokozi (1999) alifanya uchambuzi mfupi wa fani na maudhui kwa kutumia tendi za Fumo Liyongo, Al- Inkishafi na Mwanakupona kama wawakilishi wa washairi wakongwe katika historia ya Ushairi wa kiswahili. Alibaini kwamba kila mtunzi alitongoa tungo zake kulingana na muktadha wa jamii yake. Maudhui ya utendi wa Fumo Liyongo yalihusu utetezi wa nchi, kugombania utawala, usaliti na ushujaa. Kwa upande wa Al-Inkishafi, msingi wa maudhui yake ni Qurani Tukufu, anayaona maisha katika sura mbili, sura ya unyoofu maisha ya unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu na sura ya upotofu, maisha yanayomuhadaa binadamu amsahau Muumba.

Maudhui katika Utendi wa Mwanakupona, ni mawaidha ya mzazi kwa binti kuhusu maisha ya ndoa na namna ya kuishi katika jamii. Anamuhimiza binti yake ashikilie na misingi ya Dini yake na kufuata mila na dasturi za jamii yake. Upande wa fani, kwa jumla, amesisitiza juu ya kuwapo kwa mizani, mishororo, beti. Lugha iliyotumika ni ya Kiamu na ya Kipate. Matumizi ya sitiari, taswira, picha ni sifa za kawaida katika Arudhi ya Kiswahili.

Uchambuzi wa kimaudhui uliyofanywa na Mulokozi, unatoa picha kwamba, kazi za kishairi, ni njia mojawapo inayotumiwa na binadamu kutolea hisia, ujumbe, mtazamo, na fikra juu ya mambo anayoyaona katika mazingira yake. Kwa kutumia msingi huo, mtafiti alikuwa makini katika uchambuzi wa maudhui kutokana na mashairi ya ili kuweka wazi fikra za mtunzi. Matumizi ya lugha yalipewa uzito unaostahiki ili kuona, namna msanii anavyotumia kipengele hicho katika kuibua dhamira na ujumbe. Uchambuzi wa Mulokozi ulibainisha matumizi ya tamathali za usemi mbili tu, ambazo ni sitiari na taswira. Katika utafiti huu Bi Madina Ali El-Buhriy alizingatia kipengele cha matumizi ya lugha ya kisanii kwa kutumia tamathali za usemi nyingi zaidi kuliko zilizojitokeza katika utenzi wa Mwanakupona, baadhi tamathali za usemi ni kejali, ritifaa, tashihisi, sitiari na tashibiha.

Shaaban Robert (1991), aliandika kitabu cha Wasifu wa Siti binti Saad, mwanamke anayekumbukwa katika visiwa vya Unguja na Afrika Mashariki, kwa utunzi wa nyimbo na uimbaji. Katika utangulizi wa kitabu hicho, mwandishi anasema, ingawa alipata kuonanan na Siti binti Saad Februari 1950, lakini hakuweza kutimiza nia yake ya kuhojiana naye kutokana na matatizo ya kiafya, hivyo mambo yaliyomo katika kitabu hicho ni masimulizi aliyoyapata kutoka kwa majirani wa Siti Binti Saad.

Mwandishi, alikusanya jumla ya beti kumi na mbili. Beti tatu za mwanzo, ni majibu, dhidi ya mashambulizi aliyoyapata kutoka kwa watu waliomuonea wivu juu ya mafanikio yake katika uimbaji. Zipo beti nyingine tisa, alizotunga kwa ajili ya kumsifu Sultani Mfawidhi, Khalifa bin Harub, aliyetawala katika kipindi cha uhai wake. Mwandishi anabainisha kwamba, Siti binti Saad hakujuu kusoma wala kuandika, isitoshe hakuwapo mtu wa jirani kwake, ambaye aliandika mashairi ya mwanamke huyo.

Kutokana na hali hiyo, isingekuwa jambo jepesi kupata idadi kubwa ya kazi za Siti binti Saad. Kwa upande wa Bi Madina Ali El-Buhriy, ni msomi mzuri, anayejua kusoma na kuandika, isipokuwa hajafanikiwa kuandika kitabu kilichokusanya tungo zake zote. Utafiti huu ulikipa uzito kipengele cha kupotea kwa kazi za wasanii. Kwa sasa yamekusanywa mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy na kuwekwa kwenye kiambatanishi C ndani ya tasnifu hii. Kwa kufanya hivyo, tumeepusha tatizo la kupotea kwa kazi za msanii kama tulivyoona kwa Siti binti Saad.

Kutokana na maelezo ya hapo juu tumeona kwamba, Sbaaban Robert hakuwa na nia ya kuchambua maudhui ya kazi za Siti binti Saad, lakini kwa kuwa aliweka wazi ujumbe uliopo katika mashairi hayo, kitaaluma, alifanya uchambuzi wa kimaudhui. Katika mazingira hayo, mtafiti anajiuliza, Siti binti Saad ni miongoni mwa waimbaji maarufu wa taarabu katika visiwa vya Zanzibar kama ilivyo kwa Fatuma Binti Baraka maarufu kwa jina la Bibi Kidude. Jee beti tatu zinazozungumzia masuala ya wivu na nyingine tisa za kumsifu Sultani ndizo zimempa umaarufu wake?

Jee Siti binti Saad hakuwa na mashairi mengine yenye maudhui juu ya mambo mengine ya kijamii kama, ndoa, ulevi, bidii mapenzi? Mtafiti alichukua jambo hili

kama tahadhari. Jitihada za kusoma magazeti ya Uhuru, Nipashe na mzalendo, magazeti ambayo yalichapa mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy zilifanyika. Matokeo ya kufanya hivyo, tulifanikiwa kupata jumla ya masahairi ishirini na mbili na utenzi mmoja.

Khatib (1987) aliandika makala juu ya washairi wanavyoliona Azimio la Arusha. Katika kazi yake, amewagawa washairi katika makundi matatu, kwa kutumia kigezo cha mielekeo ya kiitikadi, hasa namna wanavyoweza kuyakabili mambo, katika jamii zao. Anataja makundi hayo kuwa ni washairi wanaokabili matatizo ya jamii kwa kuonesha kinagaubaga uozo wa jamii, sababu za uozo na njia za kusafisha uozo huo. Washairi wa kundi hili ni wachache. Wapo washairi ambao kazi yao ni kuangalia sauti itokayo kwa viongozi na kuitungia beti nzuri ili kuwapumbaza waongozwao, ambao ndiwo muhimu, katika kuleta mabadiliko. Washairi wa aina hii, pia huitwa makasuku. Anasema kuwa, hili ni kundi la hatari, kwani hupotosha ukweli. Washairi wakimbizi wa ukweli, mawazo na mioyo yao, hutawaliwa na khofu pamoja na woga, kwa kuhusisha majini, mashetani na ibilisi, hutoa simulizi za peponi, taabu na raha baada ya kifo. Kosa lao kubwa ni kujitia uziwi wa kutoyasikia mateso ya watu hapa duniani na kujifanya vipofu wa kutoona madhila wayapatayo watu hapa duniani. Kundi jingine ni la wanafiki, wanaojiita wanamapinduzi, wasiomthamini wala kumuabubu Muumba aliowaumba.

Mambo yaliyoelezwa na Khatib hapo juu, ni ya msaada mkubwa katika utafiti huu, kwani miongoni mwa madhumuni maalumu yalikuwa ni kuchambua maudhui katika mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy. Maudhui katika kazi za kifasihi hueleweka vizuri kwa msomaji baada ya kutambua itikadi ya mtunzi. Utafiti umebaini kwamba

Bi Madina Ali El-Buhriy ni msanii mwenye itikadi ya kuyakabili matatizo ya jamii kwa kuonesha kiunagaubaga uozo wa jamii yake, kila ovu aliloliona, hakulifumbia macho, alilitungia shairi ili jamii ipate dhati yake. Mfano ni mashairi ya mke na pesa, jiji bila maji, masikini akifiwa, mwagomeani? Silumbi na wapujufu n.k.

Kitogo (2002) anaeleza kwamba, Ushairi wa Kiswahili umetoa mchango mkubwa katika kupatikana kwa uhuru wa Tanganyika na Zanzibar. Ushairi ulitumika kama chombo kikuu cha kuhamasisha wananchi kupigania haki yao ya kujitawala wenyewe na kumiliki raslimali zao kwa manufaa ya wananchi wote na siyo wakoloni peke yao kama ilivyokuwa katika utawala wa kikoloni. Kitogo anahusisha mashairi ya Kandoro na harakati za kudai uhuru wa Tanganyika, aliandika mashairi ya kuwafanya wananchi wapate hasira kutokana na kuonewa, kukandamizwa, kunyonywa na kudharauliwa. Miongoni mwa mashairi hayo, ni k.v, siafu wamekazana na kwetu ni kwao kwa nini?

Maelezo ya Kitogo (2002), yanazidi kufumbua macho ya mtafiti. Washairi, hapa nchini, ni nyenzo muhimu katika ustawi wa taifa. Wanayapa uzito unaostahili mambo ya kisiasa ili kuhakikisha kwamba jamii yao inaishi maisha ya uhuru, usawa, haki, amani na kufaidi matunda ya uhuru wao. Hata hivyo, utafiti wa Kitogo ulishughulikia dhamira moja tu ya kisiasa katika mashairi ya Saadan Kandoro. Katika muktadha wa kazi hiyo, kuna mambo mengine ya kijamii ambayo mtafiti anaona hayakupata nafasi ya kuchambuliwa kikamilifu. Utafiti huu, umeziba pengo hilo kwa kuchambua dhamira zinazojitokeza katika mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy. Utafiti huu umegusa fikira za kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kutokana na kazi za Bi Madina Ali El-Buhriy.

Msokile (1993), aliandika uhakiki juu ya tungo za Kezilahabi. Alichambua kitabu cha Karibu Ndani. Amebainisha ujenzi wa jamii mpya ikiwa dhamira kuu inayojitokeza katika kitabu hicho. Katika maelezo yake, msanii ameikosoa sera ya siasa ya ujamaa na kujitegemea, anaona kwamba haijaleta tija na maendeleo yoyote katika kumkomboa mwananchi kutokana na hali mbaya ya ukata na badala yake siasa hizo zimeongeza ukata kwa wananchi. Katika mtazamo mwingine, amebainisha kwamba viongozi waliopo madarakani walitawaliwa na tamaa ya kujilimbikizia mali. Matokeo yake, sera za siasa ya ujamaa zikaonekana kuwa zina kasoro kubwa hapa nchini. Waliobahatika kusoma siri ya Ujamaa kwenye toleo la kwanza la kitabu kilichopigwa marufuku nchini, *Religion and Development in Tanzania* (Leiden 1967) waliona dosari kubwa ya “Ujamaa” ulioelezwa kitabuni humo.

Malalamiko ya wananchi dhidi ya viongozi, wanaotumia vibaya madaraka na mamlaka waliyopewa ni jambo linalopigiwa kelele kote ulimwenguni. Hakuna mwananchi anayependa kuona anaishi maisha ya kiukata ili hali anashuhudia jinsi rasilimali za nchi zikiporwa, kuhodhiwa, kutoroshwa na kumilikiwa na kundi dogo la watu. Kero kama hizi hutoa msukumo kwa wanafasihi na wasomi kushika kalamu na karatasi ili kupunguza hasira zao kwa kuandika uozo uliokithiri dhidi ya viongozi wao, Kezilahabi kwa kaonesha hasira zake juu ya kasoro za sera ya siasa ya ujamaa na kujitegemea.

Katika uhakiki uliofanywa na Msokile, hajabainisha hatua madhubuti za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa kwa viongozi walioharibu sera za siasa ya ujamaa na kujitegemea. Katika uchambuzi wa kazi hii, mtafiti alikuwa makini kubainisha na

kuweka wazi suluhishi zinazopendekezwa na Bi Madina Ali El-Buhriy dhidi ya matatizo ya jamii yake. Kwa kufanya hivyo, watakasoma kazi hii watapata nafasi ya kutambua matatizo ya jamii yao na kuona njia zilizopendekezwa katika kukabiliana na hali hiyo.

Wallah (1988), katika utangulizi wa kitabu chake cha Malenga wa Ziwa Kuu anasema, mtunzi wa mashairi hakosi kuwa na jambo au mambo yaliyomkera au kumfika hata aamue kushika kalamu na kutunga shairi. Dunia imejaa visa na vituko ambavyo havifai kunyamaziwa bila kutolea maoni. Mtu akiniuliza ni kwa nini kuchagua utunzi wa mashairi ambao kwa kweli ni fani ngumu zaidi kuliko fani zote za fasihi, atajibiwa kwamba, siyo kweli kuwa siwezi hizo fani nyingine, bali uwanja wa Ushairi ni mpana zaidi, kumwezesha msanii kuyazungumza malimwengu mengi kwa wakati mmoja, kwa kuwa mawaidha ya shairi moja ni maudhui kamili ya kitabu kizima cha hadithi ndefu au natiki. Kwa hiyo idadi ya mashairi yaliyomo kitabuni ni sawa na lukuki ya vitabu. Mwandishi hakuendelea na ufafanuzi mwingine wa kumsaidia msomaji kutambua vigezo vilivyotumika hadi kufikia hatua ya kutoa kauli ya kushindanisha utanzu wa natiki na ushairi.

Mtafiti akichambua maelezo ya Wallah, amepata mambo mawili muhimu; kwanza mwandishi ameeleza hatua muhimu anazopitia mshairi, mpaka kuamua kutongoa beti za Ushairi. Msanii wa mashairi hatungi beti katika ombwe, bali huwa kuna visa, migongano, matukio, unyanyasaji, mambo ambayo huzalisha malighafi katika ushairi. Katika mazingira hayo, mshairi hujikuta ameshika kalamu na karatasi, akiandika alichokisikia au kukiona. Huteua maneno mazuri, yenye mvuto na ujumbe ndani yake, na kukamilisha utungo wake.

Kwa mantiki hiyo, mwandishi, alituongezea ujuzi katika kazi yetu. Kwa upande wa pili, mwandishi anaonesha kuwa ushairi ni utanzu wenye hadhi kubwa kuliko tanzu nyingine za fasihi. “Mawaidha ya shairi moja ni maudhui kamili ya kitabu kizima cha hadithi ndefu au cha natiki. Idadi ya mashairi yaliyomo kitabuni ni sawa na lukuki ya vitabu”. Kwa kauli hiyo mtafiti anaona kwamba, Wallah (1988) ameupa ushairi kipau mbele zaidi dhidi ya hadithi ndefu na natiki. Ushairi hapo kale, ulitangulia elimu ya falsafa, kabla ya ulimbe haujatamalaki ulimwengu wake.

2.1.5 Utafiti Uliofanyika Katika Mada za Ushairi

Khalifa (2013) alifanya utafiti kuhusu masuala ya kisiasa katika ushairi wa Kandoro, utafiti uligundua kuwa, mashairi ya Kandoro yamebeba dhamira zinazohusiana na ukombozi wa Mwafrika kutoka katika mikono ya utawala wa wakoloni na hatimaye kuweza kujitawala wenyewe. Mgogo (2012) alifanya utafiti juu ya matumizi ya nyimbo za Wanyiha misibani, katika kukamilisha kazi hiyo, alibainisha dhima ya nyimbo za jadi katika shughuli za misiba Unyihani ni kuwafariji wafiwa. Omary (2011) alifanya utafiti kuhusu masuala ya Siasa katika ushairi wa Kezilahabi, utafiti uligundua kuwa katika kitabu cha Karibu ndani (1988) na Dhifa (2008) kuna dhamira zinazojadili harakati za kisiasa. Alhabib (2012) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya taswira katika nyimbo za taarab, utafiti ulibaini kuwa, matumizi ya lugha ya taswira husaidia kuibua dhamira za kijamii.

Kazi za wanazuoni waliotutangulia zilitusaidia kufikia malengo ya utafiti huu, zilituongoza kutambua namna ya kuibua na kuchambua dhamira katika mashairi ya Bi Madina Ali Buhriy.

2.1.6 Umuhimu wa Mashairi

Bi Madina Ali Buhriy (2012) anasema, tangu jadi binadamu amekuwa akitumia mashairi kama uwanja maalumu wa kutolea hisia zake juu ya maadili, elimu, kuhimiza uwajibikaji, kuliwaza, kusifu, kukashifu n.k Katika kutekeleza wajibu huo, watunzi wa mashairi hawajifungi kimaudhui, bali hujaribu kutungia kila aina ya taathira ya maisha ya jamii.

Finnegan (1976) anasema Ushairi ni kisima cha hekima ya jamii ambamo kuna maelekezo, mafunzo, maliwazo, ushindi na shangilio la pumnzi ya jamii. Hivyo tunapozungumzia Ushairi simulizi, tunajadili nyimbo, ambazo zilitungwa na kuimbwa na jamii bila kuandikwa. Nyimbo hizo, zilizingatia miktadha ya nyakati k.v harusi, huzuni, tambiko, vita, ngoma, n.k. Kila utungo wa kishairi uliongozwa na matukio maalumu ya jamii.

Olson (1975) anaeleza kwamba, Ushairi wa Kiswahili ni chombo cha kuhamasisha matarajio na matamano ya Waswahili katika kujiletea maendeleo. Katika hali hiyo, Ushairi umekuwa chombo muhimu cha mawasiliano miongoni mwa wanajamii, kote ulimwenguni. Tunakubaliana na maelezo hayo, kwani tangu kale, Ushairi umekuwa ukitumika kama nguzo muhimu ya kubainisha matatizo yaliyomo katika jamii na kuyatafutia ufumbuzi.

Watunzi wa nyimbo, ngonjera na mashairi, wanatumia taaluma hii, kuipa jamii, mwelekeo sahihi wa maisha yao. Ushairi umekuwa ukitumika katika matukio ya sherehe, misiba, harusi, kuaga na kukaribisha mwaka, jando na unyago n.k. Data zilizochambuliwa katika kazi hii zimeonesha namna jamii inavyoweza kunufaika kutokana na tungo za Bi Madina Ali El-Buhriy.

2.1.7 Hitimishi

Utalii wa kazi tangulizi zilizosomwa na mtafiti zimedhihirisha kwamba, waandishi wa kazi za kishairi na watafiti wa tungo za kishairi wameweka mkazo katika kazi za washairi wakongwe waliozoeleka katika historia ya Arudhi ya Kiswahili kama Shaaban Robert, Saadan Kandoro, Mwanakupona binti Mshamu, Khatibu, Siti binti Saad, Mnyampala, Sengo, Amri Abed wa zama za miaka ya karne ya 19 hadi 21. Jamii inapaswa kutambua kwamba wapo wataalamu wengi chipukizi, ambao wanafanya kazi za kutosha. Mtafiti anaona ipo haja ya kuwaibua washairi wapya ili kuongeza hazina ya wataalamu wa umma wa Watanzania.

Katika kutekeleza azma hiyo, mtafiti ameona ni vema afanye utafiti huu juu ya mashairi ya Bi Madina Ali-Buhriy ambaye kazi zake hazijaingizwa katika mijadala ya wasomi wengi kwa mazoea finyu kwamba, kazi haiwi kazi, hadi iwe katika sura ya kitabu. Kazi za Bi Madina Ali-Buhriy, punde hivi zitatolewa kitabu kwa udhamini wa AERA Kiswahili Researched Products wa Gwiji la Kiswahili nchini, muasisi wa taaluma ya fasihi shuleni, fasihi simulizi vyuoni na taaluma ya Uhakiki wa kazi za Fasihi.

2.2 Mkabala wa Kinadharia

Neno nadharia ni dhanna. Wanazuoni wamejaribu kufasili dhanna hii kwa namna tafautitafauti kulingana na uweledi, mazingira na mielekeo kwa viwango na tajriba za usomi wao. Owhida (2006) anasema nadharia ni kauli nzito zinazotokana na uchunguzi wa data. Nadharia huweza pia kuwa ni fikra au mawazo ya mtu mmoja au kikundi cha watu kuhusu kitu au jambo la kweli au la kudhani, ama ni mwelekeo wa mtu au watu, katika kusaidia kupata ukweli au kuthibitisha uongo kwa lengo

maalumu. Sengo (2009), anasema, nadharia ni wazo kuu, fikra kuu, mwongozo mkuu wa mtu au watu (jamii), wa pahala fulani, wakati fulani, kwa sababu fulani. Nadharia ya utafiti ni mwongozo wa kufuata wakati wa kufanya utafiti k.v. kuchambua data za kifasihi. Njogu (2007), anasema, nadharia ni miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi ya fasihi, kuifahamu kazi ya fasihi katika vipengele vyake vyote. Nadharia ni maelekezo ya jambo la kufungamana na vigezo vilivyowekwa au vinavyopatikana kutokana na majaribio ya jambo hilo. Katika kazi hii, mtafiti amechambua nadharia na amezitumia kama mwongozo na dira na kujenga mwelekeo wa utafiti huu.

2.2.1 Ufafanuzi wa Nadharia

Zipo nadharia nyingi ambazo hutumika katika kuchunguza na kuhakiki kazi za fasihi. Nadharia mpya huibuka na zile za zamani huanza kupoteza umaarufu wake kwa watumiaji. Hali hii inatokana na ukweli kwamba, katika fasihi na sayansi za jamii kwa ujumla, hakuna kimoja kilicho sahihi popote wala milele. Kilichokuwa sahihi jana, kinaweza kisiwe sahihi leo Carter (2006) na Mushengyezi (2003), hakuna nadharia bora zaidi ya nyingine, nadharia zote zina uzito sawia kutegemeana na kazi inayochunguzwa. Ntarangwi (2004) anashadidiya kwa kusema kila nadharia ni bora kuchunguza kazi fulani ya fasihi, lakini inaweza isifae kufanikisha kuchunguza kazi nyingine.

2.2.2 Nadharia ya Kijamii

Nadharia ya kijamii ilianza kujitokeza katikati ya karne ya kumi na tisa na kushamiri katika karne ya ishirini. Mwanzilishi wa nadharia hii ni Mfaransa Hippolyte Taine, (1828-1893). Kwa mujibu wa Taine (1863) mazingira, hali halisi ya maisha na asili,

huamua, namna sanaa inavyotakiwa kuwa. Kazi ya sanaa ni nakala ya tabia, mila na dasturi na kiwakilishi halisi cha jamii iliyo hai kwa wakati maalumu. Nadharia ya kijamii wanaiona kwamba, ni vigumu kuitenga fasihi na masuala ya kijamii.

Kwa kufanya hivyo, sanaa huhubiri maisha ya mwanadamu juu juu na kutimiza suala la burudani ambalo ndilo tokeo la mafunzo mengi yaliyotokana na kazi inayohusika. Fasihi ilionekana kama ghala la hekima za jamii na nyenzo kuu ya kuhifadhi hatua za maendeleo ya jamii. Bascom, (1959); Shorter, (1969); Okpewho, (1992); Mulokozi, (1996); Mushengyezi, (2003) wanakubaliana kwamba, kazi ya sanaa inatokana na jamii, haiwezi kutazamwa na kupimwa kutoka kwenye ombwe tupu, bali historia ya watu hao, mila na tamaduni zao, uchumi na siasa yao vinapaswa kuzingatiwa. Kwa kuwa ni vigumu kwa kazi ya fasihi kujitenga na masuala ya kijamii k.v tabia, mila na dasturi, siasa, uchumi, malezi, mambo hayo ni ya kuzingatiwa wakati wa uchunguzi wa kazi za fasihi. Utafiti huu umetalii kwa kina kazi ya Bi Madina Ali-Elbuhriy, kwa kubainisha dhamira zilizojitokeza ndani ya mashairi yake.

Msisitizo mkubwa katika nadharia ya kijamii ni namna fasihi inavyotenda kazi za jamii. Utendaji kazi wa fasihi ni namna, sanaa inavyotimiza wajibu wake wa kutoa maelekezo sahihi kwa wanajamii, ikiweka wazi maovu yanayotendwa na makundi tafautitafauti. Nadharia hii ilitusaidia kutukumbusha na kushadidia kuwa, dhima ya fasihi ni kuitumikia jamii. Kwa kuzingatia kipengele hiki, mtafiti alilazimika kusoma kwa kina mashairi ya Bi Madina Ali-Elbuhriy, hatimaye alifanikiwa kuibua dhamira kumi na mbili zenye ujumbe ambao, iwapo utatumika vizuri, jamii inaweza kupata

maelekeo yanayofaa maishani. Jamii itaepuka ugomvi kwa kutenda mambo mema, jamii itatunza mazingira, jamii itajiepusha na rushwa n.k.

2.2.3 Nadharia ya Semiotiki

Semiotiki ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara, ambalo hutumika kuelezea mialekeo na makundi fulani ya kihakiki. Semiotiki au Semiolojia kama wengine wanavyoliita ni nadharia ya uhakiki wa fasihi iliyoasisiwa na mwanaisimu miundo Ferdinand de Saussure na mwanafalsafa Charles S. Pierce, Eagleton (1996). Historia ya Semiotiki ilianza kujitokeza katika miaka ya 1960 na kushamiri katika miaka ya 1970 na iliwekewa misingi na shule ya Isimu ya Prague hadi leo hii inapohusishwa na wahakiki kama; A.J Greimas, T. Todorov na Roland Barthes.

Kwa mujibu wa mwanafalsafa C. S. Pierce na mwasisi wa nadharia ya Semiotiki anatafautisha aina tatu za ishara, Eagleton 1996 anasema,

Katika usemi huwa kuna ishara (iconic) ambapo kishirizi chake husimama badala ya kinachoashiriwa, ishara (indexical) ambapo kiashirizi chake kinahusiana na kiashiriwa, na ishara (symbolic) ambapo kwa mujibu wa de Saussure kiashirizi hakina uhusiano wowote na kinachoashiriwa (Tarjama yetu).

Maelezo ya Pierce yanajiegemeza katika kuichambua lugha inayotumika katika fasihi. Tafauti na kwenye masomo ya Ulimbe, fasihi hutumia lugha, wahusika na mazingira katika kuelezea hali fulani. Matumizi ya ishara katika fasihi huongeza dhanna za ziada katika kazi husika, ambazo mtazamaji, msikilizaji au msomaji huzipata baada ya kuhusisha kila kipengele kinachojitokeza katika muktadha husika

na hali ya sanaa inayotendwa. Kwa mfano *ishara ambapo kwa mujibu wa de Saussure kiashiria hakina uhusiano na kinachoashiriwa*. Hii ni kusema kwamba, utamaduni wa jamii au hali halisi ya maisha ya jamii inayozalisha sanaa husika itatumika kuchambua dhanna zinazowasilishwa katika vipengele vya kisanaa vinavyotumiwa katika sanaa hiyo.

Nadharia ya Semiotiki katika upana wake, inahusu ishara. Kwa mujibu wa nadharia hii, lugha na fasili yake, ni mfumo wa ishara zenye maana. Ishara ni kichocheo ambacho huzusha akilini mwetu dhanna inayorejelewa. Kila ishara ina umbo na dhanna inayorejelewa kutegemeana na utamaduni wa jamii husika. Hii ina maana kwamba kila kipengele kinachotumika katika kazi ya fasihi inayowasilisha dhanna fulani katika muktadha wa jamii inayotumia fasihi hiyo. Matumizi ya mbinu fulani ya kifani au hata kipengele cha kimaudhui katika mashairi si ya kibahati nasibu, bali yana maana katika fasihi yenyewe na fasihi kwa ujumla, Guiraud (1975). Mashairi kama ilivyo sanaa yoyote hutumia lugha, na lugha hubeba maana mbalimbali za kiutamaduni wa kijamii, kwa hiyo nadharia hii ilitusaidia kuchambua matumizi ya lugha katika mashairi ili kuona dhanna mbalimbali zilizomo katika kipengele cha tamathali za usemi.

2.2.4 Nadharia ya Uhalisia

Sengo (2009) Nadharia ya uhalisia ni hali halisi ya pahala fulani au jambo fulani. Penye ukame huzungumzwa njaa, kutopatikana kwa maji na taabu za kukosa vitu fulani fulani. Uhalisia wa kimiktadha na mandhari ya kazi za fasihi, imejikita katika kweli zote ziihusuzo hali hiyo. Mtunzi au mwandishi alivyo, alikozawa, alikolelelwa, alikosomeshwa na uwakala aliorudi nao, au na uzalendo alo nao. Uhalisia ni nadharia

pana na kubwa, isipelekwe Ulaya wala Marekani, Uhalisia usomwe viamboni, vijijini, mtaani na nadharia itumike kwa upana wake. Sengo anaona kwamba, katika jamii yake, mambo yote yanayofanyika hujikita katika mazingira halisi.

Kwa mujibu wa Ntarangwi (2004), nadharia hii katika upana wake, ni ya uwakilishi wa uhalisia wa mambo katika fasihi. Mhalisia husadiki matokeo ya mambo na ukweli anaouzingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa na uzoefu maishani. Vile vile, wanauhalisia huichukulia dhana ya demokrasia, kama hali ya maisha, na malighafi ya kuelezea maisha ya kawaida ya kila siku. Hivyo uhalisia wa Afrika, hujikita katika mambo yaliyopo, matukio mahsusi na matokeo yanayoweza kuonekana. Kazi ya fasihi yapaswa kuwaweka wanajamii husika katika ulimwengu wao wa kawaida, wa kweli, na halisi. Hivyo, picha za ulimwengu atakazounda msanii, zapaswa kudhihirisha hali hiyo.

Mhakiki anayezingatia nadharia hii ya uhalisia, hupembua namna mtunzi alivyodhihirisha uhalisia wa mambo kupitia kwa wahusika aliowasawiri. Hivyo, mhakiki hutazama jinsi ukweli ulivyodhihirishwa katika juhudi za mtunzi za kuchora hali halisi ya mambo katika wakati maalumu. Kwa muhtasari, msanii anatarajiwa kusawiri wahusika, matukio na mandhari yanayokubalika na kuaminika katika jamii ya wakati huo. Ufahamu wa mazingira na maisha anayoyalenga mtunzi ni nguzo muhimu kwa mhakiki wa kiuhalisia. Watu wa Ulaya huko Ufaransa Emmanuel Kant, Schiller, Flaubert wanaihusisha dhana ya uhalisia na mambo mawili, kwanza inatumika kama njia ya kutathimini uhalisia wa maisha. Pili hutumiwa katika uhalisia wa kifasihi unaoashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakika wa maisha. Hiyo fasili ya pili, ndiyo iliyotumika huko Ufaransa

katika mwaka 1850 kuelezea kazi ya sanaa iliyoonesha maisha ya binadamu jinsi yalivyokuwa.

Katika kufafanua nadharia ya uhalisia, Kant (1790), Schiller (1798), Flaubert (1800), wanamtazama mtunzi kwa jicho la mbali zaidi. Mfano, mtoto anapokuwa mchezoni, hufanana na mtunzi ambaye huunda ulimwengu wake, au huvipanga upya vitu katika ulimwengu wake, ili vimpendeze. Kulingana na nadharia hii, mtunzi hufanya kazi yake sawa na mtoto anayecheza, isipokuwa mtunzi hutumia visa halisi. Kwa upande mwingine, mtunzi anafahamu kuwa hatarajiwi kuendelea kucheza au kuota, kamaafanyavyo mtoto, bali hupaswa kutenda mambo kiuhalisia na kiutu uzima. Baadhi ya matamania yanahitaji kusitiriwa, yasijulikane kwa wengine, kwani huwa ni faragha nzito za kijamii. Kazi ya fasihi, kulingana na mtazamo huo, huwa ni jaribio la kutimiza matamania ya mtunzi juu ya mambo anayoyaona ama kuyasikia ndani ya jamii yake na kutaka yasomwe katika uhalisia huohuo wa kimaumbo.

Sengo (2009), Ntarangwi (2004), Kant (1790), Schiller (1798), Flaubert (1800) wanakubaliana kuwa, lengo la mtunzi wa kazi ya fasihi ni kuonesha ukweli jinsi ulivyo. Kulingana na wataalamu hao, mtunzi anapaswa kutoa picha ya jamii bila kuidunisha wala kuipigia chuku. Mtafiti alitumia nadharia hii kwa kuona uhusiano wa karibu na utafiti huu, hasa kwa kupembulia, kwa kina, dhamira zilizojitokeza katika mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy na kubainisha namna zinavyofungamana na hali halisi ya maisha ya Watanzania.

2.2.5 Hitimishi

Katika utafiti huu nadharia zilizoteuliwa kutumika ni tatu, nadhairia ya kijamii, nadharia ya kiuhalisia na Semiotiki. Mhalisia husadiki matokeo ya mambo na ukweli

anaouzingatia ni ule unaoweza kuonekana na kuthibitishwa na uzoefu maishani. Imetusaidia kuibua dhamira zilizojitokeza katika mashairi. Nadharia ya uhalisia na nadharia ya kijamiizimetusaidia kupata ukweli wa dhamira zinazojitokeza na hali halisi ya maisha ya Watanzania ambao, ndiyo jamii lengwa katika utafiti huu. Nadharia ya Semiotiki imetusaidia kuchambua matumizi ya tamathali za usemi, kwani msingi wa nadharia hiyo, ni taaluma ya mfumo wa alama katika mawasiliano ya kutumia lugha.

SURA YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti ametaja na kufafanua mbinu zilizotumika katika kukusanya data na zana za kukusanyia data zilizotumika.

3.2 Mbinu za Kukusanyia Data

Mgogo (2012) anasema, mbinu ni namna mtu anavyoweka mikakati ya kufanikisha jambo lake. Mbinu za kukusanyia data za utafiti, ni namna mtafiti anavyoandaa njia maalumu zitakazomwongoza mtafiti kupata data anazozihitaji katika utafiti wake. Maelezo hayo ni muhimili mkuu wa ukusanyaji wa data katika kazi hii. Kwa kuzingatia maelezo hayo, umakini ulitumika kupata njia sahihi zilizotuwezesha kupata data zilizohitajika.

3.2.1 Usaili

Usaili ni mbinu ya kukusanyia data kwa njia ya mazungumzo ya ana kwa ana baina ya mtafiti na mtafitiwa. Babbie, (1999) na Omari (2011), kwa mbinu hii mtafiti aliweza kukusanya data kutoka kwa ndugu wa karibu na Bi Madina Ali El-Buhriy pamoja na Bi Madina Ali El-Buhriy mwenyewe, kwa pamoja, walitupatia data zilizotuwezesha kupata majibu ya maswali ya utafiti yanayoonekana katika sehemu ya kwanza ya utafiti.

3.2.2 Upitiaji wa Nyaraka

Kothari (2008) anaeleza kwamba, upitiaji wa nyaraka ni mbinu ambayo inamuhitaji mtafiti kupanga kile ambacho anataka kukisoma katika nyaraka hizo. Hali hiyo

itamsaidia mtafiti kutumia muda wake vizuri. Katika utafiti huu tulipitia nyaraka zilizotuongoza kupata data za upili. Tulitalii machapisho ya mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy, tasnifu na vitabu ambavyo vilikuwa ni msaada wa kupata mwelekeo wa kazi hii ya kiutafiti.

3.2.3 Wasaidizi Katika Kukusanya wa Data

Mgogo (2012), Robert (1991) wanasema kwamba, kazi ya wasaidizi ni kumtambulisha mtafiti masikanini kwa mtafitiwa/watafitiwa ili wampatie ushirikiano. Kwa vile mtafiti ni mgeni masikanini, alilazimika kutafuta wasaidizi wa kazi yake. Wasaidizi hao walikuwa ni wenyeji wa eneo hilo, wenye kuaminika na jamii. Mwendelezo wa kuwapata watu hao, ulifanyika baina ya mtafiti na msimamizi wa kazi hii (Sengo 2012). Njia hii ilimrahisishia mtafiti kufika na kupokewa masikanini katika familia ya Bi Madina Ali El- Buhriy na kupata data zilizohitajika bila matatizo yoyote.

3.3 Ukusanyaji wa Data

Kothari (2008) anasema, ukusanyaji wa data unahusisha taarifa zilizopo katika maandishi na zile ambazo hazipo katika maandishi. Anaendelea kutaja maandiko hayo kuwa ni vitabu, tasnifu, magazeti, makala na majarida. Taarifa ambazo hazikuandikwa hupatikana kwa mawasiliano ya ana kwa ana.

3.3.1 Vyanzo vya Data

Utafiti huu ulitumia data za aina mbili, data za msingi na data za upili kwa kuzingatia vyanzo vilivyoanishwa hapo chini.

3.3.2 Data za Msingi

Kothari (1992) anasema, data za msingi ni zile ambazo zinakusanywa na mtafiti kwa mara ya kwanza kutoka masikanini, na hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine kwa mahitaji ya utafiti kama huo unaofanywa sasa. Katika utafiti huu, data za msingi zilipatikana kutoka kwa Bi Madina Ali El-Buhriy na familia yake katika mambo waliyoulizwa na mtafiti.

3.3.3 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo tayari zimekusanywa na watafiti wengine na kuchapishwa katika ripoti, tasnifu, makala, magazeti au vitabu. Merrian (1998) anasema, katika Maktaba mtafiti huweza kupata data nyingi, kwa urahisi bila gharama. Hivyo mtafiti alitembelea Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

3.4 Uteuzi wa Walengwa

Kombo na Tromp (2006), wanasema, walengwa ni kundi wakilishi la watafitiwa, linaloweza kutoa majibu ya maswali ya mtafiti. Webster (1985) anasema kundi la walengwa ni kundi la watu wachache, lililoteuliwa kutoka katika kundi la watu wengi, kwa ajili ya kufanyiwa utafiti. Walengwa wanaweza kuwa, watoto, wakulima, wavuvi, watumishi wa afya, madereva au mtu yeyote mwenye taarifa zinazohitajika na mtafiti n.k.

Keys, (1989) anasema uteuzi wa walengwa ni wa kundi dogo la watafitiwa, lililochaguliwa katika kundi kubwa, na kuwa ndio wawakilishi wa kundi hilo lote. New Man, (2006) anasema uteuzi wa walengwa ni kundi ambalo mtafiti huliteua,

akiwa na mategemeo kwamba, litampatia data itakayowezesha kukamilisha madhumuni ya utafiti wake. Kwa msingi huo, kundi lengwa katika kazi hii ni, kazi zote za Ushairi wa Bi Madina Ali El-Buhriy, ambazo zimeoneshwa katika tasnifu hii, familia yake k.v Salimu Ali Kibao, Sheikh Mohamed Ali, Mwalimu wake mzee Ali Maftaha, UKUTA, magazeti ya UHURU, MZALENDU MWANANCHI n.k

3.5 Zana za Utafiti

Zana za utafiti ni jumla ya vifaa vyote vilivyotumika katika ukusanyaji wa data. Katika kazi hii mtafiti alitumia zana kwa kuzingatia, upatikanaji wa kila zana.

3.5.1 Kalamu na Karatasi

Kalamu na karatasi ni zana za msingi katika utafiti wa kitaaluma. Kalamu ni kifaa ambacho kilitumika kama nyenzo ya kuandikia majibu ya usaili na majadiliano, kati ya mtafiti na mtafitiwa. Karatasi ni kifaa ambacho kilitumika kutunzia kumbukumbu za data zilizokusanywa kabla hazijachambuliwa.

3.5.2 Ngamizi

Kifaa hiki kilitumika kwa namna mbili katika kazi hii. Kwanza, kilitumika katika kukusanyia data za upili kwa njia ya wavupepe, pili, kifaa hiki kilitumika wakati wa kuchapa ripoti ya tasnifu hii.

3.5.3 Simu ya Mkononi (Rukono)

Kifaa hiki kilitumika kwa ajili ya mawasiliano kati ya mtafiti na watafitiwa ili kufanya makubaliano ya muda na mahali pa kukutania kwa ajili ya majadiliano, mahojiano au usaili. Umuhimu wa kifaa hiki ni kwamba, kilimwezesha mtafiti kufanikisha mipango yake kwa muda mfupi, na kwa ufanisi mkubwa.

3.5.4 Hitimishi

Sura hii imewasilisha mbinu za utafiti ambazo zimetumika katika kukusanya data za utafiti huu. Mbinu hizo zinajumuisha zile za Masikanini na Maktabani. Mbinu za maktabani zinajihusisha na usomaji wa kazi tangulizi zinzohusiana na mada ya utafiti huu. Vile vile data za msingi zilipatikana kwa kusoma kwa umakini mkubwa, mashairi ya Bi Madina Ali El – Buhriy pamoja na kufanya mahojiano ya ana kwa ana na mtafitiwa.

SURA YA NNE

4.0 UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa matokeo ya utafiti kuhusu mada ya utafiti huu. Hivyo, tunachambua maudhui, dhamira, zinazojitokeza katika mashairi na tenzi za Bi Madina Ali El-Buhriy, na namna anavyosawiri hali halisi ya jamii.

4.2 Uchambuzi wa Data

Kipengele cha uchambuzi wa data kinahitaji umakini, utulivu na ufahamu mkubwa. Katika hatua hii, mtafiti anashauriwa kuzingatia mambo matatu muhimu, ni lazima mtafiti azijue data zisizohitajika na aziondoe katika kazi yake. Pili atambue data zenye majibu yasiyo na mwelekeo. Aondoe utata huo kwa kuwashirikisha watafitiwa. Tatu atambue majibu yenye mgongano katika swali moja (Kombo na Tromp 2006).

Baada ya kukusanya data, mtafiti anapaswa kuzichambua kulingana na matarajio ya utafiti huo. Uchambuzi wowote humsaidia mtafiti kupata ukweli wa madhumuni aliyojiwekea. Kothari (2003). Davies (2002), wanasema, data ipo ngazi ya chini, taarifa ni ngazi ya pili na hatimaye maarifa ni ngazi ya juu kati ya zote tatu. Ili data ibadilishwe kuwa ripoti ya kazi, ni lazima ifasiliwe.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2003) wanasema, data hutoa jibu la swali la utafiti na ili matokeo ya utafiti yaweze kuaminika na kukubalika, lazima yachambuliwe vizuri. Data za utafiti huwa nyingi na katika mchanganyiko mkubwa. Mtafiti hulazimika

kuzichambua kwa umakini ili aweze kutoa taarifa kamili kwa wasomaji wa kazi hiyo.

4.3 Dhamira katika mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy

Katika sehemu hii tutajibu swali la pili, swali linalosema, Ni dhamira zipi zinazopatikana katika tungo za Bi Madina Ali El-Buhriy? Dhamira ni sehemu mojawapo tu ya maudhui ya kazi za fasihi, ni Ndungo na Wafula, (1993). Dhamira ni wazo kuu lililomo katika kazi ya sanaa. Ndungo na Mwai (1991) wanasema maudhui ni ujumbe maalumu katika kazi ya fasihi, maudhui katika shairi hupatikana baada ya mhakiki kupitia beti zote za shairi na kisha kujumlisha yote anayoyapata. Beti za Ushairi hutokana na hamu ya mshairi kutaka kuwasilisha hisia au maoni yake kuhusu jambo. Ushairi ni nyenzo ambayo imekuwa ikitumiwa na wasanii kuwasilisha hisia au maoni yao kuhusu mambo fulani. Hisia hizo, huwa ni mambo au matukio ya kweli yanayoathiri hisia za msanii.

4.3.1 Dhamira ya Utunzaji wa Mazingira

Bi Madina Ali El-Buhriy ni mwana harakati wa jitihada za utunzaji wa mazingira, anatoa hisia zake namna jambo hili linavyomgusa, anaonesha kukerwa na watu wanaochafua mazingira. Ameshindwa kuwafumbia macho, sasa anasema; (uk 131)

Tusitupe takataka, zilo ngumu na mipira
Majaa pamwe vichaka, ni mazalio ya vyura
Ni kero kuzilundika, tusijifanye wakora
TUYATUNZE MAZINGIRA, ILI YAPATE TUTUNZA

Watu wanaoharibu mazingira, wanafananishwa na wakora, yaani wahuni, magwagu, majangili n.k, ambao kazi yao ni kuhatarisha uhai wa binadamu wenzao na wao wenyewe. Uchafu ukikithiri katika mazingira yetu ni chanzo cha karaha.

Na maradhi yanataka, sehemu isiyo bora
 Malaria, kutapika, pia gonjwa la kuhara
 Tusidhani kutambika, ndiyo njia ya kung'ara
TUYATUNZE MAZINGIRA, ILI YAPATE TUTUNZA

Katika ubeti wa hapo juu, Bi Madina Ali El-Buhriy anatumkumbusha juu ya athari za uharibifu wa mazingira, anataja magonjwa yanayotokana na uchafu wa mazingira kuwa ni kuhara na kutapika. Kwa hakika, nchi nyingi za dunia ya tatu, Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi hizo, bado tunasumbuliwa na magonjwa ya milipuko, hasa kipindupindu na homa ya matumbo. Serikali inatumia dola nyingi za kimarekani kwa kuagiza dawa za tiba ili kukabiliana na matatizo hayo. Leo hii Bi Madina Ali El-Buhriy, anatumia tiba isiyohitaji matumizi makubwa ya fedha za kigeni, tudumishe usafi wa mazingira yetu. Serikali ifanye jitihada za makusudi, kuhimiza halmashauri zote nchini kuweka mipango thabiti ya kupambana na wachafuzi wa mazingira yetu. Halmashauri za miji, majiji na wilaya hadi vijiji zitunge sheria ndogondogo za kushughulikia suala la mazingira, kwa kufanya hivyo, tutaepuka magonjwa ya milipuko na Tanzania itaendelea kuwa na mazingira bora ya kuishi anataja kundi la wamiliki wa viwanda kuwa wapo mstari wa mbele katika uharibifu wa mazingira ya mwanadamu. Kwa ujasiri mkubwa, msanii anasema kwamba;

Wenye viwanda pulika, wengine nyie majura
 Kemikali zamwagika, hamjui mwatukera
 Nini mnachokitaka, au mpigiwe vura
TUYATUNZE MAZINGIRA, ILI YAPATE TUTUNZA

Tatizo linalojitokeza katika harakati za maendeleo ya kisasa ni uchafuzi wa mazingira, ujenzi wa viwanda vingi ambao umeshindwa kuzingatia usalama wa afya

na makazi ya watu. Mara nyingi tumesikia migogoro kati ya wamiliki wa viwanda na raia Wakazi wa Jiji la Mwanza, la Dar Es Salaam, la Tanga na Manispaa za Mtwara na ya Lindi, kila mara wamekuwa na ugomvi baina yao na wamiliki wa viwanda vya samaki kwa ajili ya uchafuzi wa mazingira. Wamiliki wengi wa viwanda wameshindwa kujenga mifumo mizuri ya kuondoa takataka kutoka katika viwanda hivyo na kutupwa kulikopangiwa uchafu huo. Katika kutatua tatizo hili Wizara ya Nyumba na Makaazi nayo inapaswa imulikwe, ikumbushwe kuepuka kutoa vibali kiholela kwa wenye viwanda bila kuzingatia afya za wananchi.

Mazingira ni jambo pana mno na nyeti katika maisha ya mwanadamu. Utunzaji wa mazingira ni jambo linalopaswa kuzingatiwa sana kwa kila mtu mwenye huruma na taifa lake. Ushahidi upo unaoonesha kwamba jamii zilizoshindwa kutunza mazingira yake, leo hii zinaishi maisha magumu, ya kuombaomba. Zinasumbuliwa na ukame usiyo kifani, zinakosa maliasili zilizotoweka baada ya kuharibika kwa ikolojia ya asilia.

Hali ya Kaskazini Mashariki ya nchi ya Kenya na Somalia, wanyama wanakufa kwa idadi kubwa, kwa sababu ya ukosefu wa maji, janga ambalo chanzo chake ni uharibifu wa mazingira. Hapa nchini tunashuhudia na kuona, katika vyombo vya habari, magazeti na runinga, jinsi akina mama wanavyohangaika kutafuta maji kwa ajili ya mahitaji ya familia zao. Mwisho Bi Madina Ali El-Buhriy, anasisitiza kuwa:

Kaditimati natweka, chondechonde MAZINGIRA

Tuyatunze akina kaka, kina dada kirakira

Wito natoa Tandika, mpaka kule Kagera

TUYATUNZE MAZINGIRA, ILI YAPATE TUTUNZA

Mazingira yasiyo salama yanasababisha ongezeko la joto duniani, mvua nyingi ya kupitiliza ama ukame (elnino na lamina), maradhi kama kansa, magonjwa ya kupumua kama athma na kifua kikuu, homa za matumbo, dengue, chanzo cha matatizo hayo ni uharibifu wa mazingira. Tujenge mazingira bora ili tupate, hewa safi, vyanzo vya maji, fedha za kigeni kupitia utalii unaotokana na utunzaji wa hifadhi na mbuga za wanyama.

Pia kupitia utunzaji wa mazingira tunaweza kupata dawa za miti, asali, chakula matundapori na mbogapori. Makaazi ya viumbe hai, yaani binadamu na wanyama wa mwituni, wadudu, ndege, mimea n.k yatabaki kuwa ya amani na salama. Udugu wa miti na mimea na mwanadamu, si wengi wanaoujua na kuuthamini. Bila ya Oksijeni na Kabonidayoksaidi, viumbe vyote haviwezi kuishi. Kwa hiyo mazingira yanapaswa kutazamwa kwa jicho pana na kwa karibu sana.

Kwa upande mwingine, mazingira ni jambo linalogusa wanafasihi wengi kote ulimwenguni. Plekanov (1957) anabainisha kuwa, fasihi ni chombo kimojawapo katika vyombo vya harakati dhidi ya mazingira. Kwa mtazamo huo sanaa haina budi kutumiwa kumsukasuka na kumzindua binadamu ili ayatunze mazingira yake. Ili fasihi simulizi iwe na manufaa katika jamii ni lazima iwe ni chombo kinachoaminika katika kufichua maovu ya jamii kwa lengo la kuutokomeza unyonge na uchafu uliokithiri katika jamii zetu. Wanafasihi wameanzisha mapambano ya utunzaji mazingira, hima kwa serikali, taasisi zisizokuwa za kiserikali na watu binafsi kuunga mkono na kuendeleleza harakati za kutunza mazingira na raslimali zilizopo. Kama kila mmoja atashiriki katika sehemu yake, Tanzania itakuwa ni kielezeo kizuri katika utunzaji wa mazingira ndani na nnje ya bara la Afrika.

Waziri wa Maji, wakati wa kusua mradi mpya wa maji katika manispaa ya Moshi, Januari, 2014. Alikumbusha juu ya utunzaji wa mazingira kwa kusema, Uhai wetu, ustawi wetu, afya zetu na maendeleo yetu, vyote, hutegemea, upatikanaji maji safi na salama pale tunapoishi. Wakati umefika, tuone, kila anayeharibu chanzo cha maji, ni adui, Tanzania itaendelea kupoteza viumbe hai na mimea kwa wingi. Hivi karibuni, athari za kukauka kwa mito, zimewasibu wananchi katika sehemu mbalimbali za Tanzania. Hata hivyo hakuna juhudi thabiti zinazofanywa na jamii au asasi za Serikali kukabili uharibifu wa kimazingira.

4.3.2 Dhamira ya Umalaya Katika jamii

Abdilatif (1980) anasema, kazi ya fasihi si kuyaeleza yale yaliyo mema tu na yapendezayo kusikiwa, bali kadhalika, ina kazi ya kuyaeleza hadharani, yale yote maovu, yatendekayo, ili yajulikane na yapate kutafutiwa dawa zake kabla hayajaozeoana na hatimaye kuiletea khasara jamii nzima. Umalaya ni hali au mwenendo wa mwanaume au mwanamke kufanya uasherati na makahaba wakitumia miili yao kama bidhaa. Umalaya na athari zake ni jambo linalozungumzwa katika kila kona, za watu waadilifu. Walimu na wazazi wanalalamikia watoto wao wanaokatisha masomo kutokana na kujiunga na makundi ya makahaba, Mahakamani na taasisi za Dini zina asa waumini wao kuepuka kusalitiana katika ndoa, halmashauri za miji na majiji zinaeleza juu athari za kuwepo kwa madanguro. Mambo haya yanapaswa kupewa nafasi ya kujadiliwar kijamii, lengo kubwa ni kujaribu kunusuru madhara makubwa yanayotokana na tatizo hilo. Uadilifu uanze nyumbani, mitaani, shuleni, kwenye nyumba za ibada, mahakamani hadi maishani. Uhimizaji wa mema na ukemeaji wa maovu ufanyike kwa nguvu zote.

Bi Madina Ali El-Buhriy aliguswa na swali hilo, akaiangalia jamii yake ya Uswahilini, kwa jicho la kisanii, akazama kwa ustadi mkubwa. Aliiangaza jamii ya Waswahili, kuanzia katika ngazi ya familia na makundi ya rika zote, wakiwemo, vijana, wazee, akina mama na akina baba, akina dada na akina kaka, matendo yao yote yazingatiwe, hatimaye yawekwe hadharani kwa kutumia sanaa ya Ushairi. Umalaya unaonekena kuwa ni moja ya matatizo makubwa na sugu Uswahilini. Wanawake ndiwo wenye kulalamikiwa zaidi juu ya tabia hiyo. Bi Madina Ali El-Buhriy aliibuka hadharani na shairi la *Kisichofunga Kipochi*'(uk 136)

Labeka napiga goti, naitika bila kefu
 Nasema japo kwa chati, kidogo kwa uratifu
 Huo wako utafiti, hakika umesadifu
KISICHOFUNGA KIPOCHI, KWANGU HAKIPATI HADHI

Kingejaa majinoti, ya mia na maelufu
 Kisibane katikati, japo kwa chake kikufu
 Kabisa sikifumbati, radhi nishike hanjifu
HADHI HAKINA DAIMA, KISICHOFUNGA KIPOCHI

Wengi tunatambua kuwa miongoni mwa matumizi ya pochi ni kuhifadhi vitu vya thamani. Usalama wa kifaa hicho ni kuwapo kwa zipu inayobana katikati ili vitu vilivyomo ndani yake visionekana ama kumtamanisha mtu mwingine kwa nia ya kupora. Katika muktadha wa kazi hii, neno kipochi limetumika kama sitiari, Bi Madina Ali El-Buhriy anafananisha sehemu za maungo mateke ya mwanamke na pochi. Mwanamke ama mwanaume mwenye tabia ya umalaya anafananishwa na pochi iliyokosa zipu, muda wote ipo wazi, inakosa thamani na hadhi. Mtafitiwa Bi Madina Ali El-Buhriy anaeleza kuwa, mwanamke ni mtu anayetakiwa kujisitiri, kujiheshimu, awe mtulivu na mwenye subira, aepuke tabia ya wanaume wanaohitaji

kufanya naye kitendo cha kujamiana nje ya ndoa. Aonavyo Bi Madina Ali El-Buhriy (2013) ni kwamba, mwanamke yeyote mwenye tabia kama hiyo, si mwanamke mwema, hafai kuolewa na kuitwa mama bora wa familia. Anaendelea kusema.

Huwezi kuwadhibiti, wenye mikono mirefu

Usiruo kama nyati, hauwapi usumbufu

Watakuacha laiti, umepasuka mapafu

KISICHOFUNGA KIPOCHI, HADHI KWANGU HAKIPATI’.

Mapenzi ni huruma ya kufanyiana makubwa zaidi ya kimaisha kuliko ngono. Uchaguzi wa jema au baya hutegemeana na hulka ya mtu binafsi katika kutawala hisia zake. Wahenga hawakukosea, waliposema sema, asali ukiisha iramba, sharti uichongee mzinga. Mwanamke akifanya kosa la makusudi la kuruhusu kufanya kitendo cha ndoa na mwanaume wa wizi, hilo ni doa katika maisha yake. Wanaume wajinga huambizana, na kila mmoja hupenda kutupa karata yake, ili kukidhi haja zake.

Katika jamii za kiafrika, mwanamke amepewa nafasi kubwa ya vyeo tisa ndani ya familia; yeye ni mama, dada, mke, binti, nyanya, shangazi, mama mkwe, shemeji na mama mkwe. Kwa hadhi hiyo, mwanamke ni mama wa jamii. Kwa mtazamo huu mwanamke ni mwalimu wa kwanza katika familia. Mwalimu yeyote ni kielezeo bora cha jamii. Matendo na mwenendo wake unapaswa uwe bora ili watu wa makundi yote ya kijamii, waige kutoka kwake. Bi Madina Ali El-Buhriy anasimama kama mama wa familia katika jamii ya Waswahili, anatoa mapendekezo yake, namna ya kupambana na kadhia hii. Katika shairi la *usisubiri*, anatanabahisha. (uk150)

Jambo jema kusubiri, subira huvuta kheri
 Subira ni jambo jema, lisokuwa na dosari
 Mwishowe huwa mzuri, mambo yanaposhamiri
NAKWAMBIA USUBIRI, NA WALA USIFIKIRI

Nishaugonga muhuri, nishaapa kwa Qahari
 Nakesha nimekariri, ndani ya yangu suduri
 Ninakuaga kwa kheri, nishaikata amari
NASEMA SISUBIRI, NA WALA USIFIKIRI

Katika dondoo hilo hapo juu, Bi Madina Ali El-Buhriy, analeza kuwa, mwanamke ajivunie uanajike wake. Wanapoamua kuingia katika uhusiano wa kujamiana, lazima wawe makini na wanaume wakorofi, wanaopenda kuwaharibia mabinti maisha yao kwa visingizio vya kuwaoa. Mwanamke alielelewa katika maadili mema, kabla ya kuingia katika uhusiano, hawezi kusita kuongozwa na kauli hizi, *Jambo jema kusubiri, subira huvuta kheri*. Kutokana na muktadha wa kazi hii, mwanamke asikubali kufungua *pochi* kabla hajafanya uchunguzi wa kina kumruhusu mwanaume anayemtaka, subira ifanyike kwanza, ni vizuri wachunguzane. Kwa muono wa Bi Madina Ali El-Buhriy, wanaume wengi wanapotaka kuo, hawako tayari kutoa nafasi ya kuchunguzwa. Wanawake wawe macho na wanaume walaghai wanaoweza kuwaingiza katika tabia mbaya na kuwaharibia thamani zao. Kwa kauli yake Bi Madina Ali El-Buhriy, anasema kwamba, mwanaume kama huyo hafai kuwamo katika jamii, kwani nia yake ni kuangamiza jamii.

Red (1970), anasema, tangu enzi za zamani, wanawake wamekuwa mbioni katika mashindano ya kuwanasa wanaume. Katika kipindi cha ukoloni mwanamke alitengwa katika elimu, haki ya kumiliki ardhi, kupata ajira na kuwapo kwa vikwazo

vingi. Mwanamke ndani ya baadhi ya mifumo alitengwa kiuchumi. Baadhi ya wanawake walianza kujiingiza katika ukahaba kama sehemu ya suluhishi dhidi ya matatizo yao ya kiuchumi. Katika mwendelezo wa mfumo huo wa kimaisha, tatizo limekuwa kubwa zaidi. Wanandoa pia, wakajiunga kuwa ni wadau wakubwa katika suala la ngono nje ya ndoa. Kutokana na kuwapo kwa tatizo la ujinga wa elimu ya ndoa, ndoa nyingi za sasa zinavunjika kwa urahisi zaidi kuliko ilivyokuwa huko nyuma. Alofundwa aliitwa mrombo, hakufanana na asiyefundwa, ambaye aliitwa Msungu. Mapenzi si tamaa ya paja kwa paja, ni huruma ya kina ya kutatuliana matatizo makubwa ya kimaisha, k.v kuuguzana, kuzikana n.k.

Wanazuoni wa fasihi wamekuwa wakimsawiri mwanamke kama chombo cha starehe kwa wanaume, Kezilahabi (1974) anatuonesha mhusika Anastazia na mama Resi wanavyoasi ndoa zao kwa kufanya mapenzi na wanaume mitaani. Mohamed (1987) anatuonesha, jinsi mhusika Rehema anavyopitia katika maisha ya ukahaba katika kutatua matatizo yake. Matteru (1982) anataja picha tatu zinazobainika katika fasihi simulizi; mwanamke kama mzazi, chombo za anasa ya mwanaume na mwanamke kama chombo cha kumilikiwa.

Bi Madina Ali El-Buhriy (2013) anasema kisichofunga kipochi, kwangu hadhi haki pati. Taswira inayojitokeza sana katika fasihi ya Kiswahili ni ile inayobainisha unyonge wa mwanamke, ni vema suala la umalaya likapewa mtazamo mpya, lawama zisiishie kwa mwanamke tu, tufahamu kwamba umalaya ni tabia inayoendeshwa na watu wawili, mwanaume na mwanamke. Wasanii na wahakiki wengi wa kazi za fasihi, macho yao yanatazama upande mmoja wa shilingi kwa kuwalaumu wanawake peke yao, muda umefika sasa, kwa jicho la pili kuangalia upande wa pili wa shilingi,

lawama zielekezwe kwa wote, kwa wanawake na wanaume, wenye tabia hizo. Wanazuoni wajizatiti kuandika fasihi yenye kuunda upya taswira ya mwanamke, itakayoonesha kwamba, mwanamke si kiumbe pekee cha kustarehesha mwanaume tu, bali ni binadamu anayetakiwa kuendesha maisha yake pamoja na mwanaume. Baadhi ya waandishi wanaoonesha uhalisia huo ni Muhando (1982).

4.3.3 Dhamira ya Kuhamasisha Wanawake Katika Utunzi wa Mashairi

Mulokozi (1993) anabainisha kuwa, utunzi wa ushairi andishi katika kipindi cha urasimi (1600-1900) haukufanywa na wanaume tu, wanawake nao walikuwa na mchango mkubwa zaidi kuliko ilivyoielezwa na wachunguzi waliotutangulia. Baadhi ya mashairi ambayo watunzi wake hawafahamiki, hasa yale yenye kuielezea kwa usahihi hali ya unyonge wa mwanamke, yalitungwa na wanawake. Baadhi ya watunzi wanawake wanaokumbukwa ni Mwanakupona bint Msham (kama 1810-1860) Mwana Said Amin (karne ya 18/19), Mwana Shekhe Lemba (1663), Saada Taji li Arifina (karne ya 18).

Dondoo hilo hapo juu linathibitisha kwamba wanawake wa Uswahilini wana historia ya muda mrefu katika utunzi wa mashairi. Jambo linalotatanisha mpaka leo ni kukosekana kwa vitabu vingi vya Ushairi vilivyotungwa na kupewa ithibati kuwa ni vya wanamke, kinyume na vile tunavyoona kwa wanaume wengi, Muyaka (1940) Diwani ya Muyaka, Mnyampala (1965) Diwani ya Mnyampala, Abdilatif (1971) Utenzi wa Adamu na Hawa, Kandoro (1972) Mashairi ya Saadan, n.k.

Bi Madina Ali El-Buhriy, yamkini amefadhaishwa na hali inayoendelea mpaka sasa. Wanawake wengi wameshindwa kujitokeza katika utunzi wa mashairi. Katika

mazingira ya Tanzania ya leo, idadi kubwa ya Diwani za Ushairi zinahodhiwa na wanaume, ushahidi upo katika vitabu vya kiada vya Ushairi vinavyotumika katika mitalaa ya kielimu vimekusanya kazi zilizofanywa na wanaume, isipokuwa katika kitabu cha Taasisi ya Kiswahili Zanzibar malenga wapya (2001) kinachotumika katika elimu ya sekondari kimekusanya mashairi yaliyotungwa na wanawake wawili Faida Moh'd Bakar na Tatu M. Ali. Kutokana na kuwapo kwa mazingira yanayofanana na haya, msanii ameona haja ya kuwahamasisha wanawake wenzake wajitokeze katika sanaa hii, katika shairi la *washairi kina mama*, anasema; (uk 140)

Ushairi wetu sote, si pekee wanaume
Kwa hiyo tujikokote, ya moyoni tuyaseme
Hima na tushike kete, kwenye bao tuiname
KINA MAMA TUSIMAME, TUSANIFU USHAIRI

Huu ni mwaliko wa msanii Bi Madina Ali El-Buhriy, kwa wanawake wenzake, kufanya jitihada za kujitokeza katika utunzi wa mashairi. Anawataka watumie Ushairi kutolea hisia zao, matarajio yao, shida za kijamii na mielekeo juu ya maisha yao. Anawakumbusha wanawake kwamba sanaa ya Ushairi siyo ya wanaume peke yao. Katika kipindi chake cha utunzi wa Ushairi, msanii alitumia zaidi vyombo vya habari, kama njia ya kusambazia na kutunzia kazi zake. Kwa kutumia uzoefu huo, anawaondoa khofu wanawake wenzake;

Tuwe shime kutongoa, redioni wakasome
Na kama wasipotoa, haki yetu tulalame
Kinamama wa Kondoa, Morogoro tuyoyome
KINA MAMA TUSIMAME, TUSANIFU USHAIRI

Tangu kipindi cha ukoloni, baadhi ya kazi za fasihi, hasa mashairi na hadithi, zimekuwa zikitegemea magazeti na redio kama nyenzo muhimu katika usambazaji

na uhifadhi wa kazi hizo. Bi Madina Ali El-Buhriy, anawataka wanawake wenzake watumie fursa hiyo muhimu, kukuza sanaa ya Ushairi hapa nchini. Kazi za Ushairi siyo lazima zisambazwe kwa njia ya maandishi kama tuonavyo katika fani nyingine za fasihi andishi, shairi laweza kughaniwa redioni na ujumbe ukaifikia jamii au shairi linaweza kuchapishwa katika gazeti. Msisitizo umewekwa ili kazi ya utunzi wa Ushairi iwe yenye mvuto machoni na masikioni mwa hadhira, wahariri wahusishwe kulingana na taalumu zao.

Wakina mama tutunge, wahariri tuwatume
 Makarani watupange, na sisi tunemeneme
 Tusiyakhofu manguke, si vizuri tutuame
 KINAMAMA TUSIMAME, TUSANIFU USHAIRI

Bi Madina Ali El-Buhriy, anatoa tahadhari juu ya utunzi wa mashairi, kwamba siyo kazi ya kufanywa kiholela bali huongozwa na utaratibu maalumu unaotumika katika kila kazi za fasihi. Mashairi ni lazima yapite mikononi mwa wahariri kabla hayajachapishwa na kuifikia jamii lengwa. Wahariri hao ni lazima wawe wenye weledi wa taaluma ya Ushairi. Kazi yao kubwa, ni kusanifu lugha iliyotumika na kile kinachozungumzwa na malenga. Wahariri ni daraja, kati ya msanii na jamii. Kupitia kwao, tunapata ujuzi, maarifa na mielekeo sahihi ya kitaaluma na hatimaye, ni kupatikana kwa vingunge wa kitaifa na kimataifa. Hatua hii ikizingatiwa, tutaongeza idadi kubwa ya malenga wanawake hapa nchini.

Umoja ni silaha pekee ya kufikia katika hatua ya maendeleo. Wanawake wakikusanya tungo zao kwa pamoja na kuwa na kauli moja dhidi ya matatizo yanayowakabili, wanaweza kupata suluhishi za kudumu. Kwa kauli hiyo moja,

wataweza kupambana na maovu ya mila gandamizi dhidi yao. Wanawake kwa pamoja, kwa kufanya utafiti wa kina, wataweza kuvitumia vyeo tisa ndani ya familia zao na kupata fursa bora zaidi ya kufahamu, yepi hasa wayashughulikie ili kizazi cha wanaume kione thamani na umuhimu wa mwanamke katika maisha halisi ya jamii.

4.3.4 Dhamira ya Umuhimu wa Wazazi

Mzazi ni baba na mama wa mtu fulani. Hakuna mwanadamu mwenye akili timamu anayeweza kukanusha fadhira za wazazi. Ni ukweli uliowazi kwamba, wazazi wawili, baba na mama ndiwo sababu ya kuwapo kwa binadamu katika ulimwengu huu. Wazazi wana haki kubwa kwa watoto wao, kwani ni wao ndio waliowalea watoto wao. Wao ndio waliopata taabu na dhiki kwa ajili ya raha, na furaha ya watoto wao. Mama amembeba mwanawe tumboni mwake. Kisha, baada ya kujifungua kwa uchungu mkubwa hufuatia mzigo mzito wa ulezi na unyonyeshaji kwa muda usiopungua miaka miwili ya taabu, uchovu na shida.

Baba kwa upande wake huhangaika huku na kule kwa ajili ya kuhakikisha kuwa anapata kila kinachohitajika kwa ajili ya maisha ya mtoto. Ikiwa ni pamoja na mavazi, chakula, malazi elimu, mpaka mtoto anapokuwa mtu mzima mwenye uwezo wa kujifanyia mambo yake madogomadogo mwenyewe. Wazazi wa Kiafrika, hawaachi watoto wao katika upweke. Hata wakiufikia umri wa utu uzima, huendelea kuwa washauri wema, wenye busara na wenye kuwatakia mafanikio mema katika maisha ya familia zao. Wahenga waliibua methali isemayo; kulea mimba si kazi, kazi ni kulea mwana, hii ni kwa jamii za Kiafrika. Bi Madina Ali El-Buhriy, anashika kalamu na karatasi, kuiandikia jamii ya Waswahili na Waafrika wengine

juu ya falsafa hii ya maisha ya Kiafrika. Watoto, kuwasaidia wazazi wao ni wajibu wa lazima wa kila binadamu. Maisha ya utotoni yamo mikononi mwa wazazi, na hasa mwa kina mama. Sasa tunakumbushwa wajibu wa watoto kwa wazazi; katika shairi la *Yakupi Mashi* (maringo yetu yako wapi): (uk139)

Majani yanakambuka, yote yakiwazunguka
Yevu yakichegeleka, kwa khofu kutoiweka
Zimenyauka na nyika, ni nyembamba ja ndakaka
KWETU MWEVU NI MASOKA, NA SASA YAKUPI MASHI

Matawi yakikatika, kuni tunazirundika
Au jua likiwaka, vivuli vyenu mikeka
Imebaki kulimbika, yanapofika masika
KWETU MWEVU NI MASOKA, NA SASA YAKUPI MASHI

Ni wajibu wa watoto kuwatendea wema wazazi wao. Ni lazima wakiri kwamba, ni haki yao kutenda hivyo kama sehemu ya kutambua fadhila. Fadhira ya wazazi haiwezi kulinganishwa na malipo ya aina yoyote kutoka kwa mtoto. Wazazi watendewe wema kwa kauli moja, kwa kutumia mawazo, mali na kila kinachomilikiwa na mtoto, ambacho kimsingi ni mali ya wazazi. Ikumbukwe kuwa, mtoto wa leo ni mzazi wa kesho. Kwa muktadha huo, watoto watafikia hatua ya utu uzima, watahitaji msaada wa watoto wao hapo baadaye. Msaada uliojaa huruma na mapenzi ya kweli. Bi Madina Ali El-Buhriy anawataka wanajamii kuwaombea wazazi wao maisha marefu, kwa walio hai na mapumnziko mema kwa waliotangulia mbele za haki, kama anavyoonyesha katika mistari hii:

Mibuyu ilojinika, narudi kwako wa peka
Ipe palipo tindika, itunzwe na malaika
Mbadala twautaka, maombi ninayaweka
KWETU MWEVU NI MASOKA, NA SASA YAKUPI MASHI

Wakati msanii anaikumbusha jamii yake juu ya umuhimu wa kuwaombea wazazi ili wapate maisha marefu na ya kheri duniani, vyombo vya habari vinaripoti habari kuhusu madhila wanayopata wazazi kutoka kwa watoto wao. Mathalani, tumekuwa tukisikia wazazi kuuawa kwa shutuma za uchawi au ushirikina. Wengine huthubutu kuwabaka mama zao na kulala na baba zao. Watoto hawapaswi kufikia hatua ya kuwadharau wazazi kwa namna yoyote ile. Hao wazazi ndiwo waliowazaa na kuwalea kwa shida na raha mpaka hatua ya utu uzima. Wazazi wanapaswa kuenziwa, kuheshimiwa kwa kutendewa mema ya huruma. Katika uchunguzi huu, tumebaini kuwa, katika hali halisi ya jamii yetu, kuna watoto ambao hawawathamini wazazi wao, wanaweza kuwatukana, kuwapiga na hata kuwaua.

Katika hali ya kushangaza kuna watu wengi ambao huwasahau wazazi wao na kuwaacha wakiishi maisha ya shida Vijijini, wakikabiliwa na ukosefu wa mahitaji ya msingi k.v, chakula, matibabu, mavazi n.k. Kazi za Bi Madina Ali El-Buhriy, zinawakumbusha watu wenye tabia za kuwasahau wazazi wao, wabadili tabia zao. Kipato kinachopatikana, kitengwe, kiasi fulani cha fedha kwa ajili ya wazazi, na fedha zinapokosekana kwa ajili ya wazazi, ni vema watoto wakatenga muda wa kuwatembelea wazazi. Kwa kufanya hivyo wazazi watapata faraja na watoto, watapata radhi.

Kwa upande mwingine, wapo wazazi wengine, ambao hawatimizi wajibu wao. Hukwepa malezi ya watoto wao. Kwa kuwatelekeza. Baadhi yao ndiwo waitwao “watoto wa mitaani”. Jamii, hasa wazazi, watambue kwamba, malezi ya watoto yanahitaji ushirikiano wa wazazi wote wawili, washirikiane kwa pamoja, wala asiwepo hata mmoja wa kukwepa wajibu huo. Wazazi kwa nafasi yao, wanao wajibu

wa kuwahudumia watoto wao, nao watoto wanao wajibu kama huo kwa wazazi wao hapo baadae.

4.3.5 Dhamira ya Kutenda na Kutendewa Mema

Matendo mema ni tabia nzuri. Matendo mema, ni jambo muhimu sana katikamaisha ya jamii. Kila mtu, kwa nafasi yake, anatakiwa kutenda na kutendewa hivyo. Kila tendo au tukio la kibinadamu, lina tafsiri yake, ndani ya utamaduni wa jamii inayohusika. Wema au ubaya hupimwa hata katika mambo madogomadogo ya kijamii. Kutenda au kutendewa mema ni jambo lililogusa hisia za msanii, Bi Madina Ali El-Buhriy, katika shairi la *usimpe asotowa anasema*: (uk 141).

Kupeana ni kikowa, walitwambia mababu
Kama wapenda kupewa, na kutwaa kwa adabu
Shuruti nawe KUTOWA, utaiondosha tabu
USIMPE ASOTOWA, UKIMPA UMETUPA

Bi Madina Ali El-Buhriy, anaanza shairi lake kwa kusema Kupeana ni kikowa, walitwambia mababu. Hii ni kauli inayorejelea maisha ya jadi katika jamii za Kiafrika, maisha yaliyojaa huruma, ambayo ndiyo dalili ya upendo wa kweli. Katika maisha ya jadi Waafrika waliishi kwa kusaidiana na kutegemeana, katika nyanja zote za maisha; waliarikana, miongoni mwa majirani, katika shughuli za kilimo, ujenzi wa nyumba, misiba, magonjwa, kuvuna, waliombana chumvi, moto, chakula, kuni, mashamba, vinywaji hata mifugo n.k. Hakuna mtu aliyethubutu kukwepa mfumo wa maisha hayo. Kuwapo kwa mfumo wa maisha ya aina hiyo, suala la nipe, nikupe, lilikuwa na tafsiri sahihi kijamii. Mtu akipokea kitu leo, lazima naye kesho atoe. Wale wenye kupokea, wapokee kwa adabu na heshima. Kutokana na mtazamo wa

msanii anaona kwamba, kupokea kuna taratibu zake. Hatuna budi, kuzijua na kuzifuata, Bi Madina Ali El-Buhriy, anasema;

Japo upate baruwa, itokayo kwa muhibu
 Maneno ya kubeuwa, na makali kama shabu
 Kujibu ni maridhawa, kuutimiza wajibu
 USIMPE ASOTOWA, UKIMPA UMETUPA.

Wahenga wana methali isemayo “*tendawema, usingoje shukrani*”. Bi Madina Ali El-Buhriy, anatafautiana na methali hiyo. Aonavyo yeye ni kwamba, kupokea na kushukuru ni sawa na pande mbili za sarafu. Ukipokea, kushukuru ni wajibu. Mtu akipokea kitu cha mtu hana budi kumfanyia vivyo hivyo kwa njia na kitu kingine atakachokipata. Shukrani inayosisitizwa hapo ni kutenda jambo jema kwa mtu anayekujali.

Ukimpa anotowa, na ataweka hesabu
 Ya kwamba utafikiwa, naye atakujaribu
 Japo hedaya yakawa, fadhila kama adhabu
 USIMPE ASOTOWA, UKIMPA UMETUPA

Bi Madina Ali El-Buhriy anaiandikia jamii yake juu ya jambo hili baada ya kuona kwamba halizingatiwi ipasavyo. Kupuuzia kipengele cha kushukuru, ni kuwakatisha tamaa watoaji. Waswahili husema, neno “ahsante” tafsiri yake ni kuomba tena. Suala la umuhimu wa matendo mema, limezungumzwa na washairi wengi hapa nchini. Miongoni mwao ni nguli wa mashairi Shaaban Robert. Katika uhakiki uliofanywa na Gibbe (1980) shairi la *tendo*, anaeleza umuhimu wa matendo mema

Tendo bora ni mwangaza, ni ada jitahidini
 Jitahidini kuweza, matendo yenye thamani
 Mwili ukisha kuoza, na roho kuwa mbinguni
 Jina liwe laangaza, kwa sifa makumbushoni

Kwa shairi hili, msanii anafungamanisha maisha ya mwanadamu hapa duniani na maisha ya huko akhera. Kadri tunavyojifanyia mambo mema hapa duniani, ndivyo tunavyojijengea mazingira ya kupata maisha mema baada ya kifo. Gibbe (1980) anasema kuwa, kutokana na athari za Dini Shaaban Robert anaona kuwa duniani ni mahali pa kutenda mema ili baadaye tukapate fidia huko Mbinguni. Mtoaji hubarikiwa zaidi na Mwenyezi Mungu, moja kwa moja. Hivyo ndivyo, waamini wa Dini tafautitafauti, wanavyoamini. Kuwahudumia wenye ukata, vikongwe, yatima na wajane, Mwenyezi Mungu hutoa baraka maradufu. Jamii inahimizwa kuendelea kutendeanamambo mema yanayokubalika na binadamu. Sengo (2009) katika shairi la *Wanangu*, ametongoa ubeti unaohimiza hisia za matendo mema;

Wanangu shikeni umoja, ukweli uaminifu
Magumu sana yawaja, hesabu yake sufufu
Iko siku itakuja, mkutane na Yusufu
Wanangu

Utafiti huu, umegundua kwamba, katika jamii ya sasa, thamani ya neno “nashukuru” inazidi kupungua kimatumizi. Watu wanatendewa mema mengi, pengine na watu hata wasiowajua, lakini ni nadra sana kusikia neno “nashukru”. Msanii anaishauri jamii, kutenda mema zaidi ili tuweze kuishi katika hali ya upendo, amani na utulivu. Kwa upande wa pili, katika jamii zetu, wapo watu wenye uwezo wa kuwahudumia wengine kimaisha lakini hawafanyi hivyo. Suala la kutoa huduma ni la yeyote anayeweza kuisaidia jamii yake kwa kutoa sehemu ya kipato chake, kwa watu wengine. Kujitolea kwa hali na mali, ndiyo dawa kuu ya kukomesha ujambazi, uzururaji na pia kupunguza wimbi la watoto wa mitaani, wanaojitokeza kila kona, kila kukicha.

4.3.6 Dhamira ya Athari za Hulka za Binadamu

Hulka ni neno linalotolewa fasili na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2010), kuwa, ni mwenendo wa kuumbwa na kuzalika na mtu. Hulka ya binadamu haibadiliki. Mpoto (2010) anashadidiya kwamba, hulka ya binadamu ni kama damu, mwili na ngozi, vitu ambavyo, daima vimeungana kwa pamoja, kamwe havitenganishwi.

Hulka ya binadamu hujidhihirisha katika matendo mema na mabaya k.v, uongo, uvivu, ugomvi, upole, ukalimu, hekima, bahati, sudi, majivuno, ukatili n.k Bi Madina Ali El-Buhriy ametongoa beti kadhaa zinazofafanua juu ya falsafa hiyo muhimu kwa mwanadamu. Katika shairi la *hulka yako pera* (uk 128)

Waonekana kuiva, mtini ulivyo huko
 Uzuriwo kama nguva, ni vyako hivyo vituko
 Kumbe la juu ni kava, huko ndani mchemko
 KUWA NGUMU TUMBA ZAKO, NI HULKA YAKO PERA

Likiwa bichi ni hivyo, likiiva ni sumbuko
 Sifa yake ya mchovy, Napata kubwa kicheko
 Mambo yake hovyohovy, kamwe sitalipa heko
 KUTOIVA TUMBA ZAKE, NI HULKA YAKE PERA.

Katika ufafanuzi wa falsafa hii, msanii ametumia sitiari ya tumba za pera kuhusu hulka za binadamu. Kila binadamu amebeba tabia nyingi njema na mbaya ambazo amezioea na kuziona kama sehemu ya maisha yake ya kila siku. Tabia hizo, haziwezi kuathiriwa na mabadiliko yoyote yanayotokea katika jamii yake. Kama ni mtu mwema, ataendelea kuwa mwema bila kujali kama kuna watu wanaomkatisha tamaa, kumbeza, ama kumuhimiza. Kama ni mkatili, ataendeleza tabia hiyo bila

kujali athari zinazojitokeza. Msanii anafananisha hali hiyo na tumba za pera ambazo, daima huwa katika hali ya ugumu, bila kujali kama tunda limeiva au bichi, *kutoiva tumba zake, ni hulka yake pera*. Hata kama zingepikwa usiku na mchana na kuwekwa viungo vya kila aina, bado hali yake asilia, haipotei kamwe;

Lingekuwa la kupikwa, libandikwe kwenye jiko
Na viungo vingepakwa, vya kukaanga kwa miiko
Ai!! Hilo la kumakwa, linatupa tetemeko
KUTOIVA TUMBA ZAKE, NI HULKA YAKE PERA.

Ingawa msanii anaona kuwa tabia ya binadamu huongozwa na malezi, zipo tabia ambazo zinapaswa kurekebishwa kijamii, hasa zile zinazovunja taratibu na kanuni za nchi k.v, wizi, unyang'anyi, uongo, ukatili, ujambazi n.k. Matendo ya aina hii, hayapaswi kuendekezwa kwa kisingizio kwamba msingi wake ni hulka ya kibinadamu. Zipo hulka, ambazo zinastahiki kuigwa na kuendelezwa miongoni mwa wanajamii; hasa; upole, utii, heshima, ukarimu, uadilifu. Wajibu wa kila mtu ni kutumia vizuri falsafa ya hulka, ikitumika vibaya, jamii inaweza kusumbuka.

4.3.7 Dhamira ya Utengano wa Wanandugu

Katika mazingira ya kawaida, ni jambo jepesi sana kupata ndugu. Mara tu mtu anapozaliwa, tayari ndugu zake ni wale anaozawa nao; k.v kaka na dada zake, udugu huu, huitwa udugu wa damu. Katika udugu huu, binadamu hana uchaguzi, kwamba, watu hawa ni wema ashirikiane nao au ni waovu, ajiepushe nao, bali hujikuta analazimika kushirikiana nao katika shida na raha. Kuna kundi jingine la udugu. Hili huanza na hatua ya urafiki katika kazi, sehemu za kuabudu, misibani, sokoni, shuleni, hospitalini n.k. Kutokana na ushirikiano huo, watu hujikuta wamejenga uhusiano mkubwa tena wa karibu, unaowawezesha kuishi kama ndugu wa damu

moja. Udugu huu, ni udugu wa hiari. Lengo kubwa la binadamu, katika kujenga na kudumisha udugu, ni kutafuta faraja, kuliwazana, kuhudumiana, kusaidiana katika shida na raha zote hapa duiani.

Bi Madina Ali El-Buhriy anaitazama falsafa hii ya mwanadamu kwa jicho pevu. Katika tafakuri yake, anaona kwamba, pesa na mwanamke ni kikwazo katika kudumisha na kuendeleza udugu miongoni mwa binadamu. Pesa zina nafasi yake ya kuvunja udugu. Baadhi ya wanandugu, hukopeshana pesa, lakini mambo, yanaweza kwenda kinyume, hudhulumiana na hili husababisha kukorofishana na kutoelewana wengine hufikia hatua ya kupigana na kuvunja udugu. Katika kipengele hiki cha pesa, msanii alitunga shairi la *mke na pesa* akisema; (uk 151).

Pesa waweza azima, shida ya nduguyo pita

Ni masiku chungu nzima, ikiwa wamfuata

Utabaki kulalama, hayawani utamwita

KATI YA MKE NA PESA, PESA HUVUNJA UDUGU

Imebanika kwamba, binadamu hawezi kuvumilia kimya cha kutolipwa anachokidai na kutoa msamaha kwa mdeni wake aliyeshindwa kulipa. Ni jambo gumu kwa mwanaume kutoa msamaha kwa mwanaume mwenzake, anayemtuhumu kumkosea adabu. Rais wa Afrika ya Kusini Mandela (1918 - 2013) alionesha uungwana mkubwa na kupewa tuzo ya Nobel mwaka 1993 kwa kuwasamehe Makaburu waliomtesa pamoja na waafrika wenzake waliobaguliwa katika nyanja zote za maisha. Pamoja na umaarufu huo mkubwa, alishindwa kuendeleza udugu na mwanaume aliyemtuhumu kutembea na mke wake Winnie Mandela. Hatima ya hayo ilikuwa ni kutoa talaka kwa mke wake tarehe 19 Machi 1996. Uhusiano kati ya

Mandela na mkewe pamoja na mlinzi wake ulisambaratika (http://sw.wikipedia.org/wiki/Winnie_Mandela)

Bi Madina Ali El-Buhriy aliendelea kuihakiki jamii, akabaini kwamba, mwanamke ana nafasi nyingine anayoitumia kuharibu udugu kati ya mwanaume na ndugu zake wengine.

Mkeo akisha sema, wifi yangu Zamlata
 Nyumba hii angehama, kutwa kucha tunabwata
 Bila hata kuinama, utamtoa mputa
KATI YA MKE NA PESA, MKE HUVUNJA UDUGU.

Baadhi ya fitina za kijamii, kati ya mtu na ndugu yake, chanzo kimojawapo ni ndugu wa mume wa kike na mke wa kaka au mama mkwe , ndivyo ilivyo. Katika jamii za kiafrika, mwanaume, akishaoa, huanza maisha mapya ya mke na mume. Anapaswa asikilize maamuzi ya familia ya wazazi wake na maamuzi ya mke wake.

Mke hujenga fikra kwamba, mume anapaswa kumtimizia mahitaji yote. Familia ya mwanamume inaona kwamba wao wanastahiki kuhudumiwa zaidi na watoto wao, kuliko mke. Wao ndiwo waliomzaa na kumlea kijana wao. Mwanaume na mwanamke kwa pamoja, hujikuta wakikabiliwa na mtihani mgumu. Katika ubeti huo hapo juu, msanii anaeleza kwamba baadhi ya wanawake hudhani kwamba, hawastahiki kuishi na ndugu wa mwanaume. Baadhi hufanya kila njia, kumshawishi mume wake, kuwafukuza ndugu zake.

Katika uchunguzi uliyofanywa na mtafiti tumegundua kwamba, mwanamke alianza kunyooshewa vidole juu ya kukosanisha ndugu tangu katika fasihi na masimulizi ya

Kibiblia. Mekacha (1993) anasema kuwa, usawiri wa mwanamke unanasibishwa na wasifu wa Hawa (Eva) wa kumdanganya Adamu, kula tunda alilokatazwa na Mwenyezi Mungu, matokeo yake ni kuharibika kwa uhusiano kati ya Mwanadamu na Mwenyezi Mungu. Katika fasihi simulizi, mwanamke anaendelea kusawiriwa kwa mtazamo huo huo wa kiharifu. Hadithi simulizi zinamchora mwanamke, namna anavyowatesa watoto wa kambo na yatima, kwa kuwanyima chakula, malazi na mavazi kutokana na wivu. Jee, ni mara ngapi, tumeshuhudia ndoa zikisambaratishwa na mawifi?

Chanzo cha tatizo la uovu wa mwanamke kinafaa kiendelezwe katika mijadala ya wanazuoni. Ingefaa wanazuoni waweke bayana, sababu za kazi nyingi za fasihi zinamhusisha mwanamke na matendo maovu. Fitina na mizozo kati ya wake na mawifi, wake na mashemeji, wake na wakwe zake, zipo nyingi. Lengo ni kuvunja udugu wa watu au? Mke anapowachonganisha ndugu, yeye hufaidika na nini? Na je ndugu wa mume wanapotaka kuharibu mahusiano ya mume na mke (mawifi, mashemeji na mama wakwe) hufaidika na nini? Jee inakuwaje, mwanaume akubali kujenga fitina na ndugu zake au mke wake kutokana na shinikizo la mke au ndugu zake. Hapa tunapaswa kujifunza kwamba, wanaume wanatakiwa kuwa makini zaidi katika maamuzi wanayoyafanya dhidi ya hoja zinazoletwa na wake zao na ndugu zao wa kiumeni.

Wake, wasishangalie kwamba, wao ni washindi katika kuvunja udugu, kati ya waume na ndugu zao wengine, vivyo hivyo, ndugu wa upande mume wasione fahari kuharibu udugu uliojengwa kati ya mume na mke kwa ndoa Takatifu. Waafrika, ni jadi yetu, kuishi ki-ujamaa. Katika tafsiri ya Kiafrika, nyumba inayokosa wageni,

haiwezi kupata Baraka. Maisha ya mtu, kuishi na familia yake tu, ni utamaduni wa nchi za Kimagharibi, ambao tafsiri yake, ni uchoyo, ulafi, ubahili. Ingefaa tuwaachie, hayo yao. Iwe kwa mume au mke.

4.3.8 Dhamira ya Kumbukizi

Kuzawa na kufa ni pande mbili muhimu zinazokamilisha sifa mbili za mja. Kuzaliwa ni mwanzo na kifo ni mwisho wa uhai wa maisha. Kila jambo ni tukio muhimu la kijamii na kihistoria. Mtoto anapozawa, huleta furaha katika jamii, hukua na baadaye kuwa mtu mzima. Katika kipindi hicho hupata nafasi ya kutenda mema na mabaya. Wanadamu wote wanajua kuwapo kwa kifo, lakini wengi wao huogopa kufikwa na kifo. Baadhi wana mawazo ya mali walizolimbikiza, wanakuwa na wasiwasi kuhusu watoto wao na ndugu watakaorithi.

Baada ya kifo, binadamu huendelea kukumbukwa na jamii yake kwa matendo aliyoyafanya katika kipindi cha uhai wake. Katika kumbukumbu za kihistoria, yapo majina ya Madikteta wa dunia ambao wameua idadi kubwa ya raia wasiokuwa na hatia. Miongoni mwa watu hao ni Hitler wa Ujerumani na Musolin wa Italy, Bukasa, Mabutu Ngwema, wa Afrika ya kati, Napoleon, Kaizar, Alekizander. Watu hao wanakumbukwa kwa mabaya yao nyakati za utawala wao. Kundi jingine ambalo limeandikwa sana katika kumbukumbu za kidunia ni la watu waliotoa mchango wao muhimu k.v kupigania haki na uhuru, kusimamia maamuzi yao, kuibua falsafa sahihi juu ya maisha ya watu. Baadhi yao, ni; Mandela wa Afrika ya Kusini, Lumumba wa Kongo, Gandhi wa India, Martin Luther King wa Amerika Nyeusi, Nkwame Nkuruma wa Ghana, Galileo wa Ulimwengu wa magunduzi mapya Ulaya n.w.

Bi Madina Ali El-Buhriy, amelipa uzito jambo hili kwa kufanya kumbukizi kwa baadhi ya wakumbukwa ambao aliridhishwa na matendo yao mema. Ametunga shairi la Enzi zao. Salim Ali Kibao. Katika shairi la *Salim Ali Kibao*: (uk 144)

Ninawajuza mahiri, huzuni imenisibu
 Kuondokwa na Jabbari, kwangu alo mahabubu
 Yule wangu askari, ameitwa na Wahabu
 ANDANENGA NAKUJUZA, KIBAO SINACHO TENA

 Kwangu kilikuwa zari, Kibao cha Kiarabu
 Kuondokewa Jabbari, kwangu alo mahabubu
 Kimekatika umuri, ni hoi sina jawabu
 MAYOKA NINAKUJUZA, SINACHO TENA KIBAO

Msanii anaonesha masikitiko yake ya kuondokewa na kaka yake ambaye alikuwa ndiye mlezi wake, anatumia sitiari ya *askari na kibao cha kiarabu*, kama njia ya kuonesha jinsi mkumbukwa alivyokuwa makini katika kutekeleza wajibu wake katika familia. Anamkumbuka kwa tabia yake ya ukarimu, upole, ucheshi na malezi aliyopewa, analalamika namna atakavyo kabiliana na maisha ya upweke, *nahisi yangu jeuri, imegota kwa bawabu*.

Aidha, Salim Ali Kibao, mbali ya kuacha pengo katika familia yake pia ameacha pengo katika sanaa ya Ushairi. Alikuwa ni mtunzi wa mashairi. Ndiye aliyetunga Utenzi wa Uhuru wa Kenya. Jambo hili ndilo lililompa msukumo, Bi Madina Ali El-Buhriy, kuwajulisha wapenzi wa fani ya Ushairi, akiwataja kwa majina, Mayoka, Sengo na Andanenga. Si miaka mingi kupita Jumanne Mayoka, naye akaifariki dunia. Anaendelea kutoa ya moyoni kwa wakumbukwa wengine waliotia faraja katika maisha yake.

Nakukumbuka Rehema, vipindi kwako si ndwele

Taarifa ukisoma, inatua hadi Hale

Utadhani nyoka moma, wafoka pasi simile

BINTI WA MWAKANGALE, AMEFARIKI REHEMA

Rehema Mwakangale alikuwa miongoni mwa wanahabari wanaochipukia na kujipatia umaarufu mkubwa. Umaarufu wake ulitokana na ufanisi alioonesha katika kazi. Mtazamo wa Bi Madina Ali El-Buhriy katika utendaji kazi unaungwa mkono na makundi mbalimbali ya kijamii ambayo yalifanya kazi kwa karibu zaidi na mkumbukwa. Taasisi za kijamii zilikuwa zinamkumbuka Rehema, kwa jinsi alivyokuwa akijituma katika kampeni za kupambana na vitendo vya kikatili dhidi ya wanawake. Rehema Mwakangale, alikuwa anajituma kikamilifu, kuandika habari za mapambano dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali za umma, mambo ambayo yanakwamisha maendeleo ya wananchi walio wengi. Akitoa salamu za serikali wakati wa mazishi Spika Sitta aliwataka waandishi wa habari nchini, kumuenzi marehemu kwa kufanyakazi kwa bidii. Inspekta Jenerali wa Polisi, IGP, Said Mwema, alisema jeshi lake limeshtushwa na kifo cha Rehema kwa kuwa alikuwa mdau muhimu hasa kwenye suala la kutoa elimu kwa umma kuhusu polisi jamii na ulinzi shirikishi. Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile, alisema kituo chake kimempoteza mchapakazi mahiri. Alisema wakati wote Rehema alipokuwa kazini alikuwa mtulivu na mtu ambaye hakuweza kutetereka kiurahisi. Kutokana na maelezo ya wahusika wengi wa serikali ni wazi kwamba Rehema alikuwa ni mtendaji mzuri katika kila shughuli iliyomkabili mbele yake.

Bi Madina Ali El-Buhriy hakusita kuwakumbuka wasanii wa Ushairi waliofungua mlango katika tasnia hii. Anawakumbuka, kutokana na kazi zao nzuri, ambazo, leo

hii tunazitumia kama marejeleo muhimu katika ushairi. Katika shairi la *enzi zao*, Bi Madina Ali El-Buhriy, anasema: (uk 133)

Enzi za SHAABAN ROBERTI, ni enzi zao wasusi
 Si enzi za hatihati, ela zimepita basi
 Zimepita na wakati, tumebaki kudurusi
 ZILE ENZI ZA MALENGA, WALIOJUA WAFANYACHO

 Zama za bwana KANDORO, na MBARUKU kasisi
 MWINYIHATIBU, ZAHORO, MDANZI na MATHIASI
 Walizitunga nyororo, tene safi kama rasi
 ZILE ENZI ZA MALENGA

Katika shairi la Enzi zao Bi Madina Ali El-Buhriy, amewakumbuka wasanii washairi wa miaka ya Hamsini, Sitini na sabini wa Ushairi, miongoni mwao, ni Shaaban Robert, Saadan Kandoro na Mathias Mnyampala, washairi ambao, wametuachia misingi imara ya utunzi wa mashairi ya Arudhi ya Kiswahili. Ndiyo maana Bi Madina Ali El-Buhriy, anakiri kwamba washairi wa leo, kazi yao ni kudurusu katika kazi za watangulizi wetu. Sengo (1987) anashadidiya kuwa, Shaaban Robert kuitwa mahashumu, ni kwa ufundi wake wa kutunga maandishi ya kudumu. Kwa hekima, yeye ni Sultani yaani bingwa. Kaifunza dunia, ya uandishi na usomi. Kwa uzito wa kazi zake, uzuri wa lugha na fani yake, wasomi wengi wanamwona Shaaban Robert, yu pamoja nao katika darasa zao. Mwenyezi Mungu Amrehemu pakubwa.

Katika utafiti huu tumegundua kwamba, binadamu hukumbukwa kutokana na mchango wake katika jamii. Kila mwenye kuitumikia vyema jamii yake, kamwe hasahauriki. Baada ya kifo chake, watu, hutafuta njia za kumuweka katika kumbukumbu za kijamii ili kuenzi matendo yake. Watumishi wa ngazi za juu

Serikalini majina yao hutunukiwa barabara, viwanja vya michezo. Hapa nchini tuna barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Mwalimu Nyerere, Rashid Kawawa, Edward Sokoine, Bibi Titi Mohamed, Nelson Mandela, Sam Nujoma n.k., ingawa baadhi yao wametunukiwa hayo bila ya kutazama mapisi halisi ya sehemu hizo, Waafrika walikuwa na utamaduni wa kufanya kumbukizi kwa kuendeleza majina ya wakumbukwa wao. Kulikuwa na utamaduni wa kumbukizi za watoto, kupewa majina ya babu zao waliofariki kama sehemu ya kuenzi matendo yao mema na kuendeleza mapisi ya kizazi k.m Tigiti Sengo aliyerithishwa jina la baba wa mama yake; Jakaya na Mrisho, aliyerithishwa majina ya mababu zake, mzaa mamake na mzaa babake, Khalfani Mrisho Kikwete.

4.3.9 Dhamira ya Matatizo ya Maji Katika Jiji la Dar es Salaam

Maji ni rasilimali muhimu kwa maisha ya viumbe vyote ulimwenguni. Katika Jiji la Dar Es Salaam, eneo linalopata maji, linahudumiwa na Kampuni ya DAWASCO (Dar es salaam Water Supply and Sewerage Company), ambayo imepewa mkataba na Mamlaka ya Maji Safi na Maji machafu Dar es Salaam, DAWASA (Dar es Salaam Water Supply and Sewerage Authority).

Maeneo yasiyo na mtandao wa DAWASA hupata maji kutoka kwenye visima vinavyoendeshwa na taasisi na watu binafsi. Aidha, vipo visima virefu 1,100 na vifupi 238 vilivyomo katika Mkoa wa Dar es Salaam, baadhi ya hivyo ni vya maji yanayojichuja kutoka mashimo ya vyoo. Maji mengine husukumwa na mitambo ya Ruvu Juu na Chini, kwa pamoja, huzalisha lita milioni 353 kwa siku. Kiasi hicho hutosheleza asilimia 75 tu ya mahitaji ya lita milioni 469.3 ya maji kwa siku. Chanzo cha data (<http://www.dsm.go.tz/kurasa/maji/index.php>).

Ni miaka hamsini na nne sasa, tangu Tanganyika ijipatie uhuru wake 09/12/1961 kutoka kwa wakoloni, kwa lengo la kujiendeshea maisha yetu wenyewe. Katika kipindi chote hicho, bado suala la upatikanaji wa maji safi na salama, limekuwa likisuasua, katika maeneo ya mijini na vijijini. Limekuwa ni tatizo sugu, siyo jambo la ajabu kuona misururu ya ndoo kwenye mabomba au watu na mikokoteni yao, wakielekea katika visima (Vioski) ndani ya Jiji la Dar es Salaam ambavyo maji yake si salama.

Nyumba nyingi zina mabomba yanayojulikana kama mradi wa Wachina, yapo kama mapambo ndani ya nyumba, usiku kucha na mchana kutwa, maji hayapatikani inavyostahili. Wahanga wakubwa wa janga hili ni wanawake ambao wana wajibu wa kuhakikisha kuwa familia zao zinapata maji ya kuoga, kunywa, kufulia na kupikia. Wanawake hujikuta wanatumia muda wao mwingi, kuhangaikia maji, badala ya kujumuika katika shughuli nyingine za kimaendeleo.

Bi Madina Ali El-Buhriy, amekerwa na hali hii inayowakumba Watanzania wengi, anawatumia watani zake WAZARAMU wa Jiji la Dar es Salaam kama kiwakilishi cha maeneo ya taifa la Tanzania. Ambayo yanakabiliwa na tatizo kubwa la upatikanaji wa huduma za maji. (uk 135)

Mwachekesha WAZARAMU, mjidaivyo na JIJI
Matao na mingurumo, mmeifunga mikwiji
Maneno mengi misemo, mwabwabwaja kama uji
HILO JIJI BILA MAJI, MTANGA NATOA ZOMO

Ukuaji wa jiji la Dar Es Salaam, ni jambo linaloongeza uzito juu ya tatizo la maji. Kwa sasa kuna idadi kubwa ya wageni wa kuhamia kuliko ya wale wanaohama. Dar

Es Salaam ni jiji linalokua kwa kasi, ni jiji la tatu kwa ongezeko kubwa la watu Barani Afrika, na ni Jiji la tisa duniani. Kuwepo na joto kali, katika majira yote ya mwaka ni hali inayoongeza kasi ya mahitaji ya raslimali ya maji kwa ajili ya usafi wa miili na mavazi. Mpaka sasa, hakuna uwiano mzuri wa usambazaji wa maji katika maeneo yote. Maji ya uhakika, hupatikana zaidi, katikati ya Jiji, hasa Oysterbay. Maeneo mengine yaliyosalia ambayo ndiyo yenye idadi kubwa ya watu, upatikanaji wa maji ni wa kubahatisha tu.

Hali ni mbaya zaidi katika mitaa wanayoishi watu wenye kipato cha chini, ambao wanashindwa kumudu ghalama za kuingiza maji ya bomba katika nyumba zao. Na ni kundi hilo ambalo linashindwa hata kumudu gharama za kununua maji ya kwenye visima, kwa bei kati ya shilingi mia tatu hadi mia tano kwa lita ishirini. Matokeo yake ni kwamba, watu hao hulazimika kuishi, kwa kutumia maji ya miferejini kwa matumizi ya kila siku. Profesa Sengo anayeishi Manzese tawi la mnazi mmoja, Kata ya Manzese ni shahidi mzuri wa dhuluma hiyo, wanayofanyiwa wazawa- wananchi wa Tanzania.

Utafiti umegundua kwamba, tatizo la maji halipo katika Jiji la Dar Es Salaam peke yake, bali ni tatizo la Watanzania wote. Kuna mikoa, ambayo, kwa asili ni mikame, Dodoma, Singida, Shinyanga, Tabora, Simiyu na Geita. Pengine mpango wa kuchukua maji kutoka ziwa Victoria na kusambazwa katika mikoa ya kanda ya kati ungepewa msukumo zaidi, badala ya kuishia Shinyanga, yaangaliwe na maeneo mengine. Yapo majiji mengine manne Mwanza, Mbeya, Tanga na Arusha, Serikali inapaswa kuchukua hadhari mapema, kabla hali haijawa mbaya kama ilivyo katika Jiji la Dar es Salaam.

Majumba yalo na kimo, makubwa yalo na taji
 Tena kila kitu kimo, mwalitambia wenyeji
 Maji kutokuwa humo, dosari ya hilo JIJI
 MTANGA NATOA ZOMO, DAR JIJI BILA MAJI

Msukumo mkubwa juu ya tatizo la maji unaelekezwa zaidi katika Jiji la Dar Es Salaam kwa sababu ndiyo uso na kielezeo cha taifa la Tanzania. Haipendezi hata kidogo, kwa wageni wanaofika Tanzania, na kukuta wakaazi wa Jiji la Dar es Salaam wakihangaika na ndoo mitaani kusaka maji, huku watendaji wa Serikali wakiwa wamejifungia maofisini na kuziba masikio kushughulikia shida za wananchi wao.

4.3.10 Dhamira ya Rushwa

Rushwa, ni dhanna pana, ambayo haiwezi kutoshelezwa na fasili moja. Watu wameifasili rushwa kwa mitazamo tafautitafauti. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (1981), wanasema kwamba, rushwa ni fedha au kitu chochote aghalabu chenye thamani, kinachotolewa na kupewa mtu mwenye madaraka ya jambo fulani, ili aweze kutoa upendeleo wa haki au kitu, kwa mtu asiyestahiki. Lengo la rushwa ni kupindisha sheria, kanuni na taratibu za nchi kwa manufaa ya mtu binafsi. Hivyo rushwa ni njia za utekelezaji wa dhuluma katika jamii. Ni dhuluma kwa mtoaji na mpokeaji.

Tanzania inakabiliwa na tatizo la rushwa katika ngazi karibu zote, Vijijini hadi Taifani. Tatizo hilo, lipo tangu kipindi cha utawala wa kikoloni na baada ya uhuru, na kutangazwa kwa Azimio la Arusha, ambalo, watu wengi, waliweka matumaini kwamba, lingeondoa dhuluma hiyo. Rushwa imekuwa ikipewa majina tafautitafauti;

chai, mchicha, mrungura, kitu kidogo, mikono kunjufu n.k. Kutokana na ukubwa wa tatizo, Serikali ya Jamhuri ya muungano wa Tanzania iliunda chombo maalumu TAKUKURU mwaka 1975 chenye mamlaka ya kisheria, kushughulikia tatizo la rushwa. Pamoja na kuwapo kwa chombo hicho, bado tatizo la rushwa ni kubwa, linazidi kuongezeka.

Pamoja na kuwepo kwa mikakati mizuri ya Serikali, lakini wapo baadhi ya viongozi wachache wenye fikra za kujilimbikizia mali na uchu wa madaraka. Hao hawapo tayari kuunga mkono sera hiyo. Baadhi ya mikakati ya Serikali katika kukabiliana na tatizo hilo ni kujenga mikakati ya ushirikiano na TAKUKURU, kutolewa Semina elekezi kwa viongozi na kuwapo kwa Kamati inayoshughulikia maadili ya viongozi na watumishi wa umma. Mikakati hiyo ilifasiliwa kuwa, ni njia ya kuleta haki sawa kwa raia wa taifa la Tanzania. Watanzania walianza kuweka matumaini ya mgao sawa wa pato la taifa linalotokana na raslimali za madini, mito, misitu, bahari, ardhi, viwanda, kwa manufaa ya wote.

Kutokana na kuwapo kwa rushwa, viongozi wetu wanajinufaisha kwa kutumia nyadhifa zao. Kuna ukiukwaji wa kusaini mikataba na wawekezaji bila kufuata taratibu za kisheria. Baadhi ya wenye uwezo, wanajimilikisha ardhi kubwa, ambazo hawaziendelezi. Kuna ajira za upendeleo. Bi Madina Ali El-Buhriy anawataka viongozi wabadilike tabia, mtu anayeoga, hutarajiwa kuondoa uchafu mwilini, viongozi wanapopewa semina za maadili wanategemewa kufanyakazi kwa uadilifu. Viongozi wazingatie maadili yao ya kazi. Katika shairi la *kwekoga*;

Chooni kunakawia, tukadhania wakoga
Twevu twakutarajia, ni mja usiyezuga

Kumbe kunajimwagia, mwili kunauvuruga
NAKUAPIA KWEKOGE, BALI KUNAJIMWAGIA

Serikali ya Tanzania inayongozwa na Chama cha Mapinduzi, Wanachama wake, ndiwo wenye kushika dola ya nchi hii. Rais na Baraza lote la Mawaziri ni wafuasi wa Chama hicho. Katika Katiba ya chama hicho, kuna ahadi za mwanachama, ahadi namba nne inasema; "Rushwa ni adui wa Haki, Sitapokea wala kutoa rushwa." Kauli hiyo, bado haijapewa uzito unaostahiki, ili kila kiongozi awe mstari wa mbele kupinga matumizi ya rushwa. Ofisi nyingi nchini zinalalamikiwa kutengeneza mazingira ya kupokea rushwa kutoka kwa wananchi wanaostahiki kupewa huduma bure. Katika mazingira ya aina hiyo, watu wenye tatizo la ukata wanakosa huduma ambazo ni haki yao kisheria. Wananchi wazawa, wenye serikali yao, ndiwo watowao kodi, ndiwo wavujao jasho, kuiendeleza nchi yao. Badala yake hubezwa na kuminywa haki zao Shuleni, Hospitalini, mahakamani, barabarani hadi usingizini. Hakika, rushwa ni dhuluma ya wazi kwa wanyonge. Bi Madina Ali El-Buhriy, anaendelea kuwashangaa wapokea rushwa;

Utelezi wa bamia, bado umekuviriga
Kipi kilokuzuia, usisugue mabega
Mnene unaemwia, atakae kusunduga
WAONEKANA KWEKOGE, BALI KUNAJIMWAGIA

Sabuni kweitumia, wabananga wakoroga
Ni baridi wakhofia, au wakimbilia sogu?
Tufahamishe Jamia, ufunzwe upate iga
UNAONESHA KWEKOGE, BALI KUNAJIMWAGIA

Serikali ya Tanzania huongozwa na mihimili mitatu; uongozi wa juu wa Serikali huongozwa na Rais, Mahakama huongozwa na Jaji Mkuu na Bunge huongozwa na

Spika. Watanzania wote ndiwo serikali ya kudumu, waajiri wa hao wote wengine, pamoja na utumishi wote wa Umma. Wazawa, Wananchi na raia wan chi yetu, ndiwo wategemewao kutekeleza maamuzi yanayotolewa na vyombo hivyo vya dola. Matumaini ya Watanzania, kujipatia maisha bora, kunategemea Sera madhubuti zinazotungwa na kusimamiwa na mihimili hiyo. Wananchi wangependa kuona, uongozi wa Serikali yao, ukiwajibika kikamilifu zaidi kwa kuwachukulia hatua zinazostahiki wahalifu wote kama tulivyoona, katika tuhuma za “EPA”, “RICHMOND” NA “KIGODA”. Jitihada hizo zisiishie tu hapo. Wizara na idara zote Serikalini, ziendee kumulikwa, mafisidi wakubwa kwa wadogo, wawekwe hadharani na kuwajibishwa. Zipo tuhuma Serikalini kuwa, wanyama wanauzwa na kusafirishwa, dawa za kulevya zinauzwa kiholela, upendeleo wa vyeo, matumizi mabaya ya madaraka. Matukio kama haya yanapofumbiwa macho, yanasababisha wananchi kukosa imani kwa viongozi wao.

Utafiti huu, umebaini baadhi ya sababu za kuwapo kwa tatizo la rushwa katika jamii. Kwanza, ni mmomonyoko wa maadili miongoni mwa viongozi na watumishi wa umma ambao wamehalalisha, kudai na kupokea rushwa kutoka kwa watu, wanaowahudumia. Pili, ni elimu ndogo kwa wananchi juu ya haki na wajibu wao wa kupata huduma. Baaadhi ya raia, wanadhani kwamba hakuna huduma wanayoweza kuipata bure bila kutoa rushwa kwa watumishi.

Hivyo, wapo raia, ambao hutoa rushwa, hata kama hawajadaiwa na watumishi. Tatu, ni ubinafsi na tabia ya uroho wa kujilimbikizia mali au utajiri. Wapo watumishi ambao hawaridhiki na mishahara yao, wanaona, rushwa ni sehemu ya kujiongezea kipato ili kumiliki mali nyingi zaidi. Nne, watu, hutumia njia ya mkato kukamilisha

na kutatua matatizo yao. Baadhi ya watu hawapendi kufuata taratibu za kazi, ambazo mara nyingi, huwa na mlolongo mrefu.

Ili kukwepa ucheleweshwaji wa huhudumiwa, watu wengi huwashawishi watumishi kutoa fedha, ili waharakishiwe kupata huduma. Mwisho, ni udogo wa viwango vya mishahara, baadhi ya idara za Serikali na Sekta binafsi, zinalipa mishahara midogo kwa waajiriwa, fedha ambazo haziendani na hali halisi ya maisha, watumishi wao hulazimika kujiingiza katika rushwa kama njia ya kujiongezea kipato. Watafiti kwa nafasi na nyadhifa zao, ni jeshi maalumu la kitaaluma, la kuyatafiti mambo mithili ya haya na kuyatongoa hadharani, vyombo stahiki, viyashughulikie, kwa manufaa ya nchi na Taifa.

Dawa ya rushwa sio kulaumiana au kunyoosheana vidole, au, wengine kujiona watakatifu, kuwa rushwa haiwaathiri. Katika mapambano ya rushwa, tunapaswa kushughulika zaidi na saikolojia za watu kuliko kutoa adhabu. Jamii ijengewe uwezo wa kiutambuzi na weledi wa kiakili na kitabia. Dini ya kweli irejeshwe madarasani kote na Mwenyezi Mungu Asitukanwe wala, Asikufuriwe. Watu waelimishwe jinsi rushwa inavyoleta madhara. Ni tendo, ambalo, hata wao wapokeaji, wakitendewa, hawawezi kuyafurahia. Watanzania, tukatae rushwa kwa vitendo. Tuungane pamoja, kwa sauti moja, kubadilisha nyendo na tabia za viongozi na zetu, ili sote, tunufaike na raslimali zetu kwa haki na usawa. Tukiliacha tatizo hili liendeleo kukita mizizi, hakuna atakayesalimika. Mabadiliko ya kijamii huanzia kwa mtu mmoja mmoja. Kila raia, achukue hatua za dhati, kupinga vitendo vya rushwa. Kwa upana wake rushwa inahujumu uchumi wa Taifa. Rushwa huongeza idadi ya watendaji wabovu Serikalini hivyo, hupunguza uwezo wa Serikali katika kutoa huduma zinazostahiki

kwa wananchi wake. Rushwa huchochea makosa ya jinai, huvunja amani na utulivu. “Rushwa hupofusha macho tusipoangalia tutatumbukia shimoni wote”.

4.3.11 Dhamira ya Athari za Mabomu ya Mbagala

Bomu la nyuklia ni silaha inayosababisha mlipuko mkubwa wa ghafla. Kati ya silaha zote, ni silaha yenye nguvu na ya hatari zaidi. Kani ya mlipuko huo hutokana na; mmenyuko mfululizo wa kinyuklia ambao ni kupasuliwa kwa kiini cha atomi, kuwa elementi mbili au mmenyetuko nyuklia, kuungana kwa viini vya Atomi viwili, kuwa elementi nzito zaidi.

Mabomu ya Atomia, hutengenezwa kwa kutumia Urani au Plutoni. Bomu moja la nyuklia, linatosha kuharibu mji mkubwa kama ilivyotokea mwaka 1945, huko Hiroshima na Nagasaki. Mabomu ya 1945 yalikuwa madogo sana tafauti na mabomu yaliyotengenezwa baada ya hayo. Tangu siku hizo za Nagasaki, hakuna bomu jingine lililotumiwa vitani. Milipuko yote iliyofuata ilikuwa ya majarabio tu; ama jangwani au baharini kusiko watu.

Nchi nyingi zinaogopa kuhifadhi mabomu kulingana na uharibifu mkubwa ambao hutokana na kifaa hicho. Nchi zenye nguvu kubwa za kiuchumi na kijeshi kama; Marekani, China, Korea, Uingereza, Urusi zinaendelea kutengeneza mabomu. Tanzania ina ghala maalumu la kuhifadhia silaha kwa ajili ya kujihami. Ingawa ni vigumu kujua hasa, ni maeneo yapi yametengwa kwa ajili ya shughuli hiyo, kwa vile, suala hili ni la usalama wa nchi, si vizuri siri za nchi, zijulikane na wote kote.

Aprili 29,2009,saa tano asubuhi, ilikuwa ni balaa kwa wakaazi wa Mbagala, jijini Dar es Salaam, Mabomu, katika ghala ya silaha ya kambi ya Jeshi la Ulinzi la

Wananchi wa Tanzania namba 671 KJ.ghafla yalilipuka kwa mfululizo, yalisababisha maafa makubwa kwa wananchi wa Mbagala, vifo vya watu zaidi ya 20, kujeruhi zaidi ya watu 200, wengi wao walikuwa ni watoto.

Uharibifu wa nyumba na mali, miundombinu, mifumo ya umeme na maji, barabara zilichimbika, majengo ya Serikali k.v. Zahanati, Shule, Ofisi vilibomoka na kuharibika vibaya. Tukio la mlipuko wa mabomu ya Mbagala lilisababisha mshituko mkubwa, siyo tu kwa wananchi wa eneo hilo, bali kwa taifa zima na majirani. Wananchi wa Mbagala, walikuwa ni waathirika wakubwa zaidi wa mlipuko hiyo. Mamia ya watu walichanganyikiwa, wakihangaika na kukimbia nyumba zao kwa lengo la kujiokoa.

Katika harakati hizo, baadhi ya wananchi hao, walitumbukia kwenye mito wakapoteza maisha, wengine waliwasahau watoto wao na vikongwe majumbani na kupotezana nao kwa siku kadhaa. Barabara ya Kilwa, kuanzia eneo la Uwanja wa Maonesho ya Kimataifa ya Biashara, Kambi ya Jeshi ya Twalipo, hadi Mbagala Kizuiani, ilipo kambi hiyo, kulikuwa na askari wa JWTZ waliojipanga kando na kuongoza magari.

Wakaazi wengine wa Dar es Salaam, waishio nnje ya Mbagala, baadhi, walisikia milio ya mabomu na kuona moshi mweusi mkubwa ukipaa angani. Hali hiyo ilijenga khofu na wasiwasi mkubwa kwa wananchi. Walihofia usalama wao na wa ndugu zao. Watanzania waishio nnje ya Dar es Salaam walipata taarifa hizo katika Vyombo vya mawasiliano; Magazeti, Redio, Televisheni, mitandao ya simu na wavupepe.

Katika mapisi ya Tanzania, hili lilikuwa ndilo tukio la kwanza, silaha kubwa kujiripua. Watanzania hawana mazoea ya kusikia milio ya silaha kubwa, imezoelekea kusikia silaha za kawaida, za askari, wakiwa mazoezini, au wakati wa kupasua miamba mikubwa kwa ajili ya ujenzi.

Hata hivyo taarifa hutolewa kwa wananchi, siku kadhaa kabla ya tukio. Tukio la mabomu ya Mbagala lilipokelewa kwa hisia tafautitauti. Hadi sasa, wasiwasi huo haujawatoka wanachi. Wapo waliosema, limefanyika kwa makusudi, na wengine walisema, ni tukio la kiajali kama ilivyotokea ajali ya M.V Bukoba mwaka 1997, ajali ya treni Wilayani Mpwapwa katikati ya kituo cha Gulwe na Msagali na ajali za meli, Zanzibar, 2011 na 2012. Bi Madina Ali El-Buhriy ni Mtanzania mwenye hisia zake juu ya jambo hilo, katika shairi la “*Mabomu ya Mbagala*” (uk 138)

Haikuwa makusudi, ila mipango mibaya
 Halikuwa lenye budi, zisingefunguka nyaya
 Ni ajali, siyo kedi, ndugu kuwafika haya
WALE WAOMBAO SHARI, ITAZAMENI MBAGALA

Hayakuwa ya kulengwa, oneni zilivyo kaya
 Majumba yameborongwa, watu kuvunjwa mataya
 Na miguu kuchorongwa, wamebakia kugwaya
MSIOPENDA AMANI, ITAZAMENI MBAGALA

Mabomu ya Mbagala yalilipuka kwa kiajali, hakuna aliyepanga kutokea kwa tukio hilo baya. Jeshi la Wananchi, ambao ndiwo watunzaji wakuu wa silaha hizo, nalo pia liliathirika. Wanajeshi kadhaa walipoteza mali zao, walijeruhiwa na wengine sita walipoteza maisha. Meja A. M Muhidin, Sajini Amelye Mbeyale, Koplo Phinias Mwambashi, Koplo Mohamed Seif na Koplo Bernard Mbilo.



Kielelezo 4.1: Rais Kikwete na Naibu Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Emmanuel Nchimbi, wakiangali baadhi ya vipande na mabaki ya mabomu, vilivyookotwa katika eneo la Mbagala

Chanzo: Taarifa http://www.zenjydar.co.uk/2009months/200905/pages/20090501_mbagala.htm 9/06/(2014)

Ofisa Mteule Daraja la Kwanza, Timothy Mtwewe. Wataendelea kukumbukwa katika kumbukumbu za mashujaa wa taifa hili, ajali iliwakuta, wakiwa ghalani wakifanya kazi zao za kawaida. Aliyewaleta, ndiye aliyewatwaa. Mwenyezi Mungu Awapokee kwa huruma, kila mmoja, apewe haki yake, amina.

Ingekuwa ya dhamira, adui toka Ulaya
Kaja fosi kama jura, kushinda wale wa KAYA
Tusingepata nusura, kubaki hata unyoya
ENYI MUOMBAO VITA, ITAZAMENI MBAGALA

Pole zangu nazituma, familia zilizopwaya
Pa kukosa pa kuhema, na sasa mwawaya waya
Ombeni kwake KARIMA, subira iwe hedaya
ENYI MTAKAO VITA, ITAZAMENI MBAGALA.

Madhara ya mabomu ya Mbagala yalikuwa ni makubwa kwa wananchi wa eneo hilo na kwa taifa zima la Tanzania. Mbali ya wananchi, kupoteza maisha ya ndugu zao, na wengine, kupata vilema vya kudumu, bado eneo hilo, siyo salama kwa makaazi ya watu, Septemba 29, 2009, mabaki ya mabomu yalilipuka na kusababisha vifo vya watoto wawili na kujeruhi wengine watatu. Wananchi bado wana khofu kuwa, pengine kuna mabaki mengine ardhini, ambayo, yanaweza kulipuka muda wowote. Serikali inakumbushwa, kuchukua hadhari kubwa kwa kuwatumia wataalamu waliopo, wafanye uchunguzi wa kina, juu ya jambo hilo. Wananchi walipoteza mali zao, zikiwamo nyumba na samani, kaya 3,750 zilikosa mwahala mwa kuishi. Hali hiyo, ilisababisha, wakaazi wengi kukabiliwa na tatizo jipya la ukata, tangu kipindi cha tukio 2009 mpaka Serikali, ilipowalipa fidia, mwaka 2012.



Kielelezo 4.2: Sehemu ya Mabaki ya Nyumba, Baada ya Kulipuliwa na Mabomu, Eneo la Mbagala

Chanzo: Taarifa http://www.zenjydar.co.uk/2009months/200905/pages/20090501_mbagala.htm (12/06/2014)

Serikali ilisimamia ukusanyaji wa misaada iliyochoangwa na taasisi za Serikali na za binafsi na watu binafsi kwa ajili ya waathiriwa wa mabomu ya Mbagala; Uongozi wa juu wa Serikali ulitoa Sh milioni 200, Ofisi ya Waziri Mkuu Sh milioni 200, Bakhresa Sh milioni 100, Quality Group, milioni 30, Mwenyekiti wa IPP, Reginald Mengi Sh milioni 25, Vodacom Sh milioni 20, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Sh milioni 20, Manispaa zote tatu Ilala, Temeke na Kinondoni Sh milioni 60 na Mabohora Sh milioni 5.2. jumla ya Sh milioni 660.2 zilipatikana. Fedha hizo zilitumika kulipia gharama za mazishi, kununulia vyakula, maji, mablanketi na vyandarua, posho za wathamini, mafuta ya magari na posho za askari. Fidha kwa wahanga ni suala ambalo limetekelezwa kwa baadhi ya watu, lakini jumla ya watu 76, wamefungua kesi ya madai, Namba 181 ya mwaka 2011, katika Mahakama Kuu, Kanda ya Dar es Salaam, dhidi ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (chanzo:www.habarileo.co.tz.).

Milipuko ya mabomu ya Mbagala imetuachia fundisho la kuchukua hadhari katika mambo mengi ya kijamii; Kwanza, kambi za jeshi zisijengwe karibu na makaazi ya raia, ni vizuri zitengwe mbali, ili tatizo kama hilo likitokea, lisilete madhara kwa raia. Pili, kambi za jeshi, ziandae utaratibu maalumu wa kukagua usalama wa silaha kila inapobidi. Tatu, wananchi wa Tanzania, wasichezee amani na utulivu uliyopo, amani ikitoweka, tutapigana kwa mabomu yatakayogharimu uhai na mali za watu kama ilivyotokea Mbagala. Bi Madina Ali El-Buhriy anasisitiza:

Tuombeni kutwa kucha, AMANI tulozoweya
Kuparurana makucha, maneno yaso na haya
Nyoyoni tusijeficha, mwisho wake ni mbaya
NINYI MUOMBAO SHARI, ITAZAMENI MBAGALA



Kielelezo 4.3: Hii ndiyo Mbagala Iliyolipuliwa

Chanzo cha picha (<http://images.search.yahoo.com/yhs/search> 20/06/2014)

4.3.12 Dhamira ya Ugomvi/Mafarakano

Ugomvi ni neno linalotolewa fasili na Kamusi ya Kiswahili Sanifu (1981) kuwa ni hali ya kutokuwa na maafikiano, hali ya kuwa na fujo, hali ya kugombana. Ugomvi unahusisha pande mbili zikiwa na mitazamo tafauti juu ya jambo la aina moja, kila upande hutetea msimamo wake kwa kuona ni bora kuliko ule wa upande mwingine.

Uvunjifu wa amani unaosikika kote duniani, chanzo chake ni ugomvi wa maneno, mwafaka ukikosekana, mapigano hufuata. Baadhi ya mambo yanayochangia kutokea kwa ugomvi katika jamii ni; imani za dini, rushwa, mipaka ya nchi, matatizo ya ardhi, mapenzi, siasa, ubinafsi, ubadhirifu wa mali ya umma, usimamizi mbovu wa serikali, uchu wa madaraka n.k. kunapokuwa na mazungumzo, kunatakiwa yapatikane masikilizano, kusikilizana kwataka utuvu wa uwezo wa tafakuri na hekima. Mihamuko haimo katika haya. Wahemukao, ndiwo wapenzi wazuri wa ugomvi.

Tanzania kama ilivyo katika mataifa mengine, inakabiliwa na tatizo la ugomvi. Yapo matukio ya kutafautiana, miongoni mwa raia wa nchi hii. Zipo taarifa zinatolewa katika vyombo vya habari zinazojua ugomvi wa makundi ya kijamii; wakulima na wafugaji, wafuasi wa vyama vya siasa wanagombana, bungeni, kuna unaa miongoni mwa wabunge, mikutano ya kampeni za uchaguzi, watu wanaumizana, ofisini kuna fitina dhidi ya madaraka.

Waumini Mekanisani na Misikitini wanadhulumiana, wanapigana, wanatetana, wanashutumiana, wanatengana, wasanii wanaparuana. Madaktari hospitalini hawawapendi wagonjwa wao, bali rushwa zao n.k. Taaluma za kielimu, Siasa, Dini zitumike kuwaunganisha watu na zisiwe chanzo cha kuleta vurugu miongoni mwetu. Bi Madina Ali El-Buhriy ni Mtanzania anayekerwa na hali hiyo, kwa niaba ya wasanii wenziwe, katika shairi la “*Mwagombeani?*” anasema. (uk 127)

Sanishikwa ni butwaa, mwagombeani jamaa

Kurasa nikiambaa, namaizi zaa zaa

Nabaki kuchuchumaa, hatua nashindwa twaa

LINI HAYO YATAKAPOKWISHA, KWA SALAMA NA AMANI?

Ninazidi kuduwaa, mwili wataka pumbaa
 Kondo yenu natakaa, chini yanibwaga pwaa
 Mwagombea mishumaa, au jumu la dagaa?

LINI HAYO YATAKAPOKWISHA, KWA SALAMA NA AMANI?

Swali hili limeulizwa, kwa Watanzania wote, Linawalenga zaidi, wenye kuendekeza tabia za fitina, uadui, chuki, uhasama na unaa katika jamii. Tangu kipindi cha serikali ya awamu ya kwanza, Tanzania, imekuwa, ikikabiliwa na mlolongo wa matatizo ya ugomvi. Ugomvi mkubwa umejikita katika misingi ya kidini, ardhi na siasa. Mikoa yenye jamii mchanganyiko za wakulima na wafugaji, ugomvi wa ardhi umeota mizizi na hauwezi kuepukwa, kwa sababu ardhi ndiyo raslimali yao kuu ya kujipatia maendeleo ya kiuchumi. Tatizo ni kubwa zaidi katika maeneo yenye idadi kubwa ya makundi hayo; Mvomero, Handeni, Kilosa, Arusha, Serengeti, Kiteto, Kongwa, ambako kila mara, kuna taarifa za mapambano makali, ya kutumia silaha za moto zinazosababisha vifo vya watu. Watu wanapoteza maisha na kupata vilema vya kudumu. Yakichunguzwa, kunakutwa mikono ya matajiri na ya wenye vyeo katika utumishi wa Umma au wanasiasa wa chama hiki na chama kile. Silaha ni biashara, wapo wanaozitengeneza ili zinunuliwe, zitumike kwa khasara ya nchi lakini, kwa manufaa yao binafsi hao ndumilakuwili.

Kumekuwa na migogoro ya ardhi baina ya wanavijiji na wawekezaji. Tabia ya wawekezaji ni kumiliki kiasi kikubwa cha mashamba na kuwaacha wazawa katika maeneo madogo madogo, yasiyofaa katika shughuli za kilimo. Kutothamini jadi ya “masokola” ya mtama, mahindi, ufuta na kukata miti mikubwa iwe alama za mashamba ya kisasa, kumeongeza khasira za “piga nikupige”. Jambo hilo linasababisha manug’uniko, chuki na malalamiko kwa watendaji na wakaazi kote

nchini. Raia wanashindwa kuelewa ardhi yote ikimilikishwa kwa wawekezaji, jee watoto watapelekwa kuishi wapi? Jamii ya Wahadzabe na Wairaq, wa mkoa wa Manyara, wana ugomvi na mwekezaji, aliyepewa hifadhi ya msitu, walioutegemea kupata vyakula vyao vya asili k.v, asali, mizizi, ndege na majani, kwa karne nenda, karne rudi, leo kaja mgeni, ausema ni wake. Hiyo ni dhuluma mbaya sana katika nchi inayoongozwa na utawala wa kisheria.

Tarehe 3/10/2012 ilikua ni siku ya ugomvi kati ya wafuasi wa Dini ya Kikristu na Kiislamu, baada ya mtoto wa dhehebu la Kikristu, kukojolea Kitabu cha Mafundisho ya Dini ya Kiislam, katika eneo la Mbagala Kizuiani. Jambo hili lilizua tafurani kubwa, kwa wafuasi wa Dini ya Kiislam. Matokeo yake, ni uharibifu mkubwa ulitokea. Wakitumia silaha za mawe, kundi la Kiislam lilivamia mitaani na kuchoma makanisa. Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Mbagala Zakhem, Assembly of God (TAG), waliharibu Kanisa la Anglican, walivunja vioo katika Kanisa la Wasabato, na kuchukua vifaa vya muziki na ibada na kuviunguza hadharani. Magari ya polisi, namba T142 AVV, PT 0966 na T 325 BQP, basi la UDA na gari la Waandishi wa habari, kutoka Clouds.

Tarehe 3/4/2013, ilikua ni siku ya tukio jingine la kihistoria katika mji wa Tunduma. Wafuasi wa Dini ya Kikristu na wa Kiislamu walipigana, chanzo cha ugomvi ni nani mwenye uhalali wa kuchinja kitoweo? Kundi la watu wanaodaiwa kuwa ni wafuasi wa dini ya Kikristo, walikuwa na madai yao kuwa, waruhusiwe na wao kuchinja kitoweo na kuuza katika bucha zao. Matokeo ya vurugu hizo ilikuwa ni kuharibu nyumba za watu, kuchoma matairi barabarani na baadhi ya raia pamoja askari wa jeshi la polisi kujeruhiwa.

Viongozi wa Dini wanauawa ama kupigwa na watu wasiojulikana, mambo hayo yanafasiliwa kuwa ni uhasama wa Kidini uliojengeka miongoni mwa Watanzania. Tarehe 17/02/ 2013 kulikuwa na taarifa za kuuawa kwa Padre E. Mushi, Paroko wa parokia ya Minara Miwili Zanzibar. Aliuawa kwa kupigwa risasi na watu wasiofahamika. Tarehe 5/7/2014 kulikuwa na taarifa ya kujeruhiwa kwa Qiblatan Sood Ali Sood, Sheikh wa Msikiti uliopo Kilombero katika jiji la Arusha, alijeruhiwa kwa bomu la kurushwa kwa mkono akiwa anakula daku nyumbani kwake. Miongoni mwa watu wasiokuwa na hatia wala kuhusika na sababu za tukio hilo, alikuwa ni kijana mpita njia tu, kumtambua hali, kiongozi huyo wa Dini yake, naye aliathiriwa na bomu hilo.

Hayo ni baadhi tu ya matukio ya vurugu yaliyotokea katika nchi yetu katika kipindi cha miaka ya 2010 hadi leo. Matukio yote hayo, yanaambatana na uharibifu wa mali na kupoteza maisha ya watu. Hii ni dalili mbaya kwa Watanzania wote, Serikali kwa kutumia watendaji wake, k.v. Jeshi la Polisi wanapopata taarifa ya uvunjifu wa amani, wafike haraka katika maeneo ya matukio ili kusimamia usalama wa watu na mali zao.

Kila mwananchi anapoona dalili ya kuharibika kwa amani katika maeneo ya makaazi, taarifa ipelekwe haraka katika vyombo vya ulinzi na usalama. Ajabu, hata hilo likifanywa, polisi hawafiki mapema (kama watu wa zimamoto), wakidai kweli na si kweli, hawana magari ya kuwafikisha kwenye matukio kwa wakati. Usitawi wa jamii zote Ulimwenguni, msingi wake ni amani. Bi Madina Ali El-Buhriy anasisitiza:

Lumbeni yalo komaa, yasiyo ya kunjagaa

Za kuwaka kama taa, ufyosi kunyanyapaa

Nyoyoni zipate kaa, cheko ziwe haa haa

NI HAPO YATAPO KWISHA, KWA SALAMA NA AMANI

Raia wote nchini, wana haki sawa katika taifa lao, hakuna aliyejuu ya sheria. Viongozi na raia wote waheshimu misingi ya katiba, ambayo ndiyo sheria mama ya kuongoza nchi. Viongozi wafanye kazi kulingana na taratibu zilizowekwa na kutambua kwamba wajibu wao mkubwa ni kuwatumikia wananchi. Wananchi wasipende kuwalaumu watendaji katika kila jambo, subira, upole na uvumilivu unahitajika katika pande hizi mbili. Wafuasi wa vyama vya kisiasa waepuke lugha za jazba, kejeli, kuzomeana na matusi wakati wa mikutano yao. Wafuasi wa dini zote huamini kuwa, asili ya wanadamu ni moja, ambayo ni Mwenyezi Mungu. Hakuna kitabu cha dini kinachohimiza vitendo vya ugomvi, chuki, kutengana au kupigana. Asili ya wanadamu ni moja, Watanzania wasikubali kupotoshwa na makundi ya watu wachache, wenye nia mbaya ya kuligawa taifa kwa misingi ya Kisiasa, Kidini, Kiukabila ama kikanda. Misugvano haiwezi kuepukwa katika jamii, inapotokea utatuzi kwa njia ya amani upewe nafasi kubwa. Kwa kufanya hivyo, taifa letu litaendelea kufurahia umoja, amani na mshikamano.

4.4 Hitimishi

Siyo jambo jepesi kwa mtafiti kuweza kubainisha dhamira zote zilizojadiliwa na msanii. Jitihada za mtafiti zimefikia upeo wa kubainisha dhamira kumi na mbili tu. Utafiti huu uwe chachu ya kufungua mlango kwa wanazuoni wengine kuendelea kutalii mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy katika taaluma za fani na maudhui. Utafiti umebaini kwamba, mashairi hayo yamesheheni dhamira nyingi,

zinazozungumzia masuala muhimu ya jamii ya Watanzania; Dhamira ya kutenda na kutendewa mema, Dhamira ya utunzaji wa Mazingira, Dhamira ya Kuhamasisha wanawake katika utunzi wa mashairi, Dhamira ya umalaya katika jamii, Dhamira ya umuhimu wa Wazazi, Dhamira ya athari za hulka za binadamu, Dhamira ya kumbukizi, Dhamira ya matatizo ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, Dhamira ya Rushwa, Mabomu ya Mbagala, Dhamira ya ugomvi/mafarakano

SURA YA TANO

5.0 MATUMIZI YA FANI KATIKA USHAIRI WA BI MADINA ALI EL-BUHRIY

5.1 Utangulizi

Fani ni ufundi anaotumia fanani katika kuunda kazi ya kifasihi. Fanani huweza kutumia njia zinazomsaidia msanii kufikisha ujumbe wake kwa jamii. Huweza kutumia ujuzi wa kipekee katika vipengele vya lugha, wahusika, muundo na mtindo n.k. Katika utafiti huu, kipengele cha lugha, hasa tamathali za usemi, kimeshughulikiwa.

5.2 Matumizi ya Lugha

Lugha ni kipengele muhimu cha utamaduni wa jamii zote Ulimwenguni. Jamii zote hutambuliwa na hujitambulisha popote kwa kutumia kigezo hicho. Binadamu anaweza kutambulika kwa kuongea lugha yake au kwa sanaa yake kama vile ngoma, nyimbo, mavazi, uchoraji, ususi, n.k. Binadamu anapotaka kuonesha hisia zake na kuwavutia wengine kwa maneno mazito yanayoweza kumtoa msikilizaji machozi ya huzuni au ya furaha, msanii huchagua maneno makali yenye hisia tarajali. Hata katika sanaa ya jukwaani au sanaa nyingine, mtu hawezi kukikwepa kipengele cha lugha, ambacho ndicho mhimili mkuu wa sanaa yoyote. Kazi za fasihi haziwezi kuvutia, kufikisha ujumbe, kuburudisha au kuonya kama matumizi ya nyenzo kuu yaani lugha haikutumika vizuri.

Ili kazi ya fasihi iweze kukidhi haja ya hadhira lazima wawasilishaji wawe mahiri katika matumizi ya lugha. Katika muktadha wa utafiti huu, lugha ya Kiswahili

imetumika. Umahiri wa lugha unaozungumziwa ni matumizi ya lugha fasaha ambayo inajumuisha sarufi, muundo na vionjo muhimu katika lugha kama vile, tamathali za usemi, nahau, methali na misemo, ambavyo vina uwezo mkubwa wa kusesitiza, kushawishi, kueleza kwa usahihi, kile kilichokusudiwa, pasipo kuwa na mlolongo wa maneno mengi. Idadi kubwa ya mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy, una matumizi ya lugha ya kisanaa iliyoongeza msisimko na mvuto. Tamathali za usemi zimetumika zaidi, ili kudhihirisha ukweli wa jambo hilo. Uchambuzi umefanyika katika baadhi ya mashairi na kuweka bayana namna msanii alivyozingatia; Tashibiha, Sitiari, Taswira, Nidaa, Ratifaa, Tashihisi, Kejeli.

5.3 Matumizi Ya Tamathali za Usemi Katika Mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy

Mwamanda, (2008), Msokile, (1992), Senkoro, (1984), wanakubaliana kwamba tamathali za usemi ni neno au fungu la maneno, ambalo hutumiwa na wasanii wa kazi za fasihi ili kuibua na kujenga dhanna pana zaidi yenye kuongeza uzito katika jambo linalosimuliwa ama kuandikwa. Wakati mwingine, hutumiwa kama njia ya kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha. Kwa jumla, tamathali za usemi ni maneno au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii au waandishi wa kazi za fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata katika sauti za kusema au za maandishi. Hutumika katika fasihi kwa lengo la kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu katika lugha iliyotumika katika kazi inayohusika. Tamathali hizo huweza kugawanyika katika vipengele tafautilautila, kama vile, tamathali za ulinganishi, tamathali za mafumbo, tamathali za msisitizo. Hii ina maana, kwamba, ili msomaji wa kazi yoyote ya fasihi apate ujumbe, hana budi kufikiri kwa kina.

5.3.1 Lugha ya Tashibiha

Tashibiha au Mshabaha ni aina mojawapo ya tamathali za usemi, inayofanya kazi ya kulinganisha vitu viwili visivyo na hadhi sawa kwa kutumia viunganishi kama; mithili ya, mfano wa, sawa na, kama vile. Mara nyingi, aina hii ya tamathali za usemi huweza kufanya kazi, endapo tu pana vitu viwili vinavyolinganishwa, wakati, kimoja, hutumiwa katika kukirejelea na kukielezea kingine, na aghalabu, kimoja kati ya vitu hivyo, huwa kinaeleweka na hivyo hutumiwa ili kuangazia hicho kingine. Taasisi ya ukuzaji Mtaala (1988). Tashibiha zilizotumika katika shairi la *Sumu tamu na utenzi wa wanawake na Ukimwi*; (uk 145 na Uk 152)

Uliifanya dhamira, mjini ukaisaga
 Kuhakiki yako dira, kila pande ukamwaga
Ukahaha kama jura, watu ukawavuruga
 SUMUYO KWANGU ASALI, SISHITUKI WANGU SHOGA

Wewe ni mtu huria, nani atayekuroga
 Na utuvu kuwania, ni vyema awache woga
Au yatakuchachia, unuke kama mzoga
 NDIPO NANENA KWEKOGA, BALI KUNAJIMWAGIA

Ugonjwa huu hatari,
kali sawa na Nari
 unauwa kwa chanjari
 umepoteza mamia

Hasha usifanye ngowa, kuwa zuzu tena zidi
Ishi kama mwananjiwa, shibe yako ni juhudi
 Basi shukuru Mwelewa, Mjuzi Aso inadi
 KHASA JITENGE BAIDI.

Hamuwi nyote shujaa, zizi moja mkakaa

Nzito mbavu zilojaa, mnaruka kama paa

Khatima ni kuzagaa, hasada kubwa kivyaa

LINI YATAKAPO KWISHA, KWA SALAMA NA AMANI?

Kwa kutumia tamathali za usemi, msanii ameshughulikia mambo makuu matatu kwa kuyahusisha ili kuongeza uzito wa dhamira. Mambo yaliyohusishwa ni Kizungumzwa, Kifananishi na Kiungo. Kizungumzwa ni kitu halisi, ambacho huzungumzwa, na kitu kinachofananishwa kwa fumbo, kifananishi kipo katika mawazo, na huzingatia maana dhahania, na kiungo ni sifa zipatikanazo katika kitu kinachozungumzwa. Kazi yake kuu ya tashibiha ni kuhusisha vitu vyote viwili katika kuunda maana kama ilivyoonekana. *“Au yatakuchachia, unuke kama mzoga”*. Viongozi wala rushwa wanatahadhari na msanii kuwa, tabia ya kupokea rushwa haifai, inadharirisha utu wao, inapoteza udhati wa taaluma zao, inapotosha maadili ya taaluma zao. Ndiyo maana anawaambia kuwa wananuka kama mizoga. Kinukacho kimeoza, hakifai kwa matumizi ya binadamu.

5.3.2 Lugha ya Sitiari

Sitiari ni dhanna katika taalimu ya fasihi yenye maana ya kufananisha vitu ili vionekone vipo sawa. Taasisi ya ukuzaji mitaala (1988) wanasema, Sitiari ni tamathali ya usemi inayolinganisha kitu kimoja na kingine, kwa kuvifanya viwe sawa. Tamathali hii, huhawilisha maana ya vitu kwa kuvifananisha, katika uwiano ulio sawa. Uhawilishaji huo, hujidhihilisaha katika vipengele vya sifa au tabia. Sitiari ni tamathali ya usemi ambayo iko sawa na tashibiha lakini hulinganisha vitu ama watu bila kutumia viunganishi linganishi vya mithili ya, sawa na, kama, na kama vile. Kwa hiyo, vitu au watu, hulinganishwa kana kwamba vipo/wapo, sawa sawa

kabisa. Binadamu, katika mwingiliano wake na mazingira, hujifunza kuunda dhanna kidhahania kwa kuhusisha mambo yake, na vitu anavyoviona, ama kuvisikia, katika mazingira hayo. Bi Madina Ali El-Buhriy, hakukwepa kutumia lugha hiyo katika shairi la *Mbebe angali lala na Usisubiri*; (uk 125 na 150)

Ya urefu kama rula, hayatopimwa kwa tola
 Tabu kama palahala, utadhani wewe sila
Thamani yako pagala, utupwe kwenye jalala
 ALIVYO MWANA MWENZIO, M-BEBE ANGALI LALA

Nasema usifikiri, usinambe ni ayari
 Kwa kuwa sipendi shari, walau japo ghururi
Huu wangu ujabari, si-uuzi kwa dinari
 NASEMA USISUBIRI, NA WALA USIFIKIRI

Katika shairi la *Usisubiri*, kuna sitiari ya *Huu wangu ujabari, si-uuzi kwa dinari*. Tafsiri iliyopo ni kwamba, binadamu, anazo sifa au tabia za jabari/ mwamba. Sifa hizo, zaweza kuwa ni ujasiri, ubabe, ukubwa, nguvu, unene. Katika mfano huo, kizungumzwa ni binadamu, kifananishi ni jabari na kiungo ni sifa ama tabia za kijabari. Katika shairi la *M-bebe* kuna sitiari ya *Thamani yako pagala, utupwe kwenye jalala*.

Kwa muktadha wa kisanii ni kuwa, thamani yake binadamu, inalinganishwa na pagala. Sifa za pagala ni sehemu chafu, isiyokuwa na thamani, ni pahala ambapo, hapafai kuishi, binadamu. Sitiari hii, ikifafanuliwa zaidi, inatuambia mengi, juu ya binadamu anayefananishwa na taswira ya jalala. Hali hiyo, humjengea msomaji, hisia za kushangaa, kuhisi kinyaa, woga, huruma, wasiwasi n.k. Lengo la wasanii (wa

kazi za fasihi), kutumia sitiari, ni kufananisha vitu vyenye asili na mazingira tafautitafauti ili kuongeza uzito wa kazi zao.

5.3.3 Lugha ya Tashihisi

Tashihisi ni tamathali ya usemi, ambayo vitu visivyokuwa na uhai na vyenye uhai, kama, udongo, moto, milima, maji, kiti, nyumba, wanyama, wadudu, mimea. Hupewa hulka ya kibinadamu na vipawa vya kufananisha matukio na mwenendo, kama anavyoweza kutenda mwanadamu. Bi Madina Ali El-Buhriy, ametumia tamathali hiyo katika Shairi la *Yakupi Mashi na Ndoto*; (uk 139 na 148)

Majani yanakambuka, yote yakiwazunguka
Yevu yakichegeleka, kwa khofu kutoiweka
 Zimenyauka na nyika, ni nyembamba ja ndakaka
 KWETU MWEVU NI MASOKA, NA SASA YAKUPI MASHI

Kochi lilinipakata, bila khofu nikawanda
 Na meza yenye kusota, ikawekwa kwenye panda
 Ya vyakula, ni kashata, yaso idadi matunda
 NDOTO INGEKUWA KWELI, WALLAHI NINGEFAIDI

Katika shairi la *Yakupi Mashi*, msanii ametumia *majani*, kitu ambacho, kwa asili, hakina uwezo wa kutenda jambo lolote. Maisha yake, hutegemea uhai wa mti. Katika muktadha wa kazi hii, majani yanapewa hulka za kibinadamu, uwezo wa kukumbuka, kuzunguka na kujenga khofu dhidi ya uhai wake. Matendo yanayotajwa kutendwa na majani, siyo jambo la kweli kiuhalisia, bali msanii analazimika kuhuisha ili kudhihirisha dhanna ya sanaa katika maandishi ya kifasihi. Katika shairi la *Ndoto*, kochi ni samani inayotumika kupumzikia. kochi limepewa urazini wa kibinadamu, *Kochi lilinipakata, bila khofu nikawanda*, limepewa uwezo wa

kumkumbatia binadamu. Wasanii hutumia tashihisi ili kuvutia wasomaji na kuweka uzito kwenye kazi zao. Jambo hilo ni muhimu kwani kazi za fasihi zinahitaji kutumia lugha nzito, inayohitaji mzamo na umakinifu mkubwa.

5.3.4 Lugha ya Kejeli

Lugha ya kejeli hutumia maneno ya kawaida lakini maana zake, huwa na maana ya kinyume cha jambo, linalozungumzwa. Mtu, anaweza kusifiwa, lakini katika muktadha wa kejeli, ina maana ya dharau. Mara nyingi, tamathali kama hii, hutumika zaidi katika makundi ya watu wanaotania, marafiki, marika mamoya n.k. Katika mazingira mengine, lugha ya kejeli, inaweza kumuudhi anayesemwa, lakini siyo nia ya mtumiaji kufanya hivyo. Mara nyingi, nia ya kejeli, ni kutoa onyo bila kusababisha bughudha kwa mlengwa.

Katika kazi za fasihi siyo rahisi kugundua matumizi ya lugha ya kejeli kwa kusoma mstari mmoja wa mtunzi ama ubeti mmoja wa shairi. Lahasha! Inabidi ipatikane aya nzima ya msanii au beti kadhaa. Kwa kupitia kifungu kilichobeba wazo zima la msanii ndipo kutaonekana matumizi ya lugha ya kejeli. Katika shairi la *sumu tamu*, Bi Madina Ali El-Buhriy anasema: (uk 145)

Uliifanya dhamira, mjini ukaisaga
Kuhakiki yako dira, kila pande ukamwaga
Ukahaha kama jura, watu ukawavuruga
SUMUYO KWANGU ASALI, HUNISHANGAZI RAFIKI

Mimi tafanya, sukari, chaini kuikoroga
Nichanganye na bizari, vyovyote nitaviriga
Hiyoyo nile kwa ari, huku nacheza mabega
SUMUYO KWANGU NI TAMU, HUNISHANGAZI RAFIKI

Hapa itakuwa tamu, nitaramba kwa kunoga
 Niile kwa shamu shamu, na huku niki-kukoga
 Mie hutanidhulumu, jua kinaga ubaga
 SUMUYO KWANGU ASALI, HUNISHANGAZI RAFIKI.

Sumu ni dawa yenye kemikali za kukidhuru kiumbe hai, agharabu hupoteza maisha ya kiumbe hicho. Wapo binadamu wenye tabia zinazofananishwa na sumu. Sumu ya mwanadamu, kwa mwanadamu mwenzake, ni fitina, chuki, uadui, uhasama, chokochoko, hasada, umbeya. Matokeo ya tabia hizo, kwa pamoja ni kusababisha ugomvi, utengano, mifarakano, ambayo inaweza kupoteza uhai wa mtu au watu.

Katika ubeti wa kwanza, msanii ameonesha jinsi mafatani wanavyoandaa sumu dhidi ya binadamu wenzao. Msanii anatumia lugha ya kejeli kwa mafatani, badala ya kuonesha, khofu kuwa sumu, huleta madhara, anawaambia kuwa, sumu zao ni *sukari, ataunga na bizari kisha atakunywa*. Sumu ni *asali, italiwa kwa shamu shamu na kurambwa yote*. Katika mazingira ya kawaida, sumu siyo chakula, bali ni kitu cha hatari, kwa uhai wa mwanadamu. Kwa kuwa fasihi ni mchezo wa maneno, ni ruksa lugha ya kejeli kutumika ili kuongeza msisitizo wa uibuaji wa dhamira.

5.3.5 Lugha ya Ritifaa

Ritifaa ni aina ya usemi, ambao mauti huombolezwa na kuliliwa, au kusifiwa kama vile nafsi yake ingali hai. Ratifaa huweza kujitokeza katika mazingira maalumu. Mawazo dhahania kwa wakumbukwa, hujitokeza wakati wa maombolezi, maombi kwa Mizimu, manung'uniko kwa wateswaji. n.k. Bi Madina Ali El-Buhriy, anawainua wakumbukwa, waliogusa nafsi yake, wakati wa uhai wao. Kwa majina anawataja, Akida, Kibao, Gongu, Ndumba katika shairi la *Enzi zao* na Rehema katika shairi la *Rehema Mwakangale*: (uk 130 na 133)

AKIDA pia KIBAO, rudini tena upesi
 GONGA, NDUMBA njoo mbio, muone hali halisi
 Sasa imekuwa mwao, hatuna njema nafasi
 ZIKO WAPI ENZI ZAO.
 Ona hata MTU CHAKE, kasusia karatasi
 makeke, tunavyokwenda kwa kasi
 Tumebakia wateke, tunapakana kamasii
 ZIKO WAPI ENZI ZAO

Nakukumbuka REHEMA, vipindi kwako si ndwele
 Taarifa ukisoma, inatua hadi Hale
 Utadhani nyoka moma, wafoka pasi simile
 BINTI WA MWAKANGALE, AMEFARIKI REHEMA

Uhaio umekoma, mwilini haupo pale
 Wadau wako twahema, umebaki mfulele
 Tumeyashika matama, waume pamwe wavyele
 BINTI WA MWANGALE, AMETUTOKA REHEMA

Kwa kutumia lugha ya ritifaa msanii amejenga upya nafsi za wakumbukwa, amepata nafasi ya kuongea naona amewaambia yanayojiri baada ya kuondoka kwao duniani. Kinachokosekana hapo, ni majibizano na hao wakumbukwa. Wasanii wa fasihi, hutumia tamathali hii, kama njia ya kuonesha uhusiano uliyopo kati ya binadamu walio hai na waliofariki dunia, pia ni njia nzuri ya kuhimiza matendo mema, binadamu wenye matendo mema huingizwa katika kumbukumbu za kijamii kutokana na michango yao.

5.3.6 Nidaa

Nidaa ni tamathali ya usemi ambayo huonesha kushangazwa kwa jambo fulani. Misemo hii huambatana na matumizi ya alama za mshangao katika kukubali jambo,

kuchukia au kuonesha heshima maalumu. Ni sauti atowayo mtu ili kudhihirisha muono wake wa ndani, namna anavyoweza kuguswa na tukio au taarifa fulani. Nidaa hubeba taarifa tafautitafauti k.v furaha, huzuni, masikitiko, mshangao. Bi Madina Ali El-Buhriy ametumia lugha hiyo, katika shairi la *Hulka yako pera*; (uk 128)

Lingekuwa la kupikwa, libandikwe kwenye jiko
Na viungo vingepakwa, vya kukaanga kwa miko
Ai!! Hilo la kumakwa, linatupa tetemeko
KUTOIVA TUMBA ZAKE, NI HULKA YAKE PERA.

Waandishi wa kazi za fasihi hutumia nidaa kwa lengo la kuonesha kushangazwa au kushangaa juu ya mambo yaliyokuwa yakifanywa na baadhi ya wahusika. Mshangao huo ndio unaosisitiza maana husika.

5.3.7 Lugha ya Takriri

Takriri ni tamathali ya usemi ambayo hujikita na urudiajirudiaji wa maneno, silabi au sauti zinazolingana katika kazi ya fasihi. Mwandishi huamua kwa makusudi kurudirudia maneno au vipengele hivyo kwa lengo maalumu kwa kusisitiza jambo ama kuleta mkazo wa jambo linaloelezwa. Msokile (1992), Takriri ni aina ya uzungumzaji ambapo kwa makusudi maneno hurudiwarudiwa na msanii, ili kutia msisitizo juu ya jambo linalizungumzwa. Takriri inaweza kujitokeza katika ngazi ya vina, neno au mstari. Katika shairi la *Silumbi na Wapujufu na Mwagombeani?*.

(uk 127 na 146)

Naona *wachimbachimba*, kwenye hili letu Jimbo
Mng'ong'o wasaka nyumba, japo ya mama wa kambo
Kwa upole si umwamba, karibu ufunzwe mambo
KWA KUIKHOFU NAZAA, SILUMBI NA WAPUJUFU

Lumbeni yalo komaa, yasiyo ya kunjagaa

Za kuwaka kama taa, ufyosi kunyanyapaa

Nyoyoni zipate kaa, cheko ziwe haa haa

NI HAPO YATAPO KWISHA, KWA SALAMA NA AMANI

Katika ubeti wa kwanza kuna matumizi ya takriri neno, msanii ametumia neno *chimba* kwa kulirudia rudia. Kwa mkutadha wa kazi hii, kinachosisitizwa hapo ni tabia ya uchokozi, kuhangaisha, kusumbua. Ubeti wa pili, kuna neno *haa haa*, ambalo kwa mkutadha ya kazi hii linaashilia kicheko cha furaha. Takriri vina imejitokeza katika kazi nzima ya msanii, katika kila shairi, vina vya kati, kwa kila mshororo vinafanana, hata vile vya mwishoni, navyo, vya aina moja.

-----mba, -----mbo

-----mba, -----mbo

-----mba, -----mbo

-----Mshororo wa kituwo-----

-----maa, -----gaa

-----taa, -----paa

-----kaa, -----haa

-----Mshororo wa kituwo-----

-----va, -----ko

-----va, -----ko

-----va, -----ko

-----Mshororo wa kituwo-----

5.3.8 Tabaini

Tabaini ni tamathali ya usemi inayosisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani, agharabu mofimu ya ukanushi si au siyo hutumika katika usemi huo. Tabaini hujitokeza ikiwa na pande mbili zinazopingana kimantiki ili kuongeza uzito wa msisitizo. Katika shairi la *ndoto*: (uk 148)

Nililala nikaota, safari ndefu nakwenda

Hatamu nimefumbata, za farasi si za punda

Njia nzuri ninapita, kwa furaha nina randa

NDOTO INGEKUWA KWELI, WALLAHI NINGEFAIDI

Katika ubeti huo, tabaini imetumika kuisisitiza dhana ya utendaji katika ushairi. Msanii anasisitiza juu ya ufahari wa matumizi ya wanyama katika safari. Farasi na punda wote hufanyakazi ya aina moja kubeba mizigo na watu lakini hadhi zao ni tafauti. Farasi ni mwenye thamani ya juu kuliko punda. Tofauti ya hadhi, ndiyo msingi wa ujenzi wa tabaini.

5.2.9 Lugha ya Taswira

Lugha ya taswira ni uwasilishaji wa mawazo, dhanna au hoja kwa njia ya vielezeo vinavyojengwa kwa maneno, msingi wa taswira upo katika ujenzi wa picha katika fikra za msomaji. Katika fasihi taswira zinaweza kugawanywa katika makundi matatu, taswira za bayana, taswira za mawazoni na taswira za hisi.

5.3.8.1 Taswira Zinazoonekana

Taswira zinazoonekana ni picha zinazojengwa kwa kutumia vielelezo tunavyovijua na vinafahamika katika maisha yetu ya kila siku. Katika shairi la *Kisichofunga kipochi*; (uk 136).

Kingejaa majinoti, ya mia na maelufu

Kisibane katikati, japo kwa chake kikufu

Kabisa sikifumbati, radhi nishike hanjifu,

HADHI HAKINA DAIMA, KISICHOFUNGA KIPOCHI

Hadhi yake siipati, mie nina kikashifu

Kiwazi kila wakati, kinanipa taklifu

Huona walio shoti, na wasio insafu

SIKIWEKI KWENYE SAFU, KISICHOFUNGA KIPOCHI

Beti hizo zimetumia taswira bayana, hadhi ya kipochi ni kufungwa kwa zipu. Bi Madina Ali El-Buhriy anaona kuwa pochi ikikosa zipu hakina hadhi. Kwa mkutadha wa kazi hii, msanii anawafananisha wanawake wenye tabia za umalaya na kipochi kilichokosa zipu. Hivyo hawana thamani katika jamii.

5.3.8.2 Taswira za Mawazoni/Kufikirika

Taswira hizo zinatokana na mawazo yanayohusu mambo yasiyoweza kuthibitika ama kuonekana katika uhalisia. Katika shairi la *Ndoto*: (uk 148)

Nililala nikaota, safari ndefu nakwenda

Hatamu nimefumbata, za farasi si za punda

Njia nzuri ninapita, kwa furaha nina randa

NDOTO INGEKUWA KWELI, WALLAHI NINGEFAIDI

Nikafika kwenye banda, lililo na kubwa kuta

Ambazo hazikupinda, na rangize kama nta

Nikashuka kwa kudanda, mlangoni nikapita

NDOTO INGEKUWA KWELI, WALLAHI NINGEFAIDI

Safari inayozungumzwa na msanii ni safari ya kimawazo tu, ni safari ya kifahari.

Usafiri wa kuaminika juu ya farasi na mapokezi makubwa kuyapata kutoka kwa

mwenyeji wake katika nyumba ya kifahari. Taswira inayojitokeza hapa ni hali ya matumaini ya wanachi kujipatia maisha bora, lakini wanapoingia katika uhalisia, mambo huwa ni kinyume, huandamwa na ukata. Matumaini ya maisha bora huendelea kubaki mawazoni tu.

5.3.8.3 Taswira za Hisiya

Picha hizi hujihusisha na hisiya za ndani zinazoweza kumfanya msikilizaji au msomaji awe na wasiwasi, aone woga, apandwe na hasira, ahisi kinyaa n.k. Picha hizo zina nguvu kubwa ya kunaswa na akili ya mwanadamu. Katika shairi la *Mabomu ya Mbagala*;(uk 138)

Hayakuwa ya kulengwa, oneni zilivyo kaya
Majumba yameborongwa, watu kuvunjwa mataya
Na miguu kuchorongwa, wamebakia kugwaya
MSIO PENDA AMANI, ITAZAMENI MBAGALA

Ingawa msomaji hajafika kwenye eneo la tukio lakini msanii amemfikisha kitaswira. Ameoneshwa majumba yaliyoborongwa, watu kuvunjwa mataya na miguu kuchorongwa. Hisiya za taswira kwa msomaji ni khofu, mashaka, huruma na majonzi kwa wahanga wa mabomu ya Mbagala.

5.4 Hitimishi

Tamathali za semi zilizotumika katika kazi hii zimeonesha mchango mkubwa katika kuibua na kukamilisha dhamira za mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy. Dhima kubwa ya tamathali za usemi katika sanaa ya fasihi, ni kuongeza uzito na msisitizo wa mambo yanayojadiliwa na msanii, kuunda maana mpya na kuwawezesha wasomaji wapate hamasa ya kuzama zaidi ili wapate mantiki ya kazi. Matumizi ya

tamathali za usemi yanahitaji ufundi mkubwa wa mtunzi, namana ya uteuzi wake na pahala mwafaka panapofaa kuzitumia, kazi ya aina hiyo inahitaji weledi mkubwa kwa wasomaji, umakini usipozingatiwa kwa wasomaji, wanaweza kuposha maudhui ya mtunzi.

SURA YA SITA

6.0 MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

6.1 Utangulizi

Katika sura hii kuna muhtasari wa kazi nzima, matokeo ya utafiti yameelezwa kwa kifupi, pamoja na maoni na mapendekezo yaliyofikiwa baada ya kufanya utafiti wa mashairi ya Bi Madina Ali El- Buhriy.

6.2 Muhtasari wa Utafiti

Walibora (2012) anasema kwamba mashairi ndiyo hisabati ya fasihi, inayohofiwa na baadhi ya wanafunzi ingawa hufurahiwa na wanaozimudu, ndivyo ilivyo raha kwa wale wanaoimudu fani ya Ushairi. Wengine watasema labda ni vipaji. Watu wote hawawezi kujaaliwa kwa kima kimoja, kujumlisha moja na moja au kuzidisha mia kwa mia. Ingawa kweli kuna vipaji misingi imara ni muhimu vile vile. Wanafunzi wakifundishwa tangu mwanzo, misingi na vipengele mwafaka vya fani yoyote, wanaweza kuikabili fani hiyo kwa kujiamini, pia wanafunzi wakiwa na mwelekeo bora, hawatatishwa na ugumu wa fani yenyewe. Bi Madina Ali El-Buhriy, ni miongoni mwa wanawake wachache, waliothubutu na kuikabili kikamilifu fani ya ushairi. Kwa ufundi mkubwa, ameitumia fani hii kubainisha masuala yanayolikabili taifa la Watanzania.

Utafiti huu uliongozwa na madhumuni matatu. Kwanza kuanisha tungo za Ushairi wa Bi Madina Ali El-Buhriy, pili kuchambua maudhui yanayopatikana katika tungo za Bi Madina Ali El-Buhriy na tatu kutathimini matumizi ya tamathali za usemi ilivyosaidia kushadidia maudhui katika mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy. Katika

kufanikisha madhumuni ya utafiti huu, mashairi yamekusanywa na kuchambuliwa kifani na kimaudhui.

6.2.1 Pengo la Utafiti na Namna Lilivyoziwa

Pengo la utafiti lilikuwa ni kwamba, utafiti mwingi uliofanywa na wanazuoni katika mada za mashairi ya Arudhi ya Kiswahili, umehusisha watunzi wa kongwe kama vile, Shaaban Robert, Saadan Kandoro, Mwanakupona binti Mshamu, Khatibu, Bi. Mwanakupona Binti Msham, Mnyampala, Sengo, Amri Abed. Baadhi yao ni wa zama za miaka ya karne ya 19 hadi 21, isitoshe wengi wao ni wanaume. Washairi chipukizi, hasa wanawake wamesahauriwa. Utafiti huu, umeziba pengo hilo, kwa kumwibua msanii mpya, ambaye ni Bi Madina Ali El-Buhriy, kazi yake imedhihirisha kwamba, wapo watunzi wa mashairi wanawake, ambao jamii inapaswa kuwatafuta, kuwatamba na kuweka wazi kazi zao, ili zisomwe na watu wengi kwa manufaa ya taifa la Tanzania.

6.2.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Lengo limefanikiwa kukusanya jumla ya mashairi ishirini na mbili na utenzi mmoja, Katika mashairi yaliyochambuliwa utafiti umefanikiwa kuibua dhamira kumi mbili. Kutokana na dhamira zilizojadiliwa, tumebaini kwamba, mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy yamebeba dhima kubwa za kijamii ambazo ni kuonya, kukosoa, kuadibu, kuelekeza, kushawishi. Utafiti umebaini kuwa maudhui hayo yanasawiri hali halisi ya maisha ya Watanzania.

Kutokana na njia ya uwasilishaji wa kazi za Bi Madina Ali El-Buhriy kutumia redio na magazeti imesababisha, kazi hizo kuwa katika mtawanyiko mkubwa. Mpaka leo

hii ni mashairi manne tu, ambayo yamechapishwa katika kitabu cha Wajaleo Diwani ya mashairi (2012) Mashairi yaliyopata nafasi ni *Washairi kina mama, kisichofunga kipochi, Buriani mwalimu Nyerere na Ndoto*. Mashairi mengine yaliyosalia yamebaki kama miswada inayosubiria kupata wahisani wa kuichapisha ili kupata vitabu vya kiada na ziada. Bado tunaamini kwamba, idadi ya mashairi inaweza kuwa ni kubwa zaidi ya hayo yaliyopatikana katika tasnifu hii.

Matumizi ya lugha, idadi kubwa ya mashairi yameandikwa kwa lugha ya Kiswahili fasaha, lugha ambayo inaeleweka na Watanzania wengi, ambao ndiyo walengwa wa kazi hii. Mashairi ametumia tamathali za usemi na mafumbo ili kuweza kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira. Matumizi mazuri ya kipengele hicho yameweza kuficha na kuepusha lugha ya karaha kwa wasomaji. Kwa hiyo, maswali matatu yaliyoongoza utafiti huu yote yamepata majibu.

6.3 Mapendekezo

Kutokana na uchunguzi uliyofanyika katika mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy, tasnifu hii inatoa mapendekezo yafuatayo”

6.3.1 Mapendekezo Katika Utafiti Ujao

Ni vema katika tafiti zijazo kuchunguza mchango wa wasanii wengine, hasa wanawake ambao kazi zao bado hazijawekwa wazi na kusomwa na kundi kubwa la watu, mfano nyimbo za taarabu zilizotungwa na kuimbwa na marehemu Fatuma binti Baraka na mashairi ya Shekha Salim Bathawab.

6.3.2 Mapendekezo kwa Wasanii wa Mashairi

Wasanii watambue kwamba jamii inawategemea wao kutumia vipaji vyao, walivyojaaliwa na Mwenyezi Mungu, kumulika kila kona ya nchi ili kuweka wazi

maovu ya kila aina, yanayojitokeza miongoni mwetu k.v, ukandamizaji, unyanyasaji, unyonyaji. Wasanii waepuke kutoa tungo zenye mwelekeo wa kuleta mafarakiano, chuki, unafiki wa kujipendekeza kwa wanasiasa. Badala yake watungie dhamira zinazolenga kuhimiza mienendo bora ya utamaduni wa Mtanzania.

6.3.3 Mapendekezo kwa Jamii

Tunaikumbusha jamii kuwa, maarifa na stadi nyingi za maisha hutunzwa kwa njia ya maandishi na kwenye mitandao ya kisasa, ni wajibu wetu sote, kujenga utamaduni wa kujisomea machapishi na kuyachunguza kwa kina ili kupata udhati wake.

MAREJELEO

- Abeid, A. (1973). Ushairi wa Kiswahili; na uhuishwe usiuliwe, katika *Zinduko*
- Abilatif, A. (1973). “*Ushairi wa Kiswahili na Uhuishwe Usiuliwe*” Katika *Zindiko*, Dar es Salaam, Chama cha Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Abilatif, A. (1971). *Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawa*. Oxford University Press, Nairobi.
- Alhabib, E. A. (2012). *Matumizi ya Taswira Katika Nyimbo za Taarabu*, Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam.
- Aronson, J. (1992). “*A Pragmatic view of Thematic Analysis*” in the Qualitative Research Methods in Nursiny. Pp (37-73), Orlando FL: Grune & Stratton.
- Babbie, E. (1999). “*The Basics of Social Research*”, Belmont, Wadsworth.
- Balisidya, M. L. 19 (1979), “*Utafiti, Mbinu na Ukusanyaji wa Fasihi Simulizi na Hatima Yake*”, Lugha yetu. 34, 36.
- Best, J. W & Kahnn, J. V (2003), “*Research in education*”, Englewood, pretence Hall.
- Carter, D. (2006). *The Pocket Essential: Literary Theory*, harpenden, herts ALS5 IXJ.
- Chiraghadin, S. (1977). *Utangulizi wa Malenga wa Mvita*. Oxford University Press
- Eagleton, T. (1996). *Literary theory: An introduction, Vol 2*, United States, The University of Minnesota Press.
- Finnegan, R. (1976). “*All Literature in Africa*”, Nairobi, Oxford University Press.
- Harries. L. (1962). *Swahili Poetry*, Oxford, University Press.
- Johanes, A. M (1959). “*Studies in African Music vol1*”, London, Oxford University Press.

- Johnson, B & Christensen, L (2000). *“Education Research, Quantitative and Qualitative Approaches”*, Allyn and Bacon, London.
- Kandoro, S. A (1978). *“Ushahidi wa Mashairi ya Kiswahili”*, Longman, Tanzania.
- Kandoro, S. A (1972). *Mashairi ya Saadani Mwananchi Publishing*, Dar es Salaam
- Keys, B na Wenzake (1989). *“Four Faces of Fully Function Middle manger”*, California Management Review, Vol. XXIV, No, 4pp, 59-67.
- Kezilahabi, E. (1983). *“Uchunguzi Katika Ushairi wa Kiswahili”*, TUKI, Dar es Salaam.
- Kezilahabi, E. (1981). *“Ushairi na Nyimbo Katika Utamaduni wetu”*, katika *Urithi wa Utamaduni Wetu*, Dar es Salaam, Tanzania Publishing House.
- Kezilahabi, E. (1983), *“Nafasi ya Fasihi Simulizi katika Jamii ya Tanzania”*, Mulika na 15, Dar es Salaam, Taasis ya Uchunguzi wa Kiswahili.
- Kiango S. D na wenzake (1987), *Uhakiki wa vitabu vya uhakiki, Sekondari na vyuo*. Nyanza Publication Agency.
- Khalifa, A. I. S. (2012), *Usawiri wa Masuala ya Kijinsia Katika Lugha ya Mashairi. Mifano Kutoka Mashairi ya Bongo Fleva Tanzania. Tasnifu ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Knappert, J. (1979), *Four Centuries of Swahili Verse*. heinemann
- King’ei, K. (2001), *“Kioo cha Lugha, Fasihi, Idara ya Kiswahili”*, Chuo Kikuu Cha Dar Es Salaam.
- Kitogo (2002), *“The Poetic Contribution to Political Development”*, A case study of Saadan Abdul Kandoro, unpublished M.A Thesis UDSM.
- Kombo, D.K. na Tromp, D. L. (2006), *“Proposal and Thesis Writing”*, Nairobi, Paulines Publications Africa.

- Koul, L. (2006), *“Methodology of Education Research”*, New Delh, Vikas Publishing.
- Kothari, C .R (2003), *“Research Methodology Methods and Techniques”*, Wishwa Prakashan, NewDelh.
- Leary, M. R (2001), *“Introduction to Behavioral Research Methods”*, Allyn and Bacon, London.
- Merrian, S. B (1998), *Qualitative Research and case study application in Education Revised and expanded from case study research in Education*. San Francisco: Jose – Bass Publishers
- Massamba, D. P. B (1983), *“Suala la Ushairi wa Kiswahili”*, katika Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili-Fasihi namba 3. Dar es Salaam, TUKI.
- Matteru, M. L. B (1982), *The Image of Women in Tanzania oral literature: A survey katika Kiswahili*, TUKI, Dar es Salaam, juzu 49/1
- Mayoka, J. (1986), *“Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka”*, TPH, Dar Es Salaam.
- Mazigwa, S. A (1991), *“Fasihi ya Kiswahili”*, Benedictine Publication Ndanda-Peramiho.
- Mohamed, S. A (1987), *Nyota ya Rehema*, Nairobi, Oxford University press
- Muhando, P. (1982), *Nguzo mama* Dar Es Salaam, Dar Es Salaam University Press
- Muhando, P. (1974), *Talaka si Mke Wangu*, Nairobi, East African Publishing House
- Mgogo, Y. (2012), *“Utanzi wa Ushairi wa Jamii; Matumizi ya Nyimbo za Wanyiha Misibani*, Tasinifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam.

- Mnyagatwa, T. K. S. Y. S, (2009), “*Tungizi za Mnyagatwa*”, ACADEMIYA, Dar es Salaam.
- Mnyapala, M. (1965), “*Waadhi wa Ushairi*”, EALB, “Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III.
- Mnyapala, M. (1965). *Diwani ya mnyampala*. K.L.B Nairobi
- Mushegyenzi, A (2003), *Twentieth Century Literary Theory*. Kampala mkono Bookshop & publishing company LTD
- Mulokozi, M. M (2003). “*Fasihi*”, Taasis ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar Es Salaam, Chuo kikuu cha Dar es Salaam.
- Mulokozi, M. M. (1999). “*Tenzi Tatu za Kale*” Taasis ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar Es Salaam.
- Mulokozi, M. M. (1996), “*OSW 105, Fasihi ya Kiswahili*”, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.
- Mulokozi, M. M na Kahigi, K. K (1982). “*Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*”, TPH, Dar Es Salaam.
- Mulokozi, M. M na Mung’ong’o (1993). *Fasihi, Uandishi na Uchapaji*, Makala ya Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania, Uwavita.
- Muyaka bin Haji (1940). *Diwani ya Muyaka* (Mh.w. Hichens) Al-Inkishafi. Oxford University Press.
- Newman, W. L na Wenzake (2006). “*Social Research*”, sixth Edition, Boston, Pearson.
- Ndulute, C, L (1977). “*The Place of Songs in Hehe*”, Oral Literature (Uph), MA Dissertation, Dar es Salaam, University of Dar es Saalam.
- Ndungo, C. W na Mwai, W. (1991). “*Misingi ya Nadharia ya fasihi ya Kiswahili*”, Nairobi, University of Nairobi.

- Nketia, H. (1962). *The Music of Ghana*, Accra, Longman.
- Ntarangwi, M. (2004). “Uhakiki wa kazi ya Fasihi”, PhD Thesis, Augustana College, Rock Island, IL 60201.
- Ntilo, S. J (1972). “*Desturi za Wachagga*”, Nairobi General Printers.
- Omary, I. M (2011). “*Education Research*”, Concept and methods, Delah Educational Publishers ltd. Dar es Salaam.
- Omary, M. (2011), “*Siasa Katika Ushairi wa Kezilahabi; Uchunguzi wa Karibu Ndani (1998, na Dhifa (2008)*”, Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Olson, S. H (1975). “*Philosophical Implication of some Swahili Idioms*”, In Kiswahili Vol 45/2, Dar es Salaam: IKR. 32-37.
- Owhida. A. B (2006). “*Ushairi wa Kiswahili na Ushairi wa Kiarabu*”, Kufanana na kutafautiana. Tasnifu ya shahada uzamivu katika fasihi ya Kiswahili PhD (Kiswahili- fasihi) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania
- Oxford University Press (2012). *Wajaleo Diwani ya Ushairi*. Oxford University Press.
- Reed, E. (1970). *Problems of Women Liberation*, Pathfinder Press
- Robert, S. (1991). “*Wasifu wa Siti Bint Saad*”, Mkuki na Nyota Publishers. Dar es Salaam.
- Sengo, T. S. Y. M (1986), “*Fasihi Simulizi*”, *Sekondari na Vyu*, Nyanza Publication Agent, Dar es Salaam.
- Sengo, T. S. Y. M. (1985), “*The Indian Ocean Complex*”, Folktales from Pemba and Unguja, PhD Thesis, Khartoum, University of Khartoum, Unpublished.
- Shariff, I. N (1988), *Tungo Zetu*. The red sea press, trento

Shorter, A. (1969). African oral traditional, History and literature, Columbia; Columbia University.

Taasis ya Elimu Tanzania, (2003). “*Moduli ya Somo la Upimaji*”, Tathmini Utafiti, Dar es Salaam, Taasis ya Elimu Tanzania.

Taasis ya Kiswahili Zanzibar (2001), “*Malenga Wapya*”, Oxford University Press, Dar es Salaam.

Taylor, S. J & Bogdan, R. (1984). “*Introduction to Qualitative Research Methods; The Search for Mearnings*”, John Wiley & Sons, New York.

Tigiti, S. Y. M (2009), “*Sengo na Fasihi za Kinchi*”, Dar es Salaam, AER Kiswahili Research Products.

Voquez, A. S (1973). *Art and society*, New York, New York, Monthly Review Press

Wafula, R. M na Njogu, K. (2007). *Nadharia za uhakiki wa fasihi*. The Jomo Kenyatta Foundation.

Wallah, B. W (1988). “*Malenga wa ziwa kuu*”, Heinmann books Ltd. Nairobi,

Wanjara, C. L (1973). “*Standard Points on African Literature*”, Heinemann books Ltd. Nairobi.

Marejeleo ya Wasailiwa/watafitiwa

Madina Bint Ali, (2012, 2013, 2014) Nyumbani kwake Sahare- Tanga.

Mwl. Sheikh Ali Hemed Ali, barabara ya 20, Tanga.

Mwanaiki Hamdun (mrs Ali Hemed Ali), barabara ya 20, Tanga.

Jedwali 3.1: Ratiba ya Mtahiniwa

[illegible]

Jedwali 3.2: Bajeti ya Mtahiniwa

MATUMIZI	KIASI	JUMLA
Karatasi (rimu)	6@10000	60,000
Kuchapa na marekebisho (kurasa)	1000@1000	1,000,000
Kudurufu (kurasa)	2000@50	100,000
Kalamu	10@500	5000
Kamera	1@300000	300,000
Laptop	1@1000000	1,000,000
Printa	1@600000	600,000
Usafiri (mbeya- Dar- Tanga, Tanga-Dar- Mbeya mara tatu kukusanya data). Mbeya-Dar, Dar- Mbeya mara tano, kuonana na msimamizi	12 @120000	1,440,000
Kujikimu	60@50,000	3,000,000
Wasaidizi	3@100000	300000
Vifaa vya ziada	500000	500000
Kuandaa ripoti ya utafiti	1,200,000	1,200,000
Jumla		9,500,500

Chanzo: Mtafiti

VIAMBATISHI
KWA AJILI YA USAILI.

Kiambatanishi 1: Maswali ya Utafiti kwa Ajili ya Ndugu Zake Bibi Madina Ali El- Buhriy

A. TAARIFA YA MHOJIWA

Majina yako kamili.....

Umri (miaka)

Jinsia

B. Maswali.

1. Tueleze kwa ufupi unavyomfahamu Bi Madina Ali El- Buhri?
2. Bi Madina Ali El- Buhriy alipendelea kuimba ama kughani mashairi katika makuzi yake? Eleza.
3. Bi Madina Ali El- Buhriy ni Mwanamke wa Uswahilini, ni mshairi pia wa Uswahilini. Kwa maoni yako anaweza kutimiza majukumu yote kama MAMA wa Uswahilini?
4. Unafikiri mashairi aliyotunga yanawasaidiaje wanawake na watanzania kwa ujumla?

Kiambatanishi 2: Maswali kwa Ajili ya Bi Madina El- Buhriy

A.TAARIFA YA MHOJIWA

Majina yako kamili.....

Umri (miaka)

Jinsia

Maswali

1. Sanaa ya utunzi wa mashairi ulianza lini?
2. Uliingiaje katika sanaa ya mashairi?
3. Watu gani wanamchango katika kuendeleza kipaji chako cha utunzi wa mashairi
4. Dhamira za mashairi yako zinalenga makundi yepi ya kijamii?
5. Jee, una vitabu vingapi vya mashairi ambavyo vimechapishwa mpaka sasa?
6. Una madhumuni gani katika kuendeleza sanaa ya utunzi wa mashairi?
7. Jee, ni matatizo gani uliyokutana nayo katika utungaji wa mashairi? na eleza
namna ulivyokabiliana nayo
8. Nini mwito wako kwa watunzi wa sanaa ya mashairi?
9. Eleza kwa kifupi historia ya maisha yako

Kiambatanishi 3: Historia ya Bi Madina Ali El- Buhriy


Bi Madina Ali El- Buhriy ni miongoni mwa wanawake walioinukia katika taaluma ya ushairi, ni mtunzi wa mashairi katika jamii za Waswahili. Katika utafiti huu tumeamua kuchunguza nafasi ya maudhui ya tungo zake namna zinavyosawiri hali halisi ya jamii ya Uswahilini na watanzania kwa ujumla. Katika sehemu hii tumezungumzia historia yake kwa kifupi.

Ukoo wa Bi Madina Ali El- Buhriy

Asili ya ukoo wa Buhriy ni huko Oman, jimbo liitwalo Dhwaam, kutoka katika kijiji kinachoitwa Ghafur. Kijiji hiki kilivunjwa na kubaki mawe tu, watu wote waliokuwa wamebaki walihamia kijiji kingine kiitwacho Wadi Mestel ndani ya jimbo hilo hilo la Dhwaam Sheikh Mas'uud bin Khelef bin Ali bin Said bin Nassor bin Suleiman Al-Buhriy Al-Hinaiy ndiye aliyehama Oman na kuja kuanzisha makazi Pemba miaka mia mbili iliyopita akipitia Mombasa. Akiwa Mombasa alioa mke wa kabila la Mazrui, na kuzaa nae mtoto aliyeitwa Sheikh Abdallah bin Mas'uud bin Khelef bin Ali bin Said bin Nassor bin Suleiman Al-Buhriy Al-Hinaiy, nae alioa na akamzaa Sheikh Said bin Abdallah bin Mas'uud bin Khelef bin Ali bin Said bin Nassor bin Suleiman Al-Buhriy Al-Hinaiy. Sheikh Said bin Abdallah bin Mas'uud bin Khelef bin Ali akakulia hapo na kuoa. Nae akamzaa Sheikh Abdallah bin Said bin Abdallah bin Mas'uud bin Khelef bin Ali bin Said bin Nassor bin Suleiman Al-Buhriy Al-Hinaiy Sheikh Abdallah bin Said bin Abdallah bin Mas'uud bin Khelef bin Ali akakulia hapo Pemba na kuoa hapo. Nae akamzaa Sheikh Hemed bin Abdallah bin Said bin Abdallah bin Mas'uud bin Khelef bin Ali maarufu "Mwalimu Kibao" Sheikh

Hemed bin Abdallah bin Said bin Abdallah bin Mas'uud, nae aliamia Saadani Tanga na kumzaa Sheikh Ali bin Hemed bin Abdallah bin Said bin Abdallah bin Mas'uud bin Khelef bin Ali bin Said bin Nassor bin Suleiman Al-Buhriy mnamo mwaka 1889 Muharram 1307. Sasa yeye Sheikh Ali bin Hemed nae akaoa jumla ya wanawake ishirini na moja kwa nyakati tofautitofauti, alikuwa na watoto ishirini na tatu, miongoni mwa watoto hao ni pamoja na Bibi Madina Ali El-buhriy.

Kielelzo cha ukoo Bi Madina Ali El-Buhriy



Kuzaliwa kwa Bi Madina Ali El- Buhriy



Picha ya Bi Madina Ali El- Buhriy.

Kwa mujibu wa mahojiano yetu na Bi Madina Ali El- Buhriy, alizawa tarehe 06 mwezi Machi, mwaka 1952, barabara ya 12, wilaya ya Tanga, mkoa wa Tanga. Baba yake mzazi, alikuwa anaitwa Sheikh Hemed bin Abdallah bin Said bin Abdallah bin Mas'uud bin Khelef bin Ali bin Said bin Nassor bin Suleiman Al-Buhriy Al-Hinaiy - Maarufu Mwalimu "KIBAO". Shughuli kubwa ya Baba yake, ilikuwa Utabibu na Uandishi. Baadhi ya tenzi maarufu alizotunga Baba yake Sheikh Ali bin Hemed: Utenzi wa Abdirrahmani na Sufiyani, Utenzi wa Kadhi Kassim bin Jaafar, Utenzi wa Seyyidna Huseni bin Ali na Utenzi wa vita vya Wadachi kutamalaki Mrima. Pia aliandika vitabu vingi kama kitabu cha sharia za NIKAH. Tenzi hizi nyingi, zilichukuliwa na J.W.T Allen kuzitafasiri kwa Kiingereza, ambaye alipewa na Sheikh Muhammad bin Hemed, mwanawe Sheikh Hemed bin Abdallah. Tenzi hizi za familia ya Sheikh Hemed bin Abadallah, sasa zimewekwa kwenye Maktaba za

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mahali kwengineko kwenye wavupepe tafautitafauti za vyuo na za utafiti wa Kiswahili.

Elimu ya Bi Madina Ali El- Buhriy

Bi Madina Ali El- Buhriy alipelekwa madrasa kwa ajili ya kupata elimu ya Quraani. Hakuwa mvivu wa kusoma Quraani. Alimaliza juzuu kadhaa na kuweza kukhitimu kiwango alichomaliza. Alikuwa msomaji mzuri wa kasida. Kipaji hicho ndicho kilichoweza kumsaidia katika kughani tungo za kishairi hadi leo. Mnamo mwaka 1962, alianza kusoma elimu ya msingi shule ya Tanga Muslim na kukhitimu mwaka 1968. Kwa sasa ni shule ya upili, inayomilikiwa na BAKWATA. Mwaka 1969- 1970 alijiunga na mafunzo ya Uhazili, katika Chuo cha biashara cha Mtakatifu Joseph. Baada ya kumaliza, aliajiriwa na Kampuni ya Wakala wa Meli kwa nafasi ya Katibu Muhtasi. Alifanya kazi hiyo kwa muda wa miaka kumi na minane. Mwaka 1995, alijiendeleza kimasomo kwa kusomea Uwakala wa meli katika Chuo cha Wakala wa Meli Dar – Es –Salaam. Mpaka sasa yeye bado ni mwajiriwa wa Bandari ya Tanga, akiwa Wakala wa Meli.

1.1.5 Maisha ya Ndoa ya Bi Madina Ali El- Buhriy

Aliolewa tangu mwaka 1974. Ana watoto watatu, wa kiume mmoja, Yassin aliyezaliwa mwaka 1977, Wa kike wawili, Mariamu mwaka 1980, Khadija mwaka 1987. Amebahatika kupata wajukuu wawili. Feysal, mjukuu wa kwanza alizaliwa mwaka 2000, Barke mjukuu wa pili, alizaliwa mwaka 2004.

Bi Madina Ali El-Buhriy katika utunzi wa mashairi

Bi Madina Ali El-Buhriy, anahisi, alizawa na kipaji cha utunzi wa mashairi na alianza kutunga mashairi tangu akiwa shule ya msingi. Pamoja na kuzawa na kipaji

hicho, mshairi huyo, aliibuliwa kipaji chake na mwalimu wake, Ali Mafutaha, aliyemjengea msingi imara katika utunzi wa kishairi. Alianza kughani mashairi akiwa darasa la tatu (1964) katika mahafali ya shule aliyosoma. Kwa kuwa alikuwa msomaji mzuri wa Maulidi na Qaswida na kughani tungo za kishairi katika madrasa yao, hilo halikumpa taabu. Hapo ndipo ilikuwa mwanzo wa kushiriki kwake kutunga mashairi. Alitunga shairi lake la kwanza lililokuwa na maudhui ya kuisifia Shule yake na Mwalimu wake Mkuu. Hayo aliyafanya akiwa darasa la sita (1967). Katika kazi hiyo, alisimamiwa na mwalimu wake wa darasa, Ali Mafutaha. Shairi hilo liliingizwa katika mashindano na mashairi ya watu wengine katika ngazi ya wilaya, nalo lilipata nafasi ya tatu ki-Wilaya. Tangu kipindi hicho, mwalimu wake, alifurahishwa na uwezo wa mwanafunzi wake, kwa kupata mafanikio makubwa katika fani ya mashairi. Aliendelea kumhamasisha kutunga mashairi mengi zaidi yanayohusu na mambo ya kijamii, k.v, mawaidha kwa jamii, siasa, kusifia viongozi wa Chama na wa Serikali. Kwa kufanya hivyo, aliendelea kupata uzoefu mkubwa katika kutunga mashairi.

Kuanzia mwaka 1973, alitunga mashairi mengi katika Magazeti ya UHURU/MZALENDO. Alishiriki vipindi vya Mashairi Redioni (Malenga Wetu). Alishiriki Matukio maalumu ya Kitaifa. K.v. Siku ya Ukimwi Duniani, na kutunukiwa zawadi. Pia mashairi yake yalipata na bado hupata nafasi ya kuimbwa redioni. Ana matarajio ya kutunga mashairi mengi zaidi. Kaka yake, Mzee Sengo, anasubiri mswada ili autoe KITABU katika shirika lake la AERAKRP- Dar es Salaam. Shirika la Oxford, la nchini Uingereza, mwishoni mwa mwaka 2012, lilichapisha kitabu cha Ushairi, chenye baadhi ya mashairi ya Bi Madina Ali El-Buhriy , kiitwacho Waja Leo, Diwani ya Mashairi.

Shughuli nyingine anazoshiriki Bi Madina Ali El-Buhriy

Ni mwanamichezo wa Netiboli. Ameshiriki kucheza Netiboli tangu shuleni hadi kazini. Alibahatika kuwa Mwalimu wa mchezo huo na kuwa Muamuzi (Umpire) wa daraja la Ki-Mataifa. Amewahi kusimamia mashindano ya Ki- Taifa na Ki-Mataifa hapa nchini na nnje ya nchi. Kwa sasa ana kampuni yake ya kupika, kupakua na kulisha katika sherehe, warsha, semina, kupamba kumbi na kufunda wali.

Kiambatanishi 4: Baadhi ya Mashairi ya Bi Madina Ali El- Buhriy

1. MASIKINI AKIFIWA

Sio jambo majaaliwa, wala sio la kubeza

Humkuta Mwanahawa, na pia kaka Hamza

Aso uwezo kutowa, na alie sheheneza

ANA VILIO VIWILI, MASIKINI AKIFIWA

Asoweza kununuwa, uwezo wa kuagiza

Havumbui lawalawa, mchelen ni miujiza

Nambie akifiliwa, kilio atanyamaza?

ANA VILIO VIWILI, MASIKINI AKIFIWA

Hulia kaondokewa, Yule wa kumliwaza

Alomnyweshwa maziwa, na mihogo ya kupwaza

Ametoka kama hewa, safari isiyo viza

ANA VILIO VIWILI, MASIKINI AKIFIWA

Pili hulia ngekewa, hanayo imemkwaza

Dukani kwenda nunua, SANDA hajui awaza

Amkope Bwana Jiwa, au Bwana Kupaza

ANA VILIO VIWILI, MASIKINI AKIFIWA

Sikwamba hana kifuwa, uchungu kutokomeza

Na kazi yake Moliwa, aijua iso giza

Hajui pa kuvumbuwa, ndipo **HUJIGARAGAZA**

MASIKINI AKIFIWA, ANA VILIO VIWILI

2. MBEBE ANGALI LALA

Kwa mbeleko ya salala, kukicha ni mbadala

Na nguvu zako Jangala, alokujalia Mola

Zikusanye kwa jumla, mchuchuza kwa muwala

HUYO MWANA WA MWENZIO, MBEBE ANGALI LALA

Mbebe kila pahala, kwa ghani kama za chela

Uchombeze bila kula, salama iwe jumla

Akiamka mlala, itabaki lahaula

ALIVYO MWANA MWENZIO, MBEBE ANGALI LALA

Akifumbua kaola, anayo mengi masuala

Ni nani huyu kachala, chambega alonitwala?

Atang'aka kama swala, na mateke kutawala

ALIVYO MWANA MWENZIO, MBEBE ANGALI LALA

Ya urefu kama rula, hayatopimwa kwa tola

Tabu kama palahala, utadhani wewe sila

Thamani yako pagala, utupwe kwenye jalala

ALIVYO MWANA MWENZIO, MBEBE ANGALI LALA

Usitoke cha ghafula, kiduva ewe msela

Na kumbe hunacho wala, wazibebeni hila

Umcheleze kabla, yakukufika madhila

ALIVYO MWANA MWENZIO, MBEBE ANGALI LALA

2. KWEKOGA

Ukadhanja wakoga

Twevu twakutarajia, ni mja usie zuga

Kumbe kunajimwagia, mwili kunauvuruga

NAKUAPIA KWEKOGA, BALI KUNAJIMWAGIA

Utelezi wa bamia, bado umekuviriga

Kipi kilokuzuia, usisugue mabega

Mnene unaemwia, atakae kusunduga

WAONEKANA KWEKOGA, BALI KUNAJIMWAGIA

Sabuni kweitumia, wabananga wakoroga

Ni baridi wakhofia, au wakimbilia sog?

Tufahamishe jamia, ufunzwe upate iga

UNAONESHA KWEKOGA, BALI KUNAJIMWAGIA

Wewe ni mtu huria, nani atae kuroga

Na utuvu kuwania, ni vyema awache woga

Au yatakuchachia, unukue kama mzoga

NDIPO NANENA KWEKOGA, BALI KUNAJIMWAGIA

Huo mwili si bandia, kaufanani na kiga

Matunzo yalo timia, sawa kuku wa kufuga

Mayai akitamia, utunze hadi kutaga

WAONEKANA KWEKOGA, BALI KUNAJIMWAGIA

3. MWAGOMBEANI?

Sanshikwa ni butwaa, mwagombeani jamaa

Kurasa nikiambaa, namaizi zaa zaa

Nabaki kuchuchumaa, hatua nashindwa twaa

LINI YATAKAPO KWISHA, KWA SALAMA NA AMANI?

Ninazidi kuduwaa, mwili wataka pumbaa
 Kondo yenu natakaa, chini yanibwaga pwaa
 Mwangombea mishumaa, au jumu la dagaa?

LINI YATAKAPO KWISHA, KWA SALAMA NA AMANI?

Hamuwi nyote shujaa, zizi moja mka kaa
 Nzito mbavu zilo jaa, mnaruka kama paa
 Khatima ni kuzagaa, hasada kubwa kuvyaa

LINI YATAKAPO KWISHA, KWA SALAMA NA AMANI?

Lumbeni yalo komaa, yasiyo ya kunjagaa
 Za kuwaka kama taa, ufyosi kunyanyapaa
 Nyoyoni zipate kaa, chrko ziwe haa haa

NI HAPO YATAPO KWISHA, KWA SALAMA NA AMANI

Nanena mmekomaa, mafundi hii sanaa
 Kunga zimetapakaa, zafurika za zagaa
 Pomokeni nawambaa, kureya kulowavaa

NDIPO HUNENA YESHE, KWA SALAMA NA AMANI

4. HULKA YAKO PERA

Waonekana kuiva, mtini ulivyo huko
 Uzuliwo kama nguva, ni vyako hivyo vituko
 Kumbe la juu ni kava, huko ndani mchemko

KUWA NGUMU TUMBA ZAKO, NI HULKA YAKO PERA

Likiwa bichi ni hivyo, likiiva ni sumbuko
 Sifa yake ya mchovy, napata kubwa kicheko
 Mambo yake hovy hovy, kamwe sitolipa heko

KUTOIVA TUMBA ZAKE, NI HULKA YAKE PERA

Mtu akitaka ng'ata, usile klwa hamaniko

Ujue pakutafuta, kupitisha jino lako

Vinginevyo utajuta, ushikwe mfidhaiko

HIYO NI SIFA YA PERA, KUTOIVA TUMBA ZAKE

Lingekuwa la kupikwa, libandikwe kwenye jiko

Na viungo vingepakwa, vya kukaanga kwa miko

Ai!! Hilo la kumakwa, linatupa tetemeko

KUTOIVA TUMBA ZAKE, NI HULKA YAKE PERA

Walo na meno ya chuma, majivuno, miondoko

Jaribuni mtakwama, muache zenu chereko

Wajibu wangu kusema, shikeni kama zindiko

JAPO LINGEIVA PERA, NGUMU BADO TUMBA ZAKE

5. KUPIKA KWA FIGA MOJA (GAZETI LA UHURU, 24/7/1987)

Hodi kwako Bin Nyoka, majibu yangu pulika

Mabinati ulitaka, nami nimekuitika

Jibu ninaliandika, nadhani utaridhika

KWA FIGA MOJA KUPIKA, SAIDI NATATIZIKA

Umri niliofika, tangu nilipozaliwa

Sijaonapo kupika, wala sijabahatika

Sufuria kubandika, juu ikaning'inika

KWA FIGA MOJA KUPIKA, SAIDI WANIPA SHAKA

Liwe la kufinyanzika, la udongo wa kushika

Limiminwe sidhihaka, aridhini kutulika

Sifikii muafaka,, wa mlo kuandalika

KWA FIGA MOJA, KUPIKA, SAIDI SITOROPOKA

Mstari wafupika, mwishi nina pumnzika

Kwa hapo mimi natweka, shairi latamanika

Mimi dona sitopika, figa moja nikiweka

KUPIKA KWA FIGA MOJA, SIWEZI NINATAMKA

6. REHEMA MWAKANGALE

Mwanangu kaunguruma, kaniita kwa kelele

Ukumbini njoo mama, haraka usichewe

Msomaji anasoma, msiba wa MWAKANGALE

BINTI WA MWAKANGALE, AMEFARIKI REHEMA

Taarifa inasema, kaaga Binti Yule

Nikahisi kutetema, hattua nisende mbele

Nikataka kuinama, nikaona sio vile

BINTI WA MWAKANGALE, AMETUTOKA REHEMA

Nakukumbuka REHEMA, vipindi kwako si ndwele

Taarifa ukisoma, inatua hadi Hale

Utadhani nyoka moma, wafoka pasi simile

BINTI WA MWAKANGALE, AMEFARIKI REHEMA

Uhaio umekoma, mwilini haupo pale

Wadau wako twahema, umebaki mfulele

Tumeyashika matama, waume pamwe wavyele

BINTI WA MWAKANGALE, AMETUTOKA REHEMA

Tunaomba kwa KARIMA, majazo yako utwale

Yalo mazuri na mema, ulotenda siku zile

Yafike yaje tuama, kukutangulia mbele

BINTI WA MWAKANGALE, AMEFARIKI REHEMA

7. SIKU YA MAZINGIRA

Naomba zako Baraka, kwako wewe Wasitara

Dunia ulie shika, kwa kubwa zako qudura

Ni wewe ulopwekeka, mwingine huyo uchwara

TUYATUNZE MAZINGIRA, ILI YAPATE TUTUNZA

Viongozi watukuka, wameshika mduara

Sauti za wakauka, kutuhimiza dhamira

Sijawaona kuchoka, aula wao kuzira

TUYATUNZE MAZINGIRA, ILI YAPATE TUTUNZA

Tusitupe takataka, zilo ngumu na mipira

Majaa pamwe vichaka, ni mazalio ya vyura

Ni kero kuzirundika, tusijifanye wakora

TUYATUNZE MAZINGIRA, ILI YAPATE TUTUNZA

Na maradhi yanataka, sehemu isiyo bora

Malaria, kutapika, pia gonjwa la kuhara

Tusidhani kutambika, ndio njia ya kung'ara

TUYATUNZE MAZINGIRA, ILI YAPATE TUTUNZA

Misitu ilo tukuka, hata ile ya mipera

Ya zamani ilochoka, tuikate kwa ijara

Ela mipya kusimika, ni lazima kwa nusura

TUYATUNZE MAZINGIRA, ILI YAPATE TUTUNZA

Vyanzo vinavyochemka, vya maji yanayofura

Vyatufanya tunapika, hakuna wa kutukera

Sasa vipi twabweteka, kutunza kwa uimara

TUYATUNZE MAZINGIRA, ILI YAPATE TUTUNZA

Wenye viwanda pulika, wengine nyie majura
 Kemikali zamwagika, hamjui mwatukera
 Nini mnachotaka, au mpigiwe vura?

Kaditimati natweka, chondechonde MAZINGIRA
 Tuyatunze kina kaka, kina dada kirakira
 Wito natoa Tandika, mpaka kule Kagera

TUYATUNZE MAZINGIRA, ILI YAPATE TUTUNZA

8. ENZI ZAO

Enzi za SHABANI ROBATI, ni enzi zao wasusi
 Si enzi za hatihati, ela zimepita basi
 Zimepita na wakati, tumbaki kudurusi

ENZI ZILE ZA MALENGA

Zile za kina MATUNGA, zikitukosha nafusi
 Zili zikijaa kunga, safi zisizo girisi
 Zikitufunza wachanga, hazikuacha jinsi

ENZI ZILE ZA MALENGA

Zama za Bwana KANDORO ALI, na MBARUKU kasisi
 MWINYIHATIBU, ZAHORO, MDANZI na MATHIASI
 Walizitunga nyororo, tena safi kama lasi

ENZI ZILE ZA MALENGA

Za HAMDUNI Dodoma, hazikuwa na Ufyosi,
 OMARI ANNA JUMA, hakulumba za matusi
 Tungo zao ukisoma, raha khasa utahisi

ZILE ENZI ZA MALENGA

Za SHEIKH MOHD ALI, zikishinda almasi

Na pia SOBOLUALI, Rufijindie mgosi

Njema zao taamuli, zikitufundisha sisi

ZILE ENZI ZA MALENGA

Simuachi MKADARU, akichora makhususi

Za machela na za faru, kapera na za kharusi

Za sasa ni za kufuru, ukumbi sasa mweusi

ZIKO WAPI ENZI ZAO

AKIDA pia KIBAO, rudini tena upesi

GONGA, NDUMBA njoo mbio, muone hali halisi

Sasa imekuwa mwao, hatuna njema nafasi

ZIKO WAPI ENZI ZAO

Ona hata MTU CHAKE, kasusia karatasi

Hakanyi yetu makeke, tunavyokwenda kwa kasi

Tumebakia wateke, tunapakana kamasi

ZIKO WAPI ENZI ZAO

Amebaki ANDANENGA, ametuona twaasi,

Atuacha twaboronga, vurugu pasi kiasi

Hata NYOKA atachenga, hatukanyi hatugusi

ZIKO WAPI ENZI ZAO

Ni SAIDI WA MPIRA, ndie anae dadisi,

Yeye hushika bakora, kuwatisha majasusi

Ni wengi mno wakora, peke yake hatopasi

ZIMEPITA ENZI ZAO

9. JIJI BILA MAJI

Mwachekesha WAZARAMO mjidaavyo na jiji

Matao na mingurumo, mmeifunga mikwiji

Maneno mengi misemo, mabwabwaja kama uji

HILO JIJI BILA MAJI

Majumba yalo na kimo, makubwa yalo na taji

Tena kila kitu kimo, mwalitambia wenyeji

Maji kutokuwa humo, dosari ya hilo JIJI

MTANGA NATOA ZOMO, DAR JIJI BILA MAJI

Mdundiko mie simo, mwacheza kujifariji

Nyimbo na nyingi nderemo, ni mbio hadi mpiji

Mkirudi nyote pomo!, mabombani hayatoji

HILO JIJI BILA MAJI, MTANI NATOA ZOMO

WAZARAMO hata kemo, vijana hadi magwiji

Kama mpo kwenye shimo, au kwenye mafriji

Huo wenu mzizimo, WADIGOkatu hatuji

MTANI NATOA ZOMO, KWENYE JIJI BILA MAJI

Huu wangu msimamo, natoa hadi kimbiji

Ni kheri niende Himo, hakuna wa kuni hoji

Kuliko kwa WAZARAMO, hufui hata bendeji

HILO JIJI BILA MAJI, MWACHEKESHA WAZARAMO

10. KISICHOFUNGA KIPOCHI

Lebeka napiga goti, naitika bila kefu

Nasema japo kwa chati, kidogo kwa ulatifi

Huo wako utafiti, hakika umesadifu

KISICHOFUNGA KIPOCHI, KWANGU HAKIPATI HADHI

Kingejaa majinoti, ya mia na maelufu

Kisibane katikati, japo kwa chake kikufu

Kabisa sikifumbati, radhi nishike hanjifu,

HADHI HAKINA DAIMA, KISICHOFUNGA KIPOCHI

Huwezi kuwadhibiti, wenye mikono mirefu

Usiruo kama nyati, hauwapi usumbufu

Watakuacha laiti, umepasuka mapafu

KISICHOFUNGA KIPOCHI, HADHI KWANGU HAKIPATI

Hasa wale afirirti, na walio wapujufu

Kwakuwa hakizatiti, zashughulikia sarafu?

Watachocha japo njiti, wakanunue madafu

SIKIPI NG'ANDA TURUFU, KISICHOFUNGA KIPOCHI

Hadhi yake siipati, mie nina kikashifu

Kiwazi kila wakati, kinanipa taklifu

Huona walio shoti, na wasio insafu

SIKIWEKI KWENYE SAFU, KISICHOFUNGA KIPOCHI

11. BURIANI MWALIMU NYERERE

Zile shule nilosoma, ELIMU bure kupata

Nikasoma zile zama, walimu wasojinata

NI KAZI YAKO NYERERE

Kisha KAZI nikapata, pasipo moja nakama

Na jishahara la shata, nikapewa mwana mama

JUHUDI ZAKO NYERERE

Nikiumwa najivuta, DAWANI kwenda tuama

Na dakitari achota, dawa bure kwa huruma

NI WEWE HUYO NYERERE

UKABILA ukafuta, si Mngoni si Manyema

Jaluo yuwala nguta, Mdigo kwenda Sukuma

SHAURI YAKO NYERERE

Sote tunacheza ngoma, mdundiko nalo gita

KRISMASI Mwajuma, nayo IDD bwana Pita

NI MAMBO YAKO NYERERE

UMOJA kama ukuta, uloondoa lawama

Nchi nzoma ukagota, ukatanda kama hema

KWA JASHO LAKO NYERERE

Leo taa umezima, yameshakwisha mafuta

UMEMWITIKA karima, wito aliokuita

NI BURIANI NYERERE

12. MABOMU YA MBAGALA

Haikuwa makusudi, ile ni bahati mbaya

Ingekuwa kuna budi, zisingefunguka nyaya

Ni ajali sio kedi, ndugu kuwafika haya

WALE WAOMBAO SHARI, ITAZAMENI MBAGALA

Hayakuwa ya kulengwa, oneni zilivyo kaya

Majumba yameborongwa, watu kuvunjwa mataya

Na miguu kuchorongwa, wamebakia kugwaya

MSIO PENDA AMANI, ITAZAMENI MBAGALA

Ingekuwa ya dhamira, adui toka Ulaya

Kaja fosi kama jura, kushinda wale wa KEYA

Tusinge pata nusura, kubaki hata unyoya

NCHI MUOMBAO VITA, ITAZAMENI MBAGALA

Tuombeni kutwa kucha, AMANI tulozoweya

Kuparurana makucha, maneno yaso na haya

Nyoyoni tusijeficha, mwisho wake ni mbaya

NYIE MUOMBAO SHARI, ITAZAMENI MBAGALA

Pole zangu nazituma, familia zilo pwaya

Pa kukosa pa kuhema, na sasa mwawaya waya

Ombeni kwake KARIMA, subira iwe hedaya

NYIE MTAKAO VITA, ITAZAMENI MBAGALA

13. YAKUPI MASHI

Mibuyu imeshang'oka, sasa tunahamanika
 Na miziziz imezuka, madongo yamong'onyoka
 Mashimo yamechimbika, hoi tunachakachika
 KWETU MWEVU NI MASOKA, NA SASA YAKUPIMASHI

Majani yanakambuka, yote yakiwazunguka
 Yevu yakichegeleka, kwa khofu kutoiweka
 Zimenyauka na nyika, ni nyembamba ja ndakaka
 KWETU MWEVU NI MASOKA, NA SASA YAKUPI MASHI

Matawi yakikatika, kuni tunazirundika
 Au jua likiwaka, vivuli vyenu mikeka
 Imebaki kulimbika, yanapofika masika
 KWETU MWEVU NI MASOKA, NA SASA YAKUPI MASHI

Mibuyu ilojinika, narudi kwako wa peka
 Ipe palipo tindika, itunwe na malaika
 Mbadala twautaka, maombi ninayaweka
 KWETU MWEVU NI MASOKA, NA SASA YAKUPI MASHI

14. WASHAIRI KINA MAMA

Ninautunga utungo, name angani nineme
 Utungo wenye mpango, azima kutia shime
 Ni shime yenye malengo, kina mama tujitume
 KINA MAMA TUJITUME, TUSANIFU USHAIRI

Kusanifu ushairi, kina mama tusimame
 Na tusimame kwa ari, kamwe isiwe kinyume
 Kujitenga si vizuri, kina mama tusigome

KINA MAMA TUSIGOME, TUSANIFU USHAIRI

Ushairi wetu sote, si pekee wanaume
 Kwa hiyo tujikokote, ya moyoni tuyaseme
 Hima natushike kete ,kwenye bao tuiname

KINA MAMA TUINAME, TUSANIFU USHAIRI

Tuwe shime kutongoa, redioni wakasome
 Na kama wasipotoa,haki yetu tulalame
 Kina mama wa kondoa, Morogoro tuyoyome

KINA MAMA TUSIMAME, TUSANIFU USHAIRI

Wakina mama tutunge, wahariri tuwatume
 Makalani watupange, na sisi tunemeneme
 Tusiya khofu magunge, si vizuri tutuame

KINA MAMA TUSIMAME, TUSANIFU USHAIRI

Si vyema kimya tukae, wenzetu tuwatazame
 Na sisi tuyaandae, ni kama keki tuchome
 Walaji wasikatae,wale ndimi wajiume

KINA MAMA TUSIMAME, TUSANIFU USHAIRI

15. USIMPE ASOTOWA (GAZETI LA MFANYAKAZI 20/1/1993)

Kupeana ni kikowa, walitwambia mababu

Kama wapenda kupewa, na kutwaa kwa adabu

Budi ujuwe KUTOWA, hapo haitawa tabu

USIMPE ASOTOWA, UKIMPA UMETUPA

Nina anza na mwelewa, alie juu WAHABU

Tutendapo ya muruwa ,kumuomba na kutubu

Nae pia huzigawa, kutupa zetu thawabu

USIMPE ASOTOWA, UKIMPA UMETUPA

Nakwambia dada Hawa, au la kaka Ayubu

Mie nina wazinduwa, ni maneno mujarabu

Kutowa bila kupewa,hayo tena masaibu

USIMPE ASOTOWA,UKIMPA UMETUPA

Japo upate baruwa, itokayo kwa muhibu

Maneno ya kubeuwa, na makali kama shabu

Kujibu ni maridhawa, kuutimiza ni wajibu

USIMPE ASOTOWA, UKIMPA UMETUPA

Kama wapanda mauwa, ya kunikia ajabu

Magugu kupaliliwa, marefu kama sharubu

Pia inatarajiwa, mazao yaso ghilibu

USIMPE ASOTOWA, UKIMPA UMETUPA

Au umeshauguwa, maradhi ya kukusibu

Ukaenda kwenye dawa, japo dakitari bubu

Wataraji kutibiwa,yalo mema matibabu

USIMPE ASOTOWA, UKIMPA UMETUPA

Wakati unaamuwa, kutowa japo zabibu
 Kumpa alochaguwa, japo ni ndugu Twalibu
 Utataka japo kuwa, SHUKRANI iwe jibu
 USIMPE ASOTOWA, UKIMPA UMETUPA

Kama wajifaraguwa, alo mwema mahabubu
 Kuntunza kama njiwa, kunyenyekea ajabu
 Moyo atakuchefuwa, pindi akikusulubu
 USIMPE ASOTOWA, UKIMPA UMETUPA

Ukimpa ANOTOWA, humpi ANAHESABU
 Yakwamba utafikiwa, nae atakujaribu
 Japo hedaya ya kawa, fadhila kama dhahabu
 USIMPE ASOTOWA, UKIMPA UMETUPA

Tamati hapa natuwa, ni mwisho wa kuhutubu
 Maneno nilotongowa, ndio NJEMA TARATIBU
 Someni na kufunuwa, kana kwamba ni kitabu
 USIMPE ASOTOWA, UKIMPA UMETUPA

16. NYAMA YA ULIMI (GAZETI LA MZALENDU, 3/01/ 1996)

Wahenga waliyosema, kuisifu hii nyama
 Kwamba ladhaye adhima, inaishinda ya kima
 Ndipo huweka azima, buchani kwenda simama
 HII NYAMA YA ULIMI, SIJAONA UTAMUWE

Ni ka-mwamba Bwana Juma, nipe kiloilo njema
 Nono isiyo parama, au la mimi tagoma

Nenda pika na kuchoma, initoke yangu homa

HII NYAMA YA ULIMI, SIJAONA UTAMUWE

Mekoni nikatuama, na viungo chungu nzima

Mapishi ni ya kusoma, yasiyo kwenda mrama

Alonifundisha mama, na nyanya yangu Salima

HII NYAMA YA ULIMI, SIJAONA UTAMUWE

Hakaa sikuegama, na wala sikuchutama

Kwa tuo lilo salama, halisogeza stima

Hakaanga kwa adhama, ladhaye isije koma

HII NYAMA YA ULIMI, SIJAONA UTAMUWE

Mwisho jiko nikazima, bakuli zikanguruma

Mwili ulinitetema, hatenda kuu huduma

Bure mejipa zahama, kheri kupika mtama

HII NYAMA YA ULIMI, SIJAONA UTAMUWE

Mapishi nikayahama, nikataka ya kuchoma

Viungo vilo lazima, hatosa kwa takrima

Mwisho mate nilitema, kwa kuchafuka mtima

HII NYAMA YA ULIMI, SIJAONA UTAMUWE

17. SALIM ALLY KIBAO (GAZETI LA NIPASHE 28/01/1999)

Ninawajuza mahiri, huzuni imenisibu

Kuondokewa jabari, kwangu alo mahbubu

Yule wangu askari, ameitwa na wahabu

ANDANENGA NAKUJUZA, KIBAO SINACHO TENA

Kwangu kilikuwa zari, kibao cha kiarabu
 Kilicho chongwa vizuri, na fundi mstaarabu
 Kimekatika umuri, ni hoi sina jawabu

MAYOKA NINAKUJUZA, SINACHO TENA KIBAO

Kili kikinisitiri, kunienzi ja zabibu
 Japo nile kachumbari, naketi sioni gubu
 Iwapi yangu ambari, imefunga ja kitabu

SENGO NAWA NAKUJUZA, KIBAO SINACHO TENA

Yale yangu machachari, kupita kujinasibu
 Kwa matao havinjari, pasi woga wala tabu
 Nahisi yangu jeuri, imegota kwa bawabu

S. NYOKA NAKUJUZA, SINACHO TENA KIBAO

Nikitamba zanzibari, sina wa kunamba hebu
 Subutu ulete shari, ya kutaka ni sulubu
 Akikujua tayari, zinamcheza sharubu

Y.O.B. MORO NAKUJUZA, KIBAO SINACHO TENA

Macho machozi tiriri, nalia kubwa harubu
 Sikupingi ya ghafuru, kazi yako ni taibu
 Nalia yangu fakhari, imetoka taratibu

CHEKANAE NAKUJUZA, KIBAO SINACHO TENA

18. SUMU TAMU

Uliifanya dhamira, mjini ukaisaga

Kuhakiki yako dira, kila pande ukamwaga

Ukahaha kama jura, watu ukawavuruga

SUMUYO KWANGU ASALI, SISHITUKI WANGU SHOGA

Kwa hakika ni asali, nakwambia bila woga

Ni tamu tangu azali, hainichomoi kiga

Hebu tulizana tuli, kama ulivyo mzoga

SUMUYO KWANGU SUKARI, SISHITUKI WANGU SHOGA

Mimi tafanya, sukari, chaini kuikoroga

Nichanganye na binzari, vyovyote nitaviriga

Hiyoyo nile kwa ari, huku nacheza mabega

SUMUYO KWANGU NI TAMU, SISHITUKI WANGU SHOGA

Hapa itakuwa tamu, nitaramba kwa kunoga

Niile kwa shamu shamu, na huku niki-kukoga

Mie hutanidhulumu, jua kinaga ubaga

SUMUYO KWANGU ASALI, SISHITUKI WANGU SHOGA

Hata ungeroga chali, kwa fundiyo huko Duga

Uchinje kuku kwa wali, na dawa kutoka Vuga

Nakwambia bilkuli, sumu hiyo kwangu mboga

NDIPO NASEMA SISUMU, SISHITUKI EWE SHOGA

19. SILUMBI NA WAPUJUFU(GAZETI LA NIPASHE, 10/04/1999)

Kutamalaki kwa somba, kwenye situ lenye tembo
 Majilisi yake mamba, ataka yatwaa Rambo
 Mbavu nafunga kwa kamba, kichekesho hili jambo

KWA KUIKHOFU NAZAA, SILUMBI NA WAPUJUFU

Kwamba kutilo la kumba, mwitikowo wa urembo
 Lishinde bati mtumba, liloundwa kwa mitambo
 Hapo nina nena kwamba, Hau ushapigwa kumbo

KWA KUIKHOFU NAZAA, SILUMBI NA WAPUJUFU

Wataka muwinda samba, mkononi una fimbo
 Hali afyayo nyembamba, kutwa washindia hombo
 Nakwamba habi mjomba, usijetoka utumbo

KWA KUIKHOFU NAZAA, SILUMBI NAWAPUJUFU

Naona wachimbachimba, kwenye hili letu Jimbo
 Mng'ong'o wasaka nyumba, japo ya mama wa kambo
 Kwa upole si umwamba, karibu ufunzwe mambo

KWA KUIKHOFU NAZAA, SILUMBI NA WAPUJUFU

Ninakoma nipo chemba, kusubiri wenye tambo
 Waadilifu wa umba, Rufiji na Namtumbo
 Hadi kule kwetu Pemba, wanaojua malumbo

KWA KUIKHOFU NAZAA, SILUMBI NA WAPUJUFU

20. JITENGE BAIDI(GAZETI LA NIPASHE, 23/06/1999)

Pale usipo takiwa, bora ujitenge baidi

Usingoje kuambiwa, ukaitwa mkaidi

Dalili ukizijuwa, ondoka kwa ueledi

BORA JITENGE BAIDI

Vituko ukifanyiwa, vya ufyosi na udodi

Midomo kubetuliwa,minyuso iso idadi

Ya nini adha kupewa, mbele uso taradadi?

KHERI JITENGE BAIDI

Na uwe unadhuriwa, kwenda kwao kina Badi

Hali zao kuzijuwa, asubuhi ya baridi

Utakapo sema kewa, kwao umewahusudi

NI BORA UWE BAIDI

Hasha usifanye ngowa, kuwa zuzu tena zidi

Ishi kama mwananjiwa, shibe yako ni juhudi

Basi shukuru Mwelewa, mjuzi aso inadi

KHASA JITENGE BAIDI

21. NDOTO(GAZETI LA UHURU, 3/5/1991)

Nililala nikaota, safari ndefu nakwenda

Hatamu nimefumbata, za farasi si za punda

Njia nzuri ninapita, kwa furaha nina randa

NDOTO INGEKUWA KWELI, WALLAHI NINGEFAIDI

Nikafika kwenye banda, lililo na kubwa kuta

Ambazo hazikupinda, na rangize kama nta

Nikashuka kwa kudanda, mlangoni nikapita

NDOTO INGEKUWA KWELI, WALLAHI NINGEFAIDI

Mapambo ya kusokota, banda lote lilitanda

Hadi kwenye kileleta, kwa ufundi kuyaunda

Nikahisi ningegota, sinapo tena pakwenda

NDOTO INGEKUWA KWELI, WALLAHI NINGEFAIDI

Mwenyeji nilimkuta, sahibu yangu Mainda

Kasema kwa kujivuta, sautiye ya kinanda

Wasi wasi wako futa, kwetu leo hebu shinda

NDOTO INGEKUWA KWELI, WALLAHI NINGEFAIDI

Kujua hali kupenda, kama inayo matata

Hamzuja pasi inda, kwamba haina utata

Asinione kukonda, tabu moja sina hata

NDOTO INGEKUWA KWELI, WALLAHI NINGEFAIDI

Kochi lilinipakata, bila khofu nikawanda

Na meza yenye kusota, ikawekwa kwenye panda

Ya vyakula ni kashata, yaso idadi matunda

NDOTO INGEKUWA KWELI, WALLAHI NINGEFAIDI

Machapati ya kukanda, kwa yenye riha mafuta

Sharubati na mirinda, na chuzi la shata shata

Hadhani yangu mafunda, yangekula na kututa

Mkono nilipokita, nipate kumega funda

Ghafula nikajikuta, nipo juu ya kitanda

Hawaza ndoto najuta, nakudondokwa udenda

NDOTO INGEKUWA KWELI, WALLAHI NINGEFAIDI

22. USISUBIRI

Jambo jema kusubiri, subira huvuta kheri

Subira ni jambo zuri, lisokuwa na dosari

Mwishowe huwa mzuri, mambo yanapo shamiri

NAKWAMBIA SISUBIRI, NA WALA USIFIKIRI

Nasema usifikiri, usinambe ni ayari

Kwa kuwa sipendi shari, walau japo ghururi

Huu wangu ujabari, si-uuzi kwa dinari

NASEMA USISUBIRI, NA WALA USIFIKIRI

Kwa hizo zako khabari, wala sito tahayari

Kuhisi yangu saari, naigonga msumari?

Ukiniita kiburi, mimi nnitasema sori

NAJIBU SISUBIRI, NA WALA USIFIKIRI

Nishaugonga muhuri, nishaapa kwa Qahari

Na kasha nimekariri, ndani ya yangu suduri

Ninakuaga kwakheri, nishaikata amari

NASEMA USISUBIRI, NA WALA USIFIKIRI

Nasema usisubiri, sitosaili hiari

Najua wake urari, nalijua lakujiri

Sitajali ni la shairi, aula liwe la kheri

NISHASEMA SISUBIRI, NA WALA USIFIKIRI

23. MKE NA PESA

Nakuitika MAWAZO, wito ulioniita

Katika huu mzozo, ambao umeuleta

Mke pesa mzo mzo, kinacholeta matata

KATI YA MKE NA PESA, MKE HUVUNJA UDUGU

Natoa yangu mawazo, ambayo nimeyapata

Tangu kupata uwezo, wa akili kukumata

Mke Khasa ni chafuzo, udugu aweza kata

KATI YA MKE NA PESA, MKE HUVUNJA UDUGU

Waweza amini Chezo, achezee kitakita

Maelufu pendekezo, ya mapesa kuburuta

Katu hutompa tuzo, la mkeo kufuata

KATI YA MKE NA PESA, MKE HUVUNJA UDUGU

Pesa waweza azima, shida ya nduguyo Pita

Masiku chungu nzima, ikawa wamfuata

Utabaki kulalama, hayawani utamwita

KATI YA MKE NA PESA, MKE HUVUNJA UDUGU

Alokuzaa ni mama, duniani kakuleta

Kwa uwezo wa karima, akili za jaa kata

Pia waweza mhama, na ukamwita salata

KATI YA MKE NA PESA, MKE HUVUNJA UDUGU

Mkeo akisha sema, wifi yangu Zamlata

Nyumba hii angechama, kutwa kucha tunabwata

Bila hata kuinama, utamtoa mputa

KATI YA MKE NA PESA, MKE HUVUNJA UDUGU

UTENZI WA MWANAMKE NA UKIMWI

1. Bismillahi Awali ,
Twaomba kwako Jalali,
Muumba lile na hili,
Katika hii dunia.
2. Ndiwe muumba Jannati,
Ardhi na samawati,
Na vilivyo katikati,
Muumba wewe jalia
3. Kwanza tuamkiane,
Hali zetu tujuane,
Ndipo tunene mengine,
Ambayo tumeyajia.
4. Wazee shikamooni,
Vijana habari gani,
Wote mlo jukwaani,
Pamoja na jumua.
5. Na wageni karibuni,
Mhisi mko nyumbani,
Tanga penu masikani,
Kaeni bila khofia.
6. Mbele yenu mesimama,
Waume na kina mama,
Nisome yetu azma,
Sote tuloifatia.
7. Nipate kuwaeleza,
Kila nitakaloweza,
Ugonjwa unavyoanza,
Na unavyoendelea.
8. Nawaomba samahani,
Ikiwa jambo Fulani,
Limepitia machoni,
Ndio hali ya Dunia.

9. Kusudio la utenzi,
Si kashifa wala enzi,
Bali nikuweka wazi,
Ugonjwa unavyokuwa.
10. Mola ametuzushia,
Janga limetufikia,
Wengi wameangamia,
Ugonjwa kuwavamia.
11. Ugonjwa UKIMWI jina,
Mkali khatari sana,
ni lazima kupambana,
tuishi kwa salimia.
12. Ugonjwa usio dawa,
Waganga wanapagawa,
Kupata japo ingawa,
Ya kinga kutupatia.
13. Ugonjwa huu hatari,
Mkali sawa na Nnari,
Unauwa kwa chanjari,
Umepoteza mamia.
14. Watu wamepukutika,
Tulobaki ni mashaka,
Imekuwa hekaheka,
Ghofu zimetuingia.
15. Ugonjwazake dalili,
Ni kudhoofika mwili,
Japo ule vya samli,
Vyote havitokufaa.
16. Homa kali za jioni,
Zijazo ndani kwa ndani,
Hutopata afuweni,
Hadi utapojifia.

17. Kikohozi utapata,
Tena cha kuperepeta,
Umekunasa utata,
Gonjwa limeshakwingia.
18. Mwili unaharibika,
Huwa mabakamabaka,
Ujikune kama paka,
Yule asie mkia.
19. Vidonda vitakubana,
Vya siri na bayana,
Kuwashwa na kujikuna,
Kazi itakuingia.
20. Kuhara kutafatia,
Na nguvu kuishia,
21. Kumuita japo mama,
Uhaio utrakoma,
Akhera utaingia,
22. Hii leo siku yetu,
Muhimu kwa kila mtu,
Ela imetengwa kwetu,
Ujumbe tupate toa.
23. Tunaombwa wanawake,
Hatamu zetu tushike,
Za ulezi maana yake,
Jamii kuelimishia.
24. Wenyewe kinga twaweza,
Punde nitawaeleza,
Tupate kutokomeza,
Tuwe na njema afia.
25. Kwanza uasharati,
Yapasa tujizatiti,
Zisituhadae suti,
Kaburi zatuchimbia.

26. Waume makalkiti,
Wapakayo kina Beti,
Mtajikuta maiti,
Watu wanawalilia.
27. Kuwa na wapenzi wengi,
Hasa wale mashangingi,
Ni kubwa wake msingi,
Wa afya kuharibika.
28. Vyombo vya kujizuia,
Yatupasa kutumia,
Mipira kujivalia,
Kuepuka na udhia.
29. Uaminifu ni bora,
Ndoani watia fora,
mtaishi kwa nusura,
maisha kufurahia.
30. Wale uliowakumba,
Epuka kupata mimba,
Kiumbe utakitimba,
Nacho utakipasiasia.
31. Sindano vichochoroni,
Haya matibabu duni,
Ni khataru epuka,
nayo pia yachangia.
32. Vyombo vya kutahiria,
Na vile vya kutogea,
Navyo vyaeneza pia,
Yapasa kuangalia
33. Zisochemshwa vizuri,
Sindano hizo khataru,
Nazo zinaleta shari,
Vibaya kuzitumia.

34. Tujiunge na vikundi,
Pamoja tutaradadi,
Tufanye yetu miradi
Mapesa kujipatia.
35. Tutapojitegemea,
Wala havitotujua,
Mwanzo wa kivizuia,
Vishawishi kutujia,
36. Namaliza kwako,
Wewe usie kabila,
Tuepushie madhila,
Waja ulotuletea.
37. Tunusuru waja wako,
Katika hili sumbuko,
Halituweki kitako,
Tunatanga na dunia.
38. Tamati sitakhutubu,
Wakhofia kuharibu,
Ninatua masahibu,
Mbele sitoendelea.
39. Ndimi Madina mtunzi,
Ambae ni mwanafunzi,
Bado sijawa maize,
Pia malenga sijawa.

MAANA ZA MANENO YALIYOTUMIKA

Afiriti	-Mwanaharamu, mjanja, mlaghai, mdanganyifu, shetani
Ambari	- Ni aina ya madini, kitu kama nta ngumu kinachonukia, chenye rangi ya hudhurungi, kinachotokana na nyangumi baharini, huliwa ili kunenepesha na kuongeza nguvu.
Ayari	-Mwongo,laghai,mnafiki,mzandiki
Baidi	-Mbali
Bilkuli	-Hata kidogo, asilani
Danda	-Nyatia, rukia
Chanjagaa	-Mnyama/mdudu wa pwani kama chura,maji yanapokupwa na Kujaa hutokea huwa katika vishimoshimo na hutoa mwanga.
Chanjari	-Sawasawa, bila ya kupitana, kwa kufuatana, kwa safusafu
Ela	-Ila, isipokuwa, lakini
Ghafuru	-Mwenyezi Mungu Msamehevu
Ghilibu	-Geresha, hadaa
Gubu	-Kuongea kwa maneno makali,maneno mengi
Gunge	-Fundi,bingwa, gwiji, nguli
Habi	-Tulia
Hau	-Mjomba
Hedaya	-Zawadi, tuzo,tunzo, hidaya
Jabbari	-Shujaa, hodari, jasiri, jina la Mwenyezi Mungu
Jamia	-Msikiti mkubwa, Jumuiya
Jumu	-Kapu (la kawaida)
Kachala	- Vitu vinavyotupwa, taka isiyo thamani, kuchakaa, bovu

Kawa	-Kitu kilichoshonwa kwa ukili uliosokotwa kwa chane za ukindu kitumiwacho kama pambo la nyumba au kifunikio vyakula mezani/mkekani
Kkedi	-Mambo yasiyopendeza, mambo ya hila,majivuno,kiburi,makuu, dharau
Kefu	-Maringo,kinyaa, unyanyapaaji wa hali ya juu
Kiga	-Paja, pingiti,kiweo, mguu
Kiduva	-Kibyongo (kimtang'ata)
Kikowa	-Ukoo
Kondo	-Ugomvi, vita (kimtang'ata)
Kudurusi	-Kurudiarudia (yaliyosomeshwa), kujisomea
Kumba	-Kuti la kufungwa
Kupwaza	-Kuchemsha (kimtang'ata).
Kuvyaa	-Kuzaliwa (kimtang'ata).
Kuyaa	-Kulala (kimtang'ata)
Kwekoga	-Hukuoga (kimtang'ata)
Kyooni	-Msalani, chooni
Lawalawa	-Tamutamu, vyakula vitamu vitamu, mfano wa peremende
Kulimbika	-Kungojea kitu kiwe kingi kwa kukusanya kitu kidogokidogo hadi kiweKingi, kulimbikiza.
Mahabubu	-Mpenzi, mpendwa, msiri, mwandani.
Majilisi	-Mahari,baraza
Mashi	-Maringo (kimtangata)
Matao	-Kujitutumua

Mcheleze	-Mteremshe (kipemba/ kintang'ata)
Moma	-Tapakaa, sambaa, tawanyika,vavagaa
Moliwa	- Mwelewa (kimvita)
Muala	-Unyenyekevu (kipemba)
Muhibu	-Mpenzi, mwandani
Mwitikowo-	-Kofia ya kuti inayotumika kuelekea nyumba. (kintang'ata)
Mzoga	-Mfu, kibudu
Nakama	-Maangamizi
Nazaa	-Hizara
Ndwele	- Ugonjwa
Ngamizi	- Kompyuta mpakato
Ngekewa	-Bahati, sudi
Nguva	-Mnyama mkubwa wa baharini anayekula mwani, na anayenyonyesha watoto wake na umbo lake limefanana na binadamu mke.
Salata	-Mtu mwenye tabia ya kudodosa uwongo na umbea na kuusambaza huku na kule , mchonganishi, mfitini.
Shata	-Mabaki yatokanayo na mafuta ya nazi, mashudu,masimbi.
Somba	-Samaki
Sharubu	-Unywele uotao kwenye mdomo wa juu na chini ya pua ya mwanamume
Shataashata	-Mchuzi mzito wenye madikodikoujiuji mtamu
Suduri	-Mtima, moyo
Taibu	-Tamko la kuonyesha kukubaliana au kupendezwa na jambo.

Tamalaki	-Kujiachia
Taradadi	-Shughurika kwa jili ya jambo fulani
Tumba	-Mbegu ya tunda kama vile pera chungwa n.k
Udodi	
Ufyosi	-Uaneno ya utani au matusi lakini yasiyoleta ugomvi
Utuvu	-Utulivu,Hali ya kutoleta matata, hali ya kutulia, amani, uraifu
Pamwe	-Pamoja
Pomoka	-Kutulua baada ya kutulizwa
Wapweka	-Mora
Wapujufu	-Watovu au wachache wa busara
Yakupi	-Yako wapi (kimtang'ata)
Zari	-Nyuzi za dhahabu
Zuga	-Chenga, danganya, chenga